# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## VERBATIM REPORT OF

## CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, WUNDANYI CONSTITUENCY HELD AT WUNDANYI COUNTY COUNCIL SOCIAL HALL

ON

29TH, APRIL 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARING, WUNDANYI CONSTITUENCY, HELD AT WUNDANYI COUNTY COUNCIL SOCIAL HALL ON 29 APRIL, 2002.**

**Present**

Com. Prof. A. I. Salim
Com. Domiziano Ratanya

**Secretariat in Atttendance**

| | | |
|---|---|---|
| Collins Mukewa | - | Programme Officer |
| Fidelils Wangatta | - | Asst. Programme Officer |
| Grace Gitu | - | Verbatim Recorder |
| Lucy Atieno | - | Sign Language Interpreter |

**Apologies:**

Com. Kavetsa Adagala

**The meeting started at 10.30 a.m. with Com. Salim in chair.**

**Com. Salim:** Tuna matatizo ya mitambo na hata hivyo mtambo mmoja haufanyi kazi sawa sawa lakini tutaweza kuendelea. Kwa hivyo sitaki kuwachelewesha zaidi na ningeanza kwa kumuomba Mrs Mwamburi hapa kumkaribisha kiongozi wetu wa kidini.

**Mrs Mwamburi:** Asante. Nashukuru Bwana Commissioner Idha Salim na Com. Ratanya kwa nafasi hii na nazidi kuwaomba msamaha kwa kuanza kuchelewa kama mwenyeji wenu. Si makusudi yetu na ningemuomba Arch -Deacon Peter Ratanya kuja kutufungulia wazo la leo na maombi. Asante.

**ArchDeacon Ratanya:** Ningeomba msimame tuombe. Baba Mtakatifu Mwenyezi Mungu uishiye milele, tunakushukuru kwa ajili ya uzima uliyotupa, tunakushuru kwa ulinzi wako, tunakushukuru hata kwa siku hii ya leo ambayo ni kuu sana katika sehemu hii yetu ya hapa Wundanyi. Umeona Bwana ni vyema tukusanyike mahali hapa kwa ajili ya kutoa maoni yetu kuhusu urekebishaji wa Katiba. Karibu Mungu wetu utupe yale ambayo yataendelea kutusaidia na yale ambayo yataendelea kutukuza wewe. Hivyo basi tuanzapo, karibu uanze nasi utupe Bwana kuelewana vyema na uendelee kubariki kila wazo na haya tumeomba katika jina la Yesu Kristo Bwana wetu. Amen.

**Mercy Mwamburi:** Mimi ambaye nimesimama hapa ni Mercy Mwamburi, mwanakamati wa 3 Cs na ningetaka kuchukua nafasi hii kuwajulisha kwenu wale wenzangu tunafanya nao kazi hii. Karibuni wanakamati.

**Councillor Joel Haji:** Mimi kwa jina ni Councillor Joel Haji. Mimi ndio secretary wa kamati hiyo inayoshugulikia mambo ya Katiba hapa.

**Mary Mwamodo:** Na mimi jina langu ni Mary Mwamodo ni mwaakilishi wa Mbale Location.

**Crispin Mwaisege:** Na mimi ni Crispin Mwaisege mwaakilishi wa Mgange Location.

**Stephen Kalama:** Na mimi ni Stephen Kalama mwaakilishi wa Umingo Location.

**Kefa Kafuta:** Mimi ni Kefa Kafuta kutoka Kususia Location.

**Nicholas Mwadime:** Na mimi ni Nicholas Mwadime mwaakilishi wa Mwanda Location.

**Darius Mbela:** Na mimi ni Darius Mbela Mbunge wa Wundanyi, mwanakamati wa Three C's ya Wundanyi.

**Mary Chumwa:** Na mimi ni Mary Mchumwa mwaakilisha wa Werugha Location.

**Mercy Mwamburi:** Mercy Mwamburi ni Chairman wa mkao huu. Asante sana na narudisha mtambo kwa Prof. Idha Salim.

**Com. Salim:** Asante sana Mercy Mwamburi, mwenyekiti wa kamati inayoshugulikia kazi hii ya Katiba katika eneo hili, asanteni kwa kazi zenu nzuri, Mheshimiwa Bwana Mbela, ndugu na dada, mimi na mwenzangu Commissioner Ratanya hapa tumefurahi kufika hivi leo kwa kazi hii muhimu, muhimu sana ya kusikiza maoni yenu kuhusu Katiba. Bila shaka wale ambao wamekuwa wakishugulika sana kueneza elimu ya raia or civic education, na pia wanakamati ambao walikuwa hapa mbele yenu hivi sasa,

wamefanya kazi yao ya kuwaelimisha, ya kuhamasisha na kueleza mambo inayohusu Katiba. Na bila shaka District Coordinator wetu Fridah, pia amekuwa akishugulika kutoka ofisi yake hapa juu pia kuwaeleza mengi juu ya kazi hii ya urekerekebisho wa Katiba. Ni kazi muhimu na ni mara ya kwanza kabisa wananchi wa Kenya watapata nafasi ya kusema ni aina gani ya Katiba wanayotaka katika nchi hii yetu tukufu.

Kwa hivyo maoni yenu ni muhimu kwetu, na muhimu kwa nchi nzima na ni peoples' driven Constitution. Sisi wanaTume hatutaandika Katiba kutoka bongo zetu au fikira zetu. Tutategemea maoni yenu hili kwamba tukirudi tuyachungue maoni hayo, tuyasome kwa fahamu nzuri na baadaye ndio kuandika hii Katiba. Kwa hivyo bila shaka mumekuja na mawazo muhimu sana ambayo sisi tutayasikia hapa pia kuyanasa kwenye mitambo yetu ili turudi nayo na kuyachungua vizuri tukirudi kule nyumbani.

Sasa njia ambayo tutaifuata, ni kwamba tutawaleta hapa moja baada ya mmoja tukianza na yule aliyeregister au kujiandikisha kwanza na kadhalika. Tutafuata list ya registration kuwaita hapa mbeleni na mbele ya wenzenu hapa. Na kuna njia mbili ambayo itafuatwa. Kama mtu atatoa maoni yake kimdomo au kikauli, kiulimi au kwa kutupa memorandum au mswada wake. Bila shaka wengi kati yenu wameandika maoni yao katika memorandum. But yule ambaye atatoa maoni yake kimdomo tu, tutampa dakika tano. Yule mwenye memorandum, tutampa dakika tatu tu, kwa sababu memorandum yake tutaipokea na tukirudi tutaisoma. Kwa hivyo hana haja ya kuisoma hapa. Atatupa katika dakika tatu hizo, atatupa yaliyomo. Points zilizoko katika memorandum yake. "*Mimi katika memorandum yangu hapa nasemea jambo hili na hili. Juu ya jambo hili maoni yangu ni hivi na hivi na hivi. Mapendekezo yangu ni haya na haya na haya*". Na tukirudi kule you know kule ofisini tutasoma memorandum yake ikiwa ni kurasa tatu, kurasa thelathini na kadhalika. Natumai twafikiana juu ya jambo hilo, tungependa kuwapa mda mrefu zaidi. Taabu yetu ni kwamba kwanza tumeanza kuchelewa.

Pili mashalah kuna watu wengi hapa ambao wanataka kutoa maoni yao ili kwamba tumalizane na kila mmoja aliyefika hivi leo lazima tugawanye kati yenu nyote.

Tatu ni kwamba lugha yeyote yaweza kutumika. Kiingereza, Kiswahili au Kitaita. Ikiwa yeyote kati yenu anataka kusema lugha ya Kitaita, nitamwomba Mrs Mwamburi hapa au jamaa yeyote mwingine atafsiri kwa wale ambao ni wachache, labda mimi na mwenzangu kwa lugha Kiswahili. Jambo lingine la muhimu kuna haja ya diversity. Tungependelea kuwe na maoni kutoka kwa kina mama kwa wingi ya kutosha si wanaume peke yao. Pia tungependa kusikia maoni ya walemavu. Sijui kama kuna mlemavu yeyote aliyefika hivi leo ainue mkono. Ni mmoja, wawili na pia maoni yao ni muhimu. Huenda tukamuomba mmoja wao aje mbele ya wenzake wengine ili kuhakikisha kwamba maoni yake tutaipata.

Pia kukiwa na ndugu yetu yeyote au dada yetu ambaye hasikii vizuri au hasikii kabisa, tuna officer hapa Lucy ambaye ajua kueleza maelezo yote. Yuko? Yeyote kati yetu hapa ambaye hasikii vizuri au hasikii kabisa? Huenda akatokea baadaye au hapo kesho maanake tuko hapa leo na kesho. Kwa hivyo yuko tayari kutusaidia. Nafikiri ni maelezo hayo tu ambayo ningependa kuwaeleza kabla hatujaanza kusikiza maoni.

La mwisho, nataka kila mmoja wenu awe huru au asiwe na wasi wasi kabisa awe huru kutoa maoni yake jinsi atakavyo. Hakuna haja ya hofu yoyote kwamba mimi nikisema hivi labda kutakuwa na jambo au tatizo fulani. La. Tume ni huru, independent na nyinyi pia ni huru kutoa maoni jinsi mpendavyo. Kuna maswala mengi katika Katiba ambayo yastahili kuchunguliwa tena kubadilishwa au yabakie vile vile. Kwa hivyo mtakuwa na uhuru kamili kutoa maoni yenu juu ya sehemu yoyote ya Katiba au sehemu ambayo iko nje ya Katiba hivi sasa, lakini yapasa iwemo, mnavyofikiria nyinyi au wengine kati yenu. Kwa hivyo nafikiri tunafahamiana kwa ile procedure ambayo tutaifuata na ikiwa kuna swala yeyote ya kutaka jambo lolote lielezwe mimi au mwenzangu hapa tuta answer. Kuna swala lolote kabla hatujaanza? Naam karibu

**Juma Bakari:** Mimi naitwa Juma Bakari Tayo. Mimi ni mzaliwa wa hapa na ni mkaazi wa hapa, na mengi yananielea swali ni hili: Kitu nimeona ni kwamba umetupa, ni zile dakika ambazo umetwaambia ni tatu, hizo dakika tatu ungetuongezea ziwe tano kwa kila kichwa cha mtu kikiwa hapa. Ndio tunaweza kuwa sawa.

**Com. Salim:** Nafikiri nilieleza ikiwa una memorandum, maelezo yako yaweza nafikiri utaweza kutupa kwa ufupi katika dakika tatu. La, ikiwa huna memorandum Bwana Bakari, Juma Bakari unayo memorandum umeandika?

**Bakari:** ------------------------- inaudible

**Com. Salim:** La, maanake dakika tano tutakupa ikiwa huna memorandum. Basi itafaa dakika tano. Sawa?

**Bakari:** Sawa

**Com. Salim:** Haraka kabisa. Nafikiri nimeona jamaa muisilamu.

**Albert Muganga:** Mimi kwa jina ni Albert Muganga. Swali langu ni hili, nikipewa hizo dakika tano na sijamalizia yale yangu, itakuwaje?

**Com. Salim:** Jawabu ni kwamba, jaribu kati ya sasa na ukipata nafasi ya kusema au ukipewa nafasi yako ya kusema, ufocus eh fikira zako na mawazo yako yafocus hili upunguze kusema sana. Wajua muhimu kabisa ni sikueleza bali kutoa mapendekezo. Maana wengi katika sisi tunaelezwa juu ya Katiba na yaliyomo katika Katiba na bila shaka mumekuwa mkifikiria jambo hili kwa mda fulani sasa. Kwa hivyo bila shaka mawazo yenu, mapendekezo yenu ni tayari. Kwa hivyo bila kuwaeleza mengi to pendekezo, maanake sote twajua yaliyomo katika Katiba sote twafahamu hali ilivyo katika nchi yetu, kwa hivyo ni kutoa mapendekezo. Kwa hivyo dakika tano nafikiri itatosha. Na mimi sasa naogopa kwa kuwa hatuna wakati tukianza kupata maswala na kujibu maswala tuokoe wakati. Tafadhali tuache, sawa?

**Background:** ------------ inaudible

**Com. Salim:** Sawa. Asante kwa wapongeza jambo hili? Naam

**Speaker:** Tumekwisha chelewa ya kutosha na tukianza maneno ambayo umezungumza sasa, tutakuwa Tumechelewa zaidi. Aanzisha na tuende mbele.

**Com. Salim**: Kwa baraka Mwenyezi Mungu tuanze. Shukrani

**People:** Tuanze

**Com. Salim:** Tuanze na mheshimiwa Bwana Derius Mbela ambaye nikifika hapa nilimkuta na ningependa Bwana Mbela uje hapa mbele tafadhali.

**Derius Mbela:** Bwana mwenyekiti wa mkao huu ambaye ni deputy Commissioner wa kurekebisha Katib,a na Comm. Ratanya, na wananchi watukufu ambao wamefika hapa leo. Nimetayarisha memorandum lakini haijakuwa typed, kwa hivyo nitazungumza kwa uchache tu juu ya shuguli hii. Kwanza shuguli hii ya leo ni muhimu ni ya kihistoria tungetaka kuwa na Katiba ambayo inayo inagurantee amani na itaweza kutuweka kama nchi moja ya Kenya pamoja. Tunaomba vile vile, Katiba hii ambayo mtaandika isiwe ni ya kigeni, iwe ni home-grown ambayo imetokana na maoni ya wananchi ambao wako hapa. Katika nafasi ambazo ziko hapa Kenya siku ya leo, tungetaka mimi hasa, maana kila mtu hapa ana mawazo yake na hatujamkanya mtu yeyote asitoe mawazo yake ili iwe sauti ni moja. Kwa hivyo ninayosema ni yale yangu.

Ningetaka kuona nchi hii ikiogozwa na President, President ambaye atachaguliwa kutokana na wananchi wa Kenya awe ni mtu ambaye amekomaa. Somebody mature ambaye ikiwezekana amekaa kwenye bunge katika term mbili za miaka mitano yaani amekuwa kwenye uongozi wa kisiasa kwa miaka kumi. Na ikizidi awe amekwisha hitimu miaka arobaini na tano kuendelea mpaka sitini. Akipita sitini basi wakati akiwa amekaa kwa miaka kumi, atakuwa amezeeka zaidi, atakuwa senile, na nchi hii ni muhimu sana, inataka uongozi ambao una experience ya kutosha lakini ambayo vile vile, si uzee wa kupita kiasi. Tunataka mtu mwenye afya nzuri ambaye atatuongoza vizuri. Tunataka mtu mwenye tabia nzuri na ambaye si mlevi wala yule ambaye anavuta au anashiriki madawa ya kulevya. Tungetaka mtu ambaye atashinda kuwa President awe amekwisha pata 50% of the votes na apate 25% kutoka kwa province ambazo hazipungui tano. President awe accountable to the people of Kenya kupitia parliament. Hivyo ni kusema kwamba President akienda akiteleza, iwezekane kwamba aweze kupatiwa kura ya kusema bunge aina imani naye na aweze kuondoka katika kazi hiyo.

Impeachment: Tungetaka President ambaye ana uwezo wa kuweza kuappoint Prime Minister, aweze kuappoint Judges, Permanent Secretaries, Chief Executives of parastatals, Ambassadors na hata ile honors and awards. Kama kuna sifa maalum, kwa niaba ya wanakenya aweze kupeana. Vile vile mimi kwa maoni yangu naona inafaa kwamba President aweze kuwa in charge of defense. Katika hiyo nafasi ya kuwa President, afanye kwa term mbili za miaka mitano yaani a mixmum of ten years.

Na President huyo awe na Vice President ambaye atakuwa ni kama running mate. Wakati anaingia kwenye kura aweze kusema mimi nataka nichaguliwe na wanakenya kuwa President, na mwenzangu ambaye atakuwa Vice President ni fulani. Ijulikane kutoka wakati huo mpaka akishinda awe ameshinda na huyo running mate wake na aendelee mpaka amalize, isije kuwa kwamba wakienda wakikosana kwa mambo ambayo si ya muhimu ianze kutatiza utawala wa nchi ya Kenya. Nchi hii ningetaka kuona ikiwa na Prime Minister. Prime Minister ambaye atachaguliwa kutoka kwa mmoja wa wabunge atakuwa amepigania kiti cha ubunge, akachaguliwa akaingia Bunge, na akishaingia basi President aweze kumchagua. Lakini hayo yote itakuwa kwamba si President peke yake, maana too much power concentrated on an individual is very dangerous.

Iwe kwamba kama ni uchaguzi wa Prime Minister, hata wa Permanent Secretaries, na wenzake wale ambayo nilitaja, iwe kwamba kuna special committee in parliament which can counter check and vet and concur with those appointments. Basi huyo Prime Minister, President akienda akisema huyo anafaa iwe kwamba anafaa baada ya kukubaliwa kwenye Bunge. Ni muhimu iwe hivyo maana kama hakubaliki bunge inaweza kupitisha vote of no confidence na ikipitishwa hivyo, lazima atoke kwenye kazi hiyo na the entire cabinet iweze ku-resign to give room for the for the new cabinet to be appointed. Prime Minister ata-appoint ministers subject to the approval of parliament, atakuwa leader of Government Business na nilivyosema ni kwamba anaweza kupata vote of no confidence na kuweza kumuondoa. Yeye hatakuwa na time limit ya kusema kwamba ni kipimo cha miaka mitano au miaka kumi, inawezekana kwamba Prime Minister aweze kuserve under two different Presidents yaani huyu mwingine akimaliza term yake aone huyu alikuwa Prime Minister mzuri aseme nataka huyu aendelee.

Katika ile Legislature, naona kwamba kuna umuhimu tuendelee kuchagua wabunge kutoka katika constituencies. Kwa sasa ziko mia mbili na kumi lakini ziwe zikiwa reviewed occasionally. Na zaidi ya wale wa kuchaguliwa mia mbili na kumi au kile kiasi ambacho kitakuwa kimepimwa baada ya wakati fulani, kuwe na nafasi ya 10% nominated members ambao hasa itakuwa ni kujalisha nafasi ili kuwe na akina mama wa kutosha kwenye bunge, ili kuwe na wengine kama wale ambao wako physically disabled, ambao pengine hawakupata nafasi ya kuweza kuchaguliwa kwa kura, na shuguli zinginge addressing disabilities. Hivyo 10% nominated haitakuwa inatoka kwa chama kimoja. Itakuwa inategemea ule uzito ulioko kwenye bunge. Kwa mfano kama Kanu imeongoza na ina number nyingi, ile percentage yake ya wale ambao wako bunge basi kutakuwa na nominated MPs, itakuwa vile vile namba yao itakuwa ni kubwa na itafuatwa namna hiyo mpaka iwe hiyo 10%. Majina yao yatatayarishwa na hizo parliamentary parties zipelekwe kwa Electoral Commission, halafu Electoral Commission ipeleke kwa President for nomination. Naona kwamba kuna umuhimu wa kuendelea kuwa na Electoral Commission kama ilivyo sasa isipokuwa namba ambayo iko sasa ni kubwa kiasi it is just too big. Twenty one is a very big Commission. As I speak to you I happened to be a former supervisor for elections and I know what is involved. It is possible to have an Electoral Commission of nine people. A chairman and one member from every Province. The number that we have of twenty-one is a mess, it is a big money gatherer. Inatumia pesa nyingi kupita kiasi ambacho kingeweza kutumika kwa election. Ukisikia kama ni by-election, siku hizi unapata wanatumia million arobaini na tano kwa constituency moja kama hii ya Wundanyi. Na inawezekana kuweza kufanya au kusimamia kura kwa kiwango cha pesa ambacho kiko chini kuliko ilivyo. Zaidi ya hayo ningetaka kuona Judiciary ikisimamiwa vizuri zaidi. Kwa sasa watu wengi walalamika kwamba kumekuwa na too much corruption, na nafikiri ni vile kumekuwa too

much interference from various sources. Ningetaka kuona Judiciary ikiwa na Magistrate courts, High court na Supreme Court na hawa wote wakiandikwa kazi na Judicial Service Commission. Appointments hizo zitapelekwa kwa President baada ya kukubalika kwenye bunge.

Vile vile hali ambayo tuko nayo kwa wakati huu ni kwamba shuguli za kiserikali zinasimamiwa na Central Government, na zingine zinafaa kusimamiwa na Provincial Administration yaani kuanzia P.C, D.C na D.O na Chiefs. Utangaalia kwenye nchi tofauti tofauti, hata huko uingereza ambapo walikuwa wakitutawala, hutapata P.C au D.C. Ukienda hata kama ni America, ukienda kama ni Japan, kuna umuhimu wa kuhakikisha kwamba kuna merger kati ya Local Authority na Provincial Administration. Even if it is to take a period of five years, phase it out, pengine katika vijiji, kuna haja ya kuwa na Chief na Assistant Chief. Lakini aidha ya huyo Chief na Assistant Chief yeye kuelewa kazi ambazo zinafaa na responsibilities kwa wale ambao wanaongoza, ingekuwa ni muhimu awe anachaguliwa kwa kura za wananchi baada ya kila miaka mitano.

Kutakuwa na haja ya kuwa na specialized officers kuwa seconded to the District lakini hakutakuwa na haja ya kuendelea kuwa na P.C yaani Provincial Commissioner. That is an unnecessary duplication, you just need to strengthen the districts na uweze kuwapa pesa za kutosha. Kwa sasa tuna mpango ambao ni kuwapatia native. native ilikubalika kwamba iwe 5% ya pesa kutoka kwa Central Government. Lakini siku hizi imepunguzwa ikawa 2%. Kuna haja ya kuhakikisha kwamba imerudi ikawa 15%. Hiyo ni 33 billion na ieleweke kwamba hizo pesa ni pesa za wananchi. Zinaweza kutumika kwenye Central Government au zitumike kwenye nyeDistricts. Kote zinafanya kazi, ni kodi ya wananchi iweze kuhakikisha kwamba maisha ya wananchi yanakuwa mazuri zaidi.

Katika hali hiyo itakuwa ni mhimu kuongeza responsibilities za Local Authorities, iweze kusimamia barabara vizuri, elimu pengine ya primary iwe chini ya hizo Local Authorities au County Councils na miradi mingine kama ya afya, vile vile iwe chini ya hiyo.

Katiba mpya vile vile ina haja ya kusimamia au kushugulikiwa usalama. Wakati huu kwa sababu ya rushwa zikiwa nyingi, wananchi wanapata shida kubwa sana. Hii corruption imeingia sana katika security services. Inaanza kwa shuguli ndogo ya toa kitambulisho na ukitoa kitambulisho hakitoshi, unapenda kufanyiwa search kwenye nyumba yako, lakini askari ni yule yule ambaye unayemlipa na kodi zako ndiye atayefuata mpaka nyumbani kwako, uweze kumtolea pesa ambazo wewe mwenyewe huna. Unapata such is being done in the poor rural homes by Kenya Police, Administration Police even prison warders, na inakuwa ni njia moja ya kusumbua mwananchi unnecessarily. Kwanza hakuna haja ya kuwa na separate forces ya kuwa na Administration Police na kuwa na Kenya police. They should be merged, wawe properly trained na wafundishwe heshima ya mwananchi. Yule ---

Yule ambaye anawalipa mshahara, ni mwananchi ambaye analipa kodi lakini, mara nyingine anawafanya kama ambao yeye ndiye ambaye amewaandika kazi. That has got to come to an at some stage. I realize that, they is need to look at their salaries

and their living condition but it is very important to have a quick look at security situation. Kuna lingine juu ya hali ya ardhi. Hii Tumeandika memorandum na iko na Commission. Lakini kwa ufupi ni tatizo kubwa lililoko katika District hii ya Taita Taveta ni ardhi, maana 62% iko chini ya KWS Wildlife na hiyo Mtaita na Mtaveta hapati chochote kuhusikana na hiyo.

Ukienda District zingine kama Kajiado na Narok ni tajiri, sana, na wanasaidia watoto wao wanasoma vizuri lakini hapa Taita Taveta KWS wanakataa kabisa kwenda kutoa pesa kwa ile ardhi ambayo wameitumia. Kwa mfano ingetumika hata kwa kulima makonge au shuguli nyingine ya kibiashara ingekuwa muhimu sana sana kwa wananchi hawa kama wangeweza kuwa in charge of that land.

Mara nyingi tunasema kwamba ni vizuri tuhakikishe kwamba tunafanya conservation ya wildlife lakini this conservation has a cost. Haiwezi kwamba inakuwa ni sacrifice all the way, it is very important that this issue be reviewed particularly to ensure that there is clarification, proper classification of the land. I enen recall kwamba the President gave a directive, 25% of all the revevue for KWS should go to the Local Authorities, but KWS just adamantly refused. Ilifanyiwa recommendation vile vile na Omamo Commission, lakini KWS still refused. Kwa sasa mtu akiuawa na ndovu au na simba pesa ambazo zinalipwa ni shilling elfu thelathini. Lakini hizo haziji pengine mpaka baada ya miaka mitano au miaka kumi. Ingekuwa muhimu kuwa na minimum of one million ilivyofanywa recommendation, na vile vile kuhakikisha kwamba kama wanyama wa pori wakiharibu chakula au wakiua livestock, au wakileta magonjwa there should be adequate compensation so that there is a proper balance between the wildlife and the human beings. Thanks for drawing my attention to the time nashukuru sana, when this has been typed I will also send it to the commission. Nashukuru sana kwa kunisikiliza.

**Com. Salim:** Tafadhali, mwenzangu ataka kukuliza swali---------- (inaudible)

**Speaker:** Mheshimiwa nina maswali kama mawili just for clarification. Ya kwanza umesema ya kwamba Prime Minister lazima awe ni member of parliament, lakini hapa huku-clarify vizuri kama President na Vice President hata wao vile vile wawe kwanza members wa parliament. Kwa hivyo hiyo ungetwaambiwa vizuri tujue hapo kuko namna gani, na halafu kuna point inginge mheshimiwa, umesema kwamba Chiefs na Assistant Chiefs wachaguliwe na wananchi moja kwa moja, na ukasema P.C aondoke kabisa sababu hakuna kazi. Sasa tungetaka kujua kama unapendekeza tuwe na kutoka D.C kwenda chini yaani, D.C, D.O, Chief and Assistant Chief kwa hiyo Provincial administration and district ama ni P.C peke yake ungetaka aondoke na kama hawa wakiachwa ni nani watachaguliwa kwa kura? Ni kutoka D.C mpaka Assistant Chief ama D.C? Ingine ni hii mambo ya shamba. Unasema kwamba 62% imechukuliwa na KWS na ile imebaki kwa wananchi ni kidogo. Sasa ungetaka kupendekeza hii misitu ipunguzwe hili wananchi nao wapewe zaidi ama unataka kuongeza hiyo compensation. Ni kitu gani unataka kuwapatia wananchi waongezwe, ni mashamba yaondolewe kutoka kwa wanyama, wananchi wapewe zaidi, au ni compensation waongewe? Asante mheshimiwa.

**Mbela:** Asante sana, mimi naona kuna umuhimu ya kuwa na President na Vice President ambao wote ni wabunge maana

wasipokuwa wabunge itakuwa ni lazima wamutume Prime Minister aende aeleze mambo mengine kwa bunge instead of doing it directly

**Com. Ratanya**: What is the other issue?

**Mbela:** Provincial Administration. Ukiondoa P.C, arudi kwenye Central Government. Sijasema afutwe. Ni hayo maamlaka maana kuna shuguli nyingi ambazo zinakosa kufanywa because of wasting time kwa kukuwa na wakubwa ambao ni wengi sana. Ondoa P.C tuwe na officer ambaye atakuwa seconded to the Local Authority ambayo umeipa maamlaka makubwa zaidi. Kama ni P.C umekuwa naye, atakuwa in charge of all departmental heads coordinating their work. Asimamie agriculture, asimamie officer wengine kama wa forest watakuwa chini ya county council, maanake misitu ni ya wananchi. Minerals zenyewe au natural resources, zinafaa kuwa kwenye Local Authorities. Lakini direct government responsibilities, ziwe na coordinators who is the D.C assisted by the D.O. Chief atakuwa kando, hata kulipwa, atalipwa na Local authority au county council, maana kazi yake ni kwa wananchi. Hatakuwa anamfanyia D.C kazi. Atakuwa anafanyia wananchi kazi, na katika ile kazi ambaye anafanyia wananchi, wananchi ndio wataweza kumpima, amefanya vizuri? Kama amefanya vizuri basi wampigie kura. Kama hajafanya vizuri basi aondoke baada ya miaka mitano

**Com. Ratanya**: Mashamba

Mashamba ningetaka kuona kwamba, ruhusu ardhi, KWS ibakishwe na only one third yaani badala ya kuwa na 62% ingekuwa na 33%. Ile nyingine irudishwe kwa mwananchi, lakini hata hivyo na tena iganywe 33% isiwe kama sacrifice kwa Wataita peke yao, Wataita na Taveta. Kama ni sacrifice, hiyo ni kwa Kwenya nzima. Wananchi walio Kiambu na Nyeri, ardhi yao waliitumia kwa chai na shuguli zingine. Mtaita na mtaveta anataka atumie ardhi yake kwa shuguli nyingine ambazo zitaweza kumsaidia.

**Com. Salim:** Asante sana mheshimiwa kwa maoni yako, sasa tutamwita --------(inaudible) Violet, what is your second name?

**Violet:** Nyambu

**Com. Salim:** Violet Nyambu. Tafadhali utaanza kwa kutaja jina lako kwenye mic eh?

**Violet:** Mimi ninayesimama hapa ninaitwa Mrs Violet Nyambu. Nawakilisha kikundi cha Maji Safi Taita Taveta Women Group. Tume ya mageuzi ya Katiba, waheshimiwa, viogongozi, wakenya wenzetu. Maji Safi Women Group ina mapendekezo---

**Interjection:** (Prof. Salim) Samahani ikiwa una memorandum, utatupatia points zako tu maana tuko na wakati mdogo.

**Violet:** Alright

**Com. Salim:** State only the main points

**Violet:** Maji Safi Women Group ina mapendekezo ambayo inahusu mradi wao ambao ulikuwa unaendelea hapa Taita Taveta. Group hii ilianza 1987, ikiwa na wanachama mia moja, na kufikia sasa, tuko wanachama mia mbili.

**Interjection:** ----------------- inaudible

**Violet**: eh? Okay

**Com. Salim:** Tafadhali mama hatuna haja ya historia ya chama.------(inaudible)

**Violet:** Mapendekezo ya maji safi---

**Interjection:** Mama kwenye Katiba -----(inaudible)

**Violet:** Mapendekezo ya Maji Safi Women Group, muundo wa Katiba Tumeona iandikwe kizungu na Kiswahili. Hiyo ndio lugha inaeza kueleweka kwa watu wote. Kuwe na Katiba ambayo ina malengo ya baadaye. Kamati ya Katiba iongoze mikutano hiyo.

Muundo wa serikali: Serikali iwe ya majimbo kwa kiuchumi na sio majimbo ya kikabila. Serikali iwe ya mseto. Kusiwe na serikali ya chama kimoja kinachotawala lakini kiunganishwe pamoja na wale wapinzani. Serikali za mitaa zipewe uwezo na vijiji kusimamia uchumi wa mashamba na mali yaliyoko ndani yake. Kuwe na waziri mkuu na Rais wa dola kuwe na ma-Chiefs wa kuchanguliwa na raia.

Vyama vya kisiasa: vyama vya kisiasa viwe na uhuru wa kujitangaza na kujieneza kwa wananchi. Vyama vya kisiasa visiwe vya kikabila na ikiwezekana, viwe vitatu Kenya nzima. Vyama hivi vya kisiasa wasiwe wakitangatanga na kuunda vyama kwa kila wakati, wanavuruga wananchi.

Bunge: Bunge ipewe uwezo wa kutunga sheria na kuteua makatibu wakuu wa wizara na ma-professor na wakurugenzi. Wabunge wasijiongeze mishahara, iongezwe na waziri mkuu. Wabunge na madiwani maalum: Wabunge na madiwani maalum, wateuliwe na wabunge wenzao, na wakilishwe kwa kila mkoa ama wilaya sio mahali pamoja. Kuwe na uteuzi wa akina mama kwa wingi. Wanapigania. Na mtu ateuliwe kulingana na uwezo wake. Kuwe na kifungu ndani ya Katiba, Mbunge au diwani akikosa, anaweza kuondolewa bungeni, badala ya kuendelea na makosa mpaka mitano. Bunge hii iwe inafanya kazi kila siku, isipokuwa Jumamosi na Jumapili.

Wabunge wasiwe mawaziri, wawe ni wabunge peke yake kwa sababu wananchi wamewapeleka pale kufanyia wananchi kazi, na sio kufanyia Rais kazi.

Mawaziri wateuliwe na waziri mkuu. Uchuguzi wa Rais ufanywe peke yake na wa wabunge na madiwani ufanyiwe siku yake.

Usichanganywe maana wanachanganya wananchi.

Uchaguzi: uchaguzi uwe ni wa siri na kura hizo zihesabiwe pale pale kwa kila station za kupigia kura. Masanduku yawe ya glass, ili kila mtu aone jinsi kura zinavyoingia.

Akina mama wapewe nafasi kadhaa bungeni, na madiwani kwa council. Tutakuwa na nguvu zile ambazo mumesajilia. Mtu asipofaulu kupata kura, asiteuliwe tena kama mbunge maalum ama diwani, kwani wanachi hawana imani naye.
Haki ya ardhi na mali: kuwe na mpango wa jamii kuridhi ardhi na mali bila malipo yoyote kwa serikali.

**Interjection:** (Com. Salim) Samahani mama, uko na mengi ya kusema, maana wakati wako umeisha?
**Violet:** Kama imeisha Commissioner sina shida maana nina makaratasi, nitakupatia. Asanteni.

**Com. Salim:** Samahani sana Margaret Nyambu kwa kukata maelezo yako lakini kwa ajili ya idadi ya watu ilibidi tufanye hivyo lakini tunakushukuru sana kwa kutupa maoni hayo, umetupa kwa mdomo sasa na yale yaliyoko katika memorandum yako, tunakuhakikishia kwamba tutayasoma kwa makini. Na nikiendelea kama mbeleni nimesema ya kwamba kila mmoja anayekuja hapa mbele kutoa maoni yake, tafadhalini ukishamaliza, mta kuja upande huu ili kusajili majina yenu. Na mtu wetu wa tatu atakuwa ni Bwana Peter Senya. Peter Senya. Tafadhali utasema jina lako kwanza kwenye mic.

**Peter Senya:** Jina langu naitwa Peter Senya Mwachi kutoka Mgange Location, Ushangoni Sub-Location, nawakilisha kijiji cha Cheke, ........(inaudible).

Kwa hivyo mimi na kamati yangu ------------(inaudible) tungetoa maoni kufuatana na kile kitabu cha Katiba. Kwa hivyo tutawapa maoni yetu kuhusu kuunda Katiba. Maoni uwezo wa Katiba maanake ni meingi mipango yetu haikuwa imechapiliwa kwamba kwani moja kwa moja mpaka kwa serikali. Kwa hivyo mimi sina mengi ya kusema, isipokuwa nina hii karatasi yangu ambayo watu wenyewe majina yao yako hapa juu ambaye ni watu arobaini kutoka kijiji cha Cheke, Sub-location ya Ushangoni Mgange Location. Asante.

**Com. Ratanya:** Asante Bwana Peter, ungekwenda pale kwenye meza, na kuwapa hiyo memorandum yako na kutia sahihi kitabu hapo, memorandum yake. Mtu anayefuatia ni Bwana Fidelis wa Wshangoni. Asante. Sasa una memorandum au maelezo yote yako hapo. Karibu dakika tatu tu utupe mapendekezo yaliyomo asante. Jina kamili Bwana Fidelis

**Fidelis:** Jina kamili ni Fidelis Kidasi.

**Com. Ratanya:** Asante. Shukrani.

**Fidelis Kidasi:** Kwa niaba ya kijiji cha watu wa Ushangoni, jina langu naitwa Fidelis Kidasi. Mimi nafikiri sitakuwa na mengi ya kusema, mambo yetu yote yako kwenye memorandum.

**Interjection:** Jaribu kutueleza kwa ufupi mapendekezo yenu.

**Fidelis Kidasi:** Pendekezo letu sisi ni kuomba tupawe mashamba ambaye kwa sasa ni ya wanyama. Watu wengi wanataka tupate ardhi ya kumiliki. Halafu hospitali zetu tungependekeza ziwe za free kwa wananchi, bila malipo yoyote. Kwa hivyo singekuwa na mengi zaidi, ningekomea hapo. Asante.

**Com. Ratanya:** Asante Bwana Fidelis Kidasi kwa maoni yako na memorandum yako, na sawa kwa hakika nakutupa mengi. Zaidi, tungependelea aendelee lakini alitaka mwenyewe kutupa mapendekezo hayo mafupi. Na tukiendelea mbele tutamuita Bwana Mlaghui Davis. Mlaghui? Jina lako sawa au nimekosea maana---

**Mlaghui:** Mlaghui

**Com. Ratanya:** Mlaghui eh? Sawa. Bwana Mlaghui unatoka kwenye Wundanyi, unatoka Wundanyi? Lakini hapa chini kuna jina uliandika nimeshindwa kusoma tafadhali.

**Davis Mlaghui:** Kwa majina mimi ni Mlaghui Davis Mwakio. Memorandum hii ni ya kibinafsi. Katika memorandum kuna ukurasa tano kwa sababu ya dakika zilizowekwa, nafikiri nitataja mambo muhimu, na kwa vile kuna maandishi Commissioners, watachukuwa hayo wajisomee wenyewe. Katika memorandum nimeanza moja kwa moja na Katiba yenyewe. Pendekezo langu ni kwamba Katiba iwe ni Katiba ya wananchi, maana wameiandika wenyewe. Pendekezo la pili, Katiba hii isibadilishwe na mtu au watu wawili isipokuwa irudishwe kwa wananchi wenyewe walioiandika. Mtu asiifanyie marekebisho. Pendekezo la tatu, atakaye badilisha Katiba hii, itakuwa ni hatia inayostahili adabu kali bila kujali cheo, elimu au hali yoyote ile. Katiba hii ichapwe kwa Kingereza na Kiswahili. Naingia katika serikali yenyewe. Kusiwe na mtu ambaye atakuwa juu ya sheria.

Number two (eight)Rais akipatikana na kosa apelekwe mahakani akabiliane na sheria.

**Interjection:** ---------------inaudible

**Mlaghuni:** Muda wa urais uwe wa mihula miwili hata ikiwa anapendwa. Waziri mkuu akipatikana na kosa, apelekwe mahakamani fuatiliana na sheria. Number two ten, magari yapeperushaye bendera, isipokuwa gari la Rais wa Jamuhuri kuu, yawe yakichunguliwa na police wa traffic. Hii ni kwa sababu bendera inawekwa kwa ajili ya kibinaadamu badala ya heshima ya kitaifa, kufanya biashara haramu.

**Laughter**

Ni ukweli kwamba, kwa sababu bendera inapepea kwenye gari, inachukuliwa kwamba bendera hii inamlinda mhusika.

Number two (eleven), wafanyikazi wa serikali za kisayansi hawaruhusiwi kufanya biashara. Haizekani mtu kutumikia mabwana wawili sawa sawa. Number two (kumi na sita) kuwe na serikali ya kitaifa sio serikali ya kimadhehebu. Ukweli ni kwamba katika sehemu fulani fulani kumezungumzwa jambo hilo, unakuta madhehebu yanan'gan'gania uongozi na kuleta fujo. Kuwe na kazi moja kwa mtu mmoja. Number six (ten), busary ziwezikitolewa kwa wanao stahili bila ubaguzi wa aina yoyote ile, na sio kwa wale walio na uwezo. Viongozi wa kisiasa. Kiongozi yeyote awe ni mbunge, awe ni diwani ni lazima apendekezwe na wananchi wenyewe katika sehemu yoyote ya uakilishi, na wala si mtu kuzunguka na kutaka achaguliwe. Mbunge au diwani akishindwa kutekeleza wajibu wake wa uongozi, arudishwe kwa wananchi na achaguliwe kiongozi mwingine. Number two (of three) mpango wa kuwalipa viongozi wa kisiasa, wabunge au madiwani marupurupu au pension iondolewe kabisa kwa sababu itafika wakati pesa zote za serikali ziwe zinalipia pension ya viongozi na kukwamisha huduma zingine za muhimu. Kwa hivyo kupandisha mishahara ya wanasiasa, wabunge na madiwani, kusiwe inafanywa na viongozi wenyewe. Kuwe na almashauri ambayo itashughulikiwa swala hili. Ukweli ni kwamba viongozi hawa wanaposhughulikia mjadala wa kuongeza mishahara yao hupitisha haraka haraka, na kusahau kwamba wao wenyewe ni wa kufaidi, na kwa hivyo hakuna anayeshinda.

**Com. Ratanya:** Asante sana, na anayefuata ni Francis Mo-- samahani majina yao yako na taabu. Asante, karibu.

**Francis:** Kwa majina naitwa James Francis Mtoto. Mimi ninataka kuongezea yale yamezungumzwa, kufuatia nimetoa katika (inaudible). Ya kwanza ni kuhusu mbuga za wanyama. Ningependa hizi mbuga za wanyama zipunguzwe kutoka 62% zirudishwe kufikia 48%. Wanyama wa porini wawekwe ulinzi kila pahali walioko, wasiharibu mashamba ya wananchi. Tatu, kama ndovu akiharibu vyakula vya watu ama kuua mtu yeyote kuwe na malipo. Kwa mfano kama shamba ikiharibiwa chakula, mtu alipwe shillingi million moja, na mtu akuuawa na mnyama mdogo alipwe kama million mbili. Maanake, hiyo itawezesha KWS kuzuia wanyama wao wasiingie mashamba ya watu.

**Interjection:** Prof. Salim: -----inaudible

**Mlaghui:** Million moja kwa shamba zinazoharibiwa.

**Prof. Salim:** ---inaudible

**Mlaghui:** Million mbili. Pesa zinazopatikana katika mbuga za wanyama zipewe County Council ziweze kusaidia wananchi katika sehemu hii kama asilimia hamsini kwa mia. Kwa mashamba yetu ambayo yako katika District ya Taita, yapewe watu ambao wanatoka hapa katika Taita, wasipewe watu kutoka nje. Kuna watu wengine kwa mfano wako na mashamba kuanzia

acre mia tano hadi acre elfu kumi. Ikiwezekana hayo mashamba zipunguzwe kwa nusu, na hizo acre zingine zipewe wananchi ambayo hawana mashamba kabisa katika sehemu hii. Wakati wa kupiga kura, tunaomba kama ikiwezekana watu wapewe siku tatu za kuweza kufikia pale wanapopigia kura, kwa mfano walioko town, kama ni mbali siku moja ya kusafiri na ingine ya kurudi. Kwa ufupi ni hayo nilikuwa nayo.

**Com. Ratanya:** Asante sana Bwana James Francis Mtoto kwa maoni yako. Afuataye ni Bwana Calistus Mwandoe.

**Calistus Mwandoe:** Kwa majina naitwa Calistus Mwandoe natoka Wudanganyika. Nitaanzia kwa upande wa uraia. Raia ana haki ya kulindwa na kujitetea hasa upande wa ulinzi. Rais asiwe amri jeshi mkuu, na kama ma-officer wa police hawana nidhamu wafutwe. Kuhusu vyama vya kisiasa. Vyama viwe viwili, vikizidi sana viwe ni vitatu. Kila chama kiwe na mwakilishi katika bunge. Miundo na aina ya serikali. Waziri mkuu atawale nchi, na Rais awe mteuzi. Kuhusu bunge, bunge iwe na jukumu la kuchagua wakuu wa serikali. Mbunge awe anaelewa lugha ya taifa na lugha ya Kingereza vizuri. Mamlaka ya nchi. Kama mtu atachaguliwa mbunge, lazima atangaze vile alivyopata mali yake. Rais asiwe juu ya sheria, wala asiweze kuvunja bunge atakavyo, na asihudumie shughuli za mahakama . Yangu ni hayo machache. Asanteni.

**Com. Ratanya:** Asante Bwana Mwandoe. Felix Mwandigha.

**Felix Mwadigha:** Jina langu ni Felix Mwadigha kutoka hapa Wundanyi. Nilikuwa nasema walemavu waendeleze biashara zao bila kutozwa kodi yeyote Kamati ambayo inashughulikia mambo ya walemavu iwakilishwe na walemavu wawili ama watatu. Kuhusu mambo ya mashamba, wale watu ambao wamechaguliwa kupatiwa mashamba, watu watatu au wanne wawe ni walemavu.

**Prof. Salim:** -------inaudible

**Felix Mwadigha:** Kati ya hiyo idadi ambayo imetajwa na serikali. La. Kama ni watu hamsini, watu kama kumi hivi ama watano wawe ni walemavu. Wale wabunge ambao wanachaguliwa na Rais, kati ya hao wawili au watatu wawe ni walemavu.

**Laughter**

**Interjection:** (inaudible)

Kuhusu hii mambo ya rehabilitation committee. Rehabilitation committee kama hii ya kituo cha Bura, walemavu wawe wakijisimamia wenyewe, kwa sababu wale watu walio sawa sawa hawawezi kujua uchungu. Ule unaopata walemavu, kwa hivyo wanajipangia wenyewe, na ndio maana miradi ya walemavu inadidimia. Tunaomba hii mambo ya National Council For the Disabled isimamiwe na sisi walemavu, kwa sababu hizo pesa nyingi zinazotumwa hapa hatuzipati kabisa. Naomba walemavu

mahali waliko kama barabarani hivyo, wasichukuliwe na police, wawe free. Kama mlemavu anaenda na wheel chair, kweli ataweza kwenda kulala huko cell ? Awe free.

**Interjection:** (not audible).

Kama amefanya mistake asiwekwe huko ndani.

Kuhusu mambo ya barabara. Naomba Ministry of works mahali wamelima, pale kando kando watengeneze barabara, ili walemavu wawe na njia rahisi wasiangushwe na gari. Kwa hivyo—

**Laughter**

Kuhusu mambo ya lifts. Tunaomba ikiwezekana hizo lifts ziwe na kengele tena ziwe zikimwelezea yule kipofu nambari ya ghorofa ili ajuwe kule anakokwenda.

Kuhusu mambo ya simu, naomba ziwe za chini chini iwe rahisi kwa mlemavu kupiga simu. Kwa vile nimeandika memerandum yangu sitakuwa na mengi.

**Com. Ratanya:** Asante sana Bwana Felix Mwandigha kwa mapendekezo yako ambayo yanahusu walemavu, mapendekezo ambayo ni ya muhimu, tunakubali sisi katika hii Tume tumeambiwa kwamba tuhakikishe kwamba maslahi ya walemavu lazima tuyachukue. Asante. Sasa ni Bwana J. Mwalolo.

**J. Mwalolo:** Kwa majina mimi Bwana Mwalolo na mimi sina memorandum yeyote. Ndani yangu ni maoni mafupi tu, na maoni yangu mimi mwenyewe binafsi ni kwamba ninapendelea serikali iweke majimbo. Na majimbo haya yasiwe majimbo ya kikabila bali sote tuwe kama taifa moja. Na majimbo haya yawe yakitumia mali yao ya kiasili yenyewe. Na mbuga zetu za kuifadhi wanyama zipunguzwe, kama tulivyosikia watu wale wengine, kwamba 33% zipunguzwe mpaka 25%, ili mwananchi aweze kunufaika vizuri. Kwa sababu sisi wataita hapa hatuna mashamba ya kutosha. Wenyeji wa hapa mashamba yao ni 0.01, hilo ni eneo la ardhi waliopewa ambalo haliwezi kutosha. Na nyinyi wenyewe mnaona kwamba wataita wamedharauliwa kidogo.

**Intejection:** --------------- inaudible

**J. Mwaloko:** Tunadharauliwa kwa sababu ukitembea nje unakuta mkulima mwingine ana shamba hamsini acres. Mwingine ana acre mia moja au themanini. Sisi hatuna shamba hata eneo la heka tano, na eneo letu liko limetumika kama kikaratasi. Ningaliomba serikali ichunguze haya maneno kwa imani yetu sisi Wataita na Wataveta kwa jumla, kwamba tupatiwe ardhi ya kutosha tuweze kulima na tupate chakula, kwani mimi mwenyewe nina imani ninaweza kulima hata kwa matinga ikiwezekana.

Lakini uwezo huu tumenyimwa. Kwa hayo machache sina mengi zaidi ni hayo mafupi tu.

**Com. Ratanya:** Asante Bwana Mwaloko. Bwana Ngali, R. Ngali

**R. Ngali:** Jina ni Ngali M. Maoni yangu ni mafupi. Ninatoka hapa Wundanyi. Sikuja kuwakilisha kikundi bali maoni yangu binafsi. Maoni yangu ya kwanza ni kwamba mkenya awe ni mzaliwa wa Kenya au awe na asili ya Kenya. Pia ----

**Interjection:** ----------------------inaudible

**R. Ngali:** Mkenya awe ni mzaliwa wa Kenya awe raia wa Kenya. Na tuwe na serikali ya majimbo. Watu waweze kujitegemea wenyewe. Lingine ni kuhusu National Parks. Tunaomba kwamba hizi National Parks zibadilishwe, na ziwe Taita Game Reserves.

Hivyo tutaweza kunufaika kwa zile raslimali ambazo zinapatikana kwa Game Reserves. Kuhusu ardhi ile wanyama wamechukua, ipunguzwe hadi kufikia 30% badala ya 62%. Katika hali ya utawala, mamlaka ya Rais yapunguzwe. Tuwe na Rais Mkuu na yeyote asiwe juu ya sheria. Hali ya ufisadi umeongewa sana, ningesema kwamba wale ambao wamepora mali ya taifa irejeshwe. Natilia mkazo zile pesa ambazo ziko nje, zirejeshwe kwa sababu wakenya wengi hawana kazi ama ninasema kwamba Kenya haina raslimali nyingi, lakini zimeporwa na kupelekwa nchi za nje. Yangu ni hayo machache asanteni.

**Com. Ratanya:** Asante Bwana Ngali na sasa tutamwita Mwashigadi Musa Jori.

**Mwashigadi Musa:** Mimi ni Mwashigadi Musa Jori kutoka Wundanyi Location. Maoni yangu ni kuhusu County Council ya Taita Taveta. County Council ya Taita Taveta kwa Katiba hii iliyoko sasa ilinyanganywa license za vilabu. Vilabu vya pombe ya kienyeji. Na zamani wakati Council ilikuwa na vilabu, watoto wetu walikuwa wameandikwa kazini.

**Laughter**

Na bursery za schools tulikuwa tunapata kutoka kwa County Council, zikaondolewa. Kwa hivyo mapendekezo yangu, nataka County Council ya Taita Taveta irudishiwe vilabu vya pombe ya kienyeji. Watoto wetu waandikwe kazi, na bursery za schools, watoto wetu wapate.

Maoni yangu ya pili, hii inaitwa National Parks, mimi mapendekezo yangu binafsi iitwe game reserve kwa sababu hata sisi Wataita Wataveta Tumeumia sana. Mali yetu inatoka hapa Taita Taveta inapelekwa Nairobi na Mtaita anabaki maskini. Kwa hivyo yangu ni hayo. Maoni yangu ni mawili sina mengi. Asanteni sana.

**Com. Ratanya:** Na sasa ni Bwana Emmnuel Nyambu.

**Emmanuel Nyambu:** Mimi ni Emmanuel Nyambu kutoka Mwange Division, na maoni yangu nikiwa kiongozi mmoja wa viongozi wa Wataita, umeandika kuhusu taita nzima kwa jumla maana niligusa pande zote za taita. Ningependa Katiba izingatie neno moja tu katika District hii. Badala ya kwita district hii Taita Taveta, ibadilishwe kuwa Taita. Hata kwenya map ya Kenya kuna Taita District peke yake.

Halafu ya pili tuwe na serikali ya regional government ambayo ni ya majimbo. La tatu power ambayo ni nguvu ya President ipunguzwe. Iwe ni ya ceremonial activity. Tuwe na Prime Minister ambaye atakuwa akishughulikia mambo ya administration. President asiwe na uwezo mkubwa kuliko kiasi. Powers za President za kutoa directives kama sheria, bila kibali ya bunge, ziondolewe.

Hasa kuhusu mambo ya land. Kwa mfano, hivi majuzi mwezi sijui, nadhani ni March ilitangazwa katika broadcasting service kwamba amempatia Kamlesh Patni acres and acres of land. Halafu Biwott acres and acres of land. Uhuru Kenyatta acres and acres of land. Sasa hiyo ni directives. Sasa ukiwa President na unaanza kutoa directives katika districts zingine na kupeana mashamba huko, je wale waliopo katika sehemu hiyo watapata mashamba wapi?

Ukiangalia Bwana Commissioner hapa katika Taita wale Wataita ambao wamegawanishiwa mashamba ama mashamba yao yako demarcated, wameishia kwenye kituo ---------(?) sector. Kama kuna mtaita ambaye aliye na acre tano ni wachache hata kama wako ni mmoja au wawili wa bahati. Kwa hivyo we get concerned. Taitas in 5 years time watakuwa landless. Kwa hivyo tunasema kwamba directives hizo ziondolewe. Tukiangalia tena kuna sarakasi ambayo hizo directives zimefanya, alitoa directives ya traditional liquour kuondolewa na aiko na inakuwa ni criminal case ama sijui ni nini. Lakini kwa nini traditional liquor peke yake iondolewe na wakati kuna ma-whisk, ma-brandy, ma-beers na tunaendelea kuniua. Pombe ni pombe hakuna pombe iliyotofauti. Traditional liquor kama hii yetu ni pombe, kwa hivyo hiyo directive iwe revoked na pombe yetu irudishwe.

Amendments ya Constitution isiwe inafanywa jinsi hii. Iwe ikifanywa na referundum.

Automatic citizenship. Automatic citizen iwe ye Mkenya, ambaye amezaliwa Kenya, kwa mfano, Mkenya aliyezaa na mtu wa nje, lakini kusiwe na automatic citizenship ambapo mtu anakuja nakuwa citizen. Sasa mambo ya land. Land should strictly be under County Council of the district, not under Central Government. Kutambuliwa mtu awe na identity card au driving license ambayo imetoka Kenya sio nje ya Kenya. Constitution nayo iwe ndio inaangalia mambo ya military na police na prisons. Mambo ya vyama, tuwe watu wa democracy ile inayotakiwa. Kama mtu anatoka chama kingine na kama alikuwa mbunge asilazimishwe kupigania tena kiti, hapana, aende katika chama kingine au awe independent candidate. Tusije tukamfunga kamba ati tunataka kulinda chama ama tunataka kulinda nyinyi. Sasa kama Mungu anakutaka leo si unakufa? Sasa kama chama kinakufa kwa sababu kinaongozwa vibaya na watu wanataka kutoka, ya nini kufungiwa njia ya kwenda katika chama

kingine? Sasa kama nimeona chama ziko nyingi wacha nijaribu ingine wataifa wenzangu wasikie. Kuna kipande kimoja ambacho cha wataita kutoka asili lakini kimekatwa kikapelekwa Kwale na Kilifi, nacho kiko Taru mpaka Mackinon road. Kipande hicho tunataka Katiba iangalie na kirudishwe maana ni cha wataita.

**Interjection:** (not audible).

Mtito Andei bado kubadilishwa,uko kama ulivyo. Sasa kuna kitu kingine Bwana Commissioner kama utanisamehe. Mishahara ya member of parliament iwe ikijadiliwa in public. Hatujaona mtu ambaye ameandikwa kazi, halafu anajiongeza mshahara mwenyewe.

Kama bungeni iko basi hiyo watume. Tena hao watu wana ukabila huko ndani. Wanabagua Council. Wabunge hupewa pension in ten years time wakati ma-councilor hupewa in 20 years time. Hiyo ni discrimination ya hali ya juu. Kwa hivyo Katiba iangalie jambo hilo na lisahihishwe.

**Interjection:** (not audible).

Kama saa tuwe na secret ballot miaka ijauo, tusiwe na mlolongo.

**Com. Ratanya:** Asante sana Bwana Emmanuel Nyambu kwa maoni yako. Nasikitika kwamba wakati ni mfupi hatuwezi kukupa wakati mrefu zaidi kutueleza lakini natumai kwamba una memorandum hapo, na tunakupa assurance kwamba tutaisoma kwa maakini. Asante. Sasa namwita Bwana Armoga Mukala Mawori.

**Armoga Mukala:** Mimi naitwa Armoga Mkala kutoka Mwanda natumai mtanisameha hii kitu nimeandika katika lugha ya kingereza lakini nafikiri mtaelewa. Honourable Commissioners, The National park should be changed to national reserve in Taita Taveta district. Chiefs should be elected by people.

**Interjection:** -------------- (inaudible) kidogo mic ni mbaya

**Armoga Mkala:** All roads should be taken by Municipalities or County Councils. The National Park of Tsavo East and West should be divided by a settlement scheme. The Taita people should be given a piece of the land from Tsavo East and Tsavo West. Local brews, should be reinstated under the surveillance of the Local Government. The department that enjoys the national cake of Kenya is police, so something should be done about it. All religious leaders, (inaudible) should undergo mental check up ------------(inaudible) the problem in ufungamano. We should go back to the old system of education. From 8-4-4 to 7-4-2-3. The residents should enjoy all the benefits from the natural resourcesin their areas. There should be an

investigation on how outsiders were allocated these farms in Taita Taveta were to be rewarded to Taveta. The Government should give assistance to ordinary peasants to fight the free market, by providing free seeds, fertilizers and medicine. To revert to pay export, the government should revert to pay export there. Windpower should be considered as the best power if we don't have oil. District focus has never shown any development activities, it should be replaced by the County Council. Money allocated is just enjoyed by the offices at the headquarters. Corruption should start from the President to the messengers and not the other way round. The salaries for the parliamentarians should be considered by mwananchi. People who want to stand parliamentary seats should not have a bank account outside the country and should declare their wealth. If we call donors to assist, the money they give should be monitored closely. ------------(?) also the. All election petitions should be solved within six months. Because ---------------(inaudible) and we are going to another elections. It is unfair. Cases should not be in court for more than one year if they are, those concerned should be compensated by the state. The protection given not to prosecute the president should be removed. Any person who wants to vie for presidency should be screened and found free from HIV virus.

**Laughter.**

The same should apply to all Ministers, Permanent Secretaries, Ambassadors, Directors and Commissioners. We need central government both majimbo. All chiefs should be provided with mobile phones.

**Laughter.**

Pension; the minimum should be 3,000 shillings because there are people receiving 200 shillings per month.

**Interjection** by Com.

The special entertainment of the constitution, requiring for the majority to amend the constitution, should be increased from 65% to 85%. The referendum should be conducted by professionals, senior government officers and local leaders, and businessmen who are connected to the business. [Referendum tribunal and --------- (inaudible) for example the city council referendum should be conducted in Nyanza Province Coast Province Rift Valley and not people from Eastern Province because --------------(inaudible) ] tape not clear.

Automatic citizens of Kenyan be any child born of Kenyan citizen mother. If born to a Kenyan citizen should be entitled automatic citizenship and not -----------(inaudible). The discipline forces, the military and para-military, police, prison should be established by the Constitution. There should be a -----------(inaudible) established by the Constitution. The present state of bank robbery and other lawlessness is is a combination of criminals and up to date fire-arms prison where they live to the general people. The President should be the Commander-in-Chief of the Armed Forces. Political parties should be financed according to the percentage of their parliamentarians. Political parties should be banned from public funds. Before the Ministry

of Commerce imports, farm implements and inputs, it should first consult farmers and peasants. ………… (inaudible)

**Com. Ratanya:** Thank you very much Bwana Mwaura na sasa nitumuita Vigilance S. Mchigani.

**Vigilance Mchigani:** Mimi naitwa Vigilance Mchigani. Mimi nimesikia watu wamezungumza lakini, hawajataja mambo ya wanawake. Mimi kawaida nasimamia haki za wanawake. Haki ya mama ni muhimu sana kwa ujenzi wa taifa. Kwa hivyo mama aruhusiwe kuamua ni watoto wangapi anayetaka kuzaa.

Akina mama mnasikia?

**Response:** ndio.

Mama aruhusiwe ni watoto wangapi anataka kuzaa, awe na uamuzi. Nyumbani, bwana na bibi wasaidiane kazi, maana ikifika wakati wa starehe, hawatafurahi mama atakuwa amechoka sana. Mama anaanza kazi asubuhi saa kumi na moja ametoka anakamua ng'ombe anapeleka, mnajua kazi za nyumbani. Basi wasaidiane ili ikifika wakati wa jioni, wastarehe pamoja.

**Laughter**

Kuna dhuluma ambazo ni dhidi ya wanawake. Kupiga bibi. Bwana atakaye mpiga bibi ovyo afungwe kabisa na achapwe viboko akimbie vile akina mama wanakimbia.

**Laughter**

Kuna dhuluma nyingine ambazo ni psychological, yaani mama pengine anaenda kufanya biashara. Lakini bwana akikuta unazungumza na mteja, anaanza kukufikiria mambo mengine anamwaambia huyu mwanamke ni Malaya. Hiyo ni dhuluma, hatutaki kufikiriwa mambo ambayo hatufanyi. Kuna dhuluma ingine kwa kina mama. Mimi ninasimamia ofisi ingine ambayo tunaletewa kesi nyingi sana. Kuna dhuluma ya akina mama wanatumiwa nyuma na wanaume zao. Hiyo ikomeshwe kabisa na ipitishwe sheria ikipatikana hivyo mtu afungwe kabisa. Tena mwanamume akitaka kuoa bibi mwingine, tunataka ipitishwe sheria mali ile walitengeneza na yule bibi iachiwe yule bibi, na aende aanze na bibi yake mwingine, aanze upya maana hiyo mali ingine walitengeneza na bibi.

**Noise from the background.**

Naingia kwa mambo mengine ya sexual harassment. Kazini, akina mama wengi wanafanya kazi kwa shida kwa sababu ya ma-boss wao. Wanataka kufanya mapenzi nao, ati mama akitaka kupandishwa cheo, lazima walale na huyo boss. Si ndio?

Wafanye mapenzi ndipo apandishwe cheo. Akitaka kazi, afanye mapenzi aandikwe kazi. Katika magari tuemona jinsi pia kina mama wanapata hizo sexual harassment. Yaani unaona magari yamejaa abiria, mama anasimama bwana amesimama anamsukuma anataka kujibana tu karibu na huyo bibi. Na hiyo ni kuabisha huyo mama na tunaomba ipitishwe sheria, magari yasiwe yakibeba watu kupita kiasi. Ikiwa yatapita kiasi ipitishwe sheria akina mama wawe wakiketi wale watakao wakisimama wawe mabwana.

**Noise from the background**

Asante najua itauma wanaume lakini hivyo ndivyo ilivyo. Bungeni; ikiwa kutakuwako na nominations bungeni, wanawake ikiwezekana iwe one third ya wabunge au nomination iwe ya wanawake, sio wanaume, maana najua wanaume wataingia wengi. Councils tunavyotaka, iwe one third wanawake kwa sababu wakatiwa kura tunabaki nyuma. Akina mama wasibaguliwe kazini, uongozini au popote, wakiwa na vyeti vya sawa sawa. Biashara; akina wamama wengi ndio wanalinda familia siku hizi tumeona. Fee za county council zimekuwa too high kwa akina mama, hata tunaona wanabeba mizigo, mama mmoja anatoka shambani, hata hajauza amebeba mzigo, kuweka chini hivi anatakiwa pesa ama si hivyo mzigo unabebwa unawekwa ndani. Naye anaomba "niacheni niuzwe niwalipe", lakini hawataki. Tuangalie mambo ya County Council siri zao zichunguzwe.

Ninaingia uharibifu wa mazao ya akina mama wanaolima. Kuna wanyama wengi wanaoharibu mazao ya akina mama, na imewavunja mioyo hata wengine wanaona hakuna haja ya kulima na hakuna compensation yoyote. Halafu tunaingia neno ambalo linatuudhi sana sisi wanawake, ni rape. Rape cases. Rape cases zimezidi siku hizi na sijui ni kwa vile tumeanza kufundisha akina mama watoke wazungumze. Watoke wasiseme sijui maana kumekuwa na cases nyingi sana za rape. Basi tunaomba Katiba ipitishe ya kuwa mwanamume yeyote atakaye rape mama au mtoto, asifungwe, afanyiwe castration.

**Laughter**

Kama hiyo haiwezekani, afungwe maisha. Siku hizi tunaona anafungwa miaka saba, lakini tunataka afungwe zaidi, kama miaka kumi na kuendelea. Tena achapwe viboko. Nasema ni asante kwa kunisikiliza.

**Com. Ratanya:** Asante Vigilance Mchigani. Holliness Njumwa, Holliness Njumwa. Karibu.

**Holliness Njumwa:** Kwa majina naitwa Holliness Njumwa na nasimamia haki za wanawake. Ya kwanza ni kwamba mtu yeyote atakayechaguliwa na wananchi kwenda bunge au kwenda Council ahudumu kwa miaka kumi, halafu basi mwingine achaguliwe.

Pili, mwanamke akipatikana na makosa kama ya madawa ya kulevya, au na makosa yoyote yale, kifungo chake kipunguzwe, maanake wengi wao wana familia.

**Interjection from the audience.**

Mwanamume akimpiga mwanamke hadi kumuumiza, kumvunja mkono au kumvunja mguu ama jicho, kifungo chake kiongezwe kiwe zaidi ya miaka saba. Mwanamume akipatikana na rape case, badala ya kufunga miaka saba iwe miaka kumi na tano.

**Noise from audience**

Basi yangu ni hayo machache na Mungu awabariki

**Noise from the backround**

**Com. Ratanya:** Asante. Scollar Mwagiganga pia anatoka kwenye league. Naona akina mama muko sana pamoja, sijui kama ni mapya tofauti na yale yaliyosemwa na wenzako? Tofauti kidogo? Haya.

**Scollar Mwagiganga:** Kwa majina yangu ni Scollar Mwagiganga.

A) Urithi. Tunataka Katiba iweke wazi yaani bibi arithi mali ya mumewe. Bwana atakapokufa bibi ndiye atarithi hiyo mali na watoto wake.

b) Pia kila kitu kile bwana amenunua na bibi, ikiwa wataachana mali hiyo igawanywe sawa kati ya bibi na bwana. Bibi na bwana wakinunua shamba, majina yao wote yaweko kwenye Title Deed. Na wakati wa kugawanya mali, tusibague watoto wasichana. Hata kama ni shamba msichana apatiwe ili endapo ataachana na mumewe au asipo olewa, ataweza kujisaidia.

c) Upande wa pension. Ikiwa bwana atakufa akiwa kazini, na bibi yake apewe hiyo pension mpaka yeye afe, badala ya kupewa kwa miaka tano halafu inaisha.

**Interjection from Audience**

Rasilimali ya Wataita, irithiwe na ya Wataita au tutumie robo tatu na serikali itumie robo. Rasilimali hiyo kwa mfano mbuga ya wanyama pesa zinazopatikana zitusaidie kulipia watoto wetu school fees.

d) Mwisho tungetaka Katiba iandikwe kwa lugha ya Kiswahili ambayo kila mtu ataweza kusoma. Kwa hayo machache asanteni.

**Com. Ratanya:** Asante Bi Scoller na sasa namwita Bwana Ayub Mwachofi. Bwana Ayub Mwachofi Hayuko, yuko Jeferson

Ngechu? Jina hili halionekani sawa sawa hapa. Unaitwa Jeferson Ngechu. Hili hapa ni jina lako? Uliandika mwenyewe au uliandikiwa? Jeferson Mghendi? Haya.

**Jeferson Mghendi:** Kwa majina naitwa Jeferson Mghendi. Mimi kulingana na maoni kuhusu Katiba naonelea majimbo. Kwa hivyo -----------(inaudible)

**Interjection:** -------------------------------------------(inaudible).

Mimi nasema kwamba nataka majimbo kwa sababu hasa Wundanyi. Jambo lingine ni kunyanyaswa. Wageni wanaingia mbuga za wanyama na pesa zinaenda mpaka Nairobi. Wenyeji wa upande huu hawapati. Basi yangu ni hayo.

**Com. Ratanya:** Tafadhalini tuna ombi hapa kutoka kwa wenzetu hawa officers ambao wanashughulikia sana ya kunasa maneno, kama tukitulia kimya ni bora ili kwamba recording za sauti ziwe safi, na hasa kile ningezungumza sana ushawishi recording ya sauti. Tafadhalini mtulie kidogo.

**Com. Ratanya:** Sasa tunamwita Bwana Christopher Shako. Christopher Shako, yuko Christopher Shako?

**Christopher Shako:** Mwenye kiti wa Katiba, pamoja na maofisa wako na wageni wote ambao mumeudhuria hapa, ninawasalimia kwa jina la Bwana. Kwa hivyo nina maoni yangu ambayo nimeandika mimi mwenyewe ningependa kusema katika Katiba hii ya leo. Jambo langu la kwanza---

**Interjection:** Jina lako.

**Christopher:** Oh Jina langu naitwa Captain Christopher Shako kutoka Mbale Location. Jambo langu la kwanza, tunataka serikali ya majimbo katika mkoa wetu wa Pwani na Kenya nzima. Jambo la pili mashamba yetu ya Taita Taveta na Likoni turudishiwe. Watu wanaoendesha kwa wakati huu lease iondolewe kwa sababu hii lease ilitolewa na wakoloni. Jambo la tatu tunayo maji ambayo imetoka Mzima Springs yamepelekwa mpaka Mombasa, ambapo sisi Wataita hatuna maji. Tungeomba serikali kuna maji mengine ambayo yanaweza kupitishwa, yasambazwe katika Taita Taveta ili wakati wa ukame hata wakati mwingine wale ambao hawaishi katika mlima, wasipate shida ya maji.

Jambo la nne mbuga za wanyama wa pori. Tunataka zirudishwe kwa Wataita, Taita Taveta. Na pia hili jina la Tsavo National Park igeuzwe iwe Game Reserve ya Taita Taveta.

Jambo la tano, uchimbaji wa madini, watu wa kutoka nje wasiruhusiwe, bali wananchi wa Taita Taveta washirikiane kuchimba madini yao, katika ardhi yetu ya Taita Taveta.

Jambo la sita, watu wanaouwawa na wanyama wa mbuga za porini, tunataka wawe wakilipwa shilling elfu mia moja badala shilling elfu thelathini.

**Interjection by Audience**

**Christopher:** Hayo ni maoni yangu nimeandika. Elfu mia moja.

**Com. Ratanya:** hayo ni maoni yake. Kila mmoja ana haki ya kutoa maoni yake.

Namba saba, elimu ya msingi watoto waruhusiwe kusoma bure katika Kenya nzima.

Namba nane, mikutano ya D.C and Chiefs ambayo huwa inafanywa katika Taita Taveta, tunataka mwenye kiti awe mzaliwa wa Taita Taveta, sio D.C kuwa chairman katika mkutano huu wa Chiefs.

Jambo la tisa, siku ya uchaguzi watu watumie card za siri, hatutaki mlolongo. Nilikuwa na memorandum ambaye tulifanya warsha, natarajia mtaisoma. Ningependa kumalizia hapo. Asanteni sana kwa kunisikiliza.

**Com. Ratanya:** Asante Bwana Shako kwa maoni yako na tukiendelea mbele sasa namwita Bwana Davidstone Nyambu.

**Githui:** Naomba niruhusiwe kusoma hii kwa lugha ya Kingereza.

**Interjection:** Jina lako

**Speaker**: Jina langu ni James Githui kwa niaba ya SDA church. As we fully support change---

**Interjection:** -------------------------------------- (inaudible)

**James Githui:** As we fully support change of Constitution in Kenya, we would like a final Constitution document to contain our spiritual based recommendations as follows:

The Government should recognize honour and respect Seventh Day Adventist rights as stated below.

a) National cerebrations, development activities should not be programmed for Saturdays. Religious persecutions to Adventist students in schools, colleges and institutions of higher learning should be stopped. These are attending forced classes on Saturdays. Sitting for exams on Saturdays, having a parents' day on Saturday.

2) There should be an equal distribution of plots to all denominations.

**Interjection**: (Inaudible)

3) Denial of job opportunity, those in the public and the private sector to the SDA members due to their Sabbath observance should be stopped.
4) The denial of minority rights in the name of democracy when by-elections are conducted on Saturdays should be stopped.
5) The Constitution should guarantee the right to profess or not to profess the religion.
6) The right to receive or not to receive religious instructions should be guaranteed.
7) The right to participate or not in any form of worship should be guaranteed.
8) The right to refuse to take any oath controlling to personal conditions shoud be guaranteed.
9) The right to express openly personal religious beliefs or to maintain silence about such belief should be guaranteed.

The last one. The right to observe a day of worship of one choice and not to be compelled to do any work on that day. Thank you.

**Com. Ratanya:** Thank you very much na sasa tunamwita Jane Mwandoe. Jane Mwandoe?

**Jane Mwandoe:** Kwa majina naitwa Jane Mwandoe, natoka Mbale Location. Rasilimali zetu. Tunataka rasilimali zetu sote zimilikiwe na Wataita. Kwa mfano KWS.

**Interjection:** ------------- (inaudible)

**Jane Mwandoe:** Rasilimali zetu. Jane Mwandoe. Rasilimali zetu zote zimilikiwe na Wataita, kwa mfano KWS. Watalii wote ambao wanakuja kuona wanyama hapa Taita Taveta, three quarters ya huo ushuru upewe Wataita. Wageni wote wanaochimba madini hapa Taita Taveta, waondolewe tuchimbe hayo madini sisi wenyewe. Pesa zinatozwa katika KWS ni mapendekezo yangu, three quarters ya pesa hizo ziingie katika kufundisha watoto yatima. Kuanzia standard one mpaka form four hata zaidi ya hiyo.

Kwa upande wa wabunge. Wabunge wapewe kazi moja sio zaidi. Kwa mfano utasikia mbunge ndio mbunge, ni chairman wa wilaya, yaani tuseme wamechukua kazi nyingi zaidi. President asipewe mamlaka mengi asiwe above the law, na akikosa aadhibiwe. Kazi zigawanywe moja kwa moja, si kwa mfano hapa Wabunge wasichukue kazi nyingi na watoto wetu wanakosa kazi. Naomba serikali yetu iangalie masilahi ya vijana wetu.

Utawala wa ma-Chief. Ma-Chief na Mayors wachaguliwe na wananchi na wapewe miaka kumi. Nitazungumzia kuhusu mbuga za wanyama, that is KWS. Revenue sharing with KWS, is an issue of advocacy in Taita Taveta, and also reduction of the size of National Park. Tunaomba hiyo reduction ifike asilimia 30% wala si 33%. Asanteni sana.

**Com Ratanya:** Sasa tutamwita Elizabeth Waleghwa.

**Elizabeth Waleghwa:** Kwa majina naitwa Elizabeth Waleghwa mimi ndio natoa elimu ya umma katika constituency ya Wundanyi. Mapendekezo yangu ni ya kibinafsi. Pendekezo la kwanza National Park ibadilishwe iwe Game Reserve. Halafu waliopewa lease ya mashamba ya makonge ambayo ni 18.6% wasipewe tena lease, na waliopewa zikatwe huo muda. Halafu jambo lingine, pombe ya kienyeji ihalalishwe halafu watu wawe wakilipa kodi.

**Response:** noise

Mwenye kiti wa County Council na Mayor wawe wanachaguliwa na wananchi. Halafu wabunge wasiwe mawaziri, wawe wanafanya kazi moja. Halafu Rais asiwe wadhafu wa kuteuwa watumishi wa umma, na mawaziri, hawa wawe watu wakiajiriwa. Mawaziri waajiriwe kulingana na taaluma zao. Kama ni afya awe amesomea mambo ya udaktari.

Jambo lingine kiwango cha kulipa wanaouwa na wanyama iongezwe na hatua ichukuliwe. Halafu pia watu wasilazimishwe kula nyama mbichi ambapo wameua huyo mnyama wakiwa wanatunza mimea yao isiharibiwe. Vyeti vya kuchimba madini hapa Taita, viwe vinatoka County Council na pahali penye madini wenyeji wa eneo hilo wajulishwe.

Jambo lingine County Council isiwe inabomoa vibanda vya watu wakati wanafanya biashara zao, bila ya kumpa muda wa kutoa vitu vyao. Pia vile wananchi wamepewa 11.9% lile shamba la wanyama, ili tupate ardhi ya kutosha. Yangu ni hayo asanteni.

**Com. Ratanya:** Asante Elizabeth Waleghwa na sasa tunamuita Bwana Jimmy Mwandigha.

**Jimmy Mwandigha:** Jina langu ni Jimmy Brown Mwandigha. Maoni yangu ni kama yafuatayo. Nataka kuwe na creation ya post ya Prime Minister. Huyu awe leader of the government, ajibu maswali katika Parliament na handle any kind of duty directed by the government. Halafu nataka tuwe na restoration of the two systems of Parliament. Tuwe na ile Senate yaani Upper house na pia tuwe na Lower house. Hizi zote mbili zipewe uwezo wa kufanya appointments zifuatazo: Cooperative Chiefs, Permanent Secretaries, Attorney General, Chief Justice, Governor of Central Bank, Commissioner of police na Electoral Commissioner Chairman. Halafu tunataka Constitutional court ibuniwe. Kazi yake iwe ni handle any interpretation na ihakikishe kwamba ikiwa mtu ameshtakiwa na hana uwezo wa ku-hire services of the lawyer, serikali itoe legal aid na hiyo iwe Constitutional right.

Mayors na Council Chairman wawe elected directly na wananchi. Tunataka Constitution itoe maximum number of government ministries na hii mambo ya Cabinet reshuffling iwe outlawed kabisa, isifanywe kila wakati. Halafu mambo ya sovereignty. Hatutaki mambo ya kusikia kwamba kuna World Bank IMF inaleta mambo kama retrenchment. Kenya ni uhuru inaweza kupanga mambo yake kwa kuaangalia hali ya uchumi wake. Kwa kumalizia nitasema tuko na hii tunaita Professional Bodies kama Law Society of Kenya, ama Kenya Nation Union of Teacher zipewe recognitiont na respect ili ziwe involved katika any issues that pertain to their services. Yangu ni hayo.

**Com. Ratanya:** Asante bwa Mwandigha na sasa Chola Charles.

**Chola Charles:** Kwa majina naitwa Charles Chola na napendekeza mambo yafuatayo.

1. Kwa sababu tunatengeza Katiba kitu cha kwanza ningependa kirekebishwe hapa ni kuwa Katiba hii ya sasa hatujui ni ya nani. Ningependekeza katika Katiba hii, Kenya iwe government of the people and by the (inaudible) are by the people.
2. Pendekezo langu la pili ni uchaguzi wa Rais usifanywe pamoja na ule wa wabuge.
3. Halafu kitu ya tatu, ningependekeza Katiba ambayo itaondoa mamlaka ya Rais kabisa na kuyaweka kwa bunge.
4. County Council ipewe mamlaka ya kufanya ushuru wowote ule bila kupeleka kwa serikali.
5. Muda wa wabunge usizidi miaka kumi, na kila kipindi kiwe cha miaka tano kama Rais.
6. Katiba ambayo itakuwa na uakilishi mkubwa wa akina mama.
7. Nyingine wabunge wote wachaguliwe na wananchi, tusiwe na nominated MPs.
8. Mkenya yeyote aliyefikia miaka kumi na nane apewe kitambulisho free of charge na awe mpiga kura automatic.
9. Mfumo wa elimu ya 8-4-4 iondolewe na kuchukuwa mfumo ule wa zamani wa 7-4-2-2.
10. Electoral Commission ichaguliwe na wabunge.

11. President atakapo-retire apewe pension. Asipewe security, governing allowances yoyote, maana amekuwa raia.
12. Elimu ya nursery kutoka nursery mpaka chuo kikuu, mpaka university iwe ni free.
13. Halafu la kumi na tatu, ni kuhusu ardhi. District zipewe mamlaka yote ya kutatua mambo ya ardhi bila kupitia Nairobi. Kwa hayo machache asante sana.

**Com. Ratanya:** Asante Bwana Charles chola, Presence Jacob, hayuko? Bwana Maghanga. Wisdom Maghanga? Karibu.

**Wisdom Maghanga:** Kwa majina ni Wisdom M. Maghanga. Maoni yangu ni juu ya Taita Taveta County Council. County Council hii imenyimwa haki zake. Mali ya haki iliyoko katika Taita Taveta, ninapendekeza iwe chini ya County Council. Kwa mfano wanyama wa pori walioko katika Taita Taveta wawe chini ya County Council, 75% iwe kwa County Council, 25% iwe

kwa serikali. Madini inayochimbwa katika Taita Taveta 75% ya kodi iwe ya Taita Taveta, 25% iende kwa serikali. Shamba zilioko katita Taita Taveta lease ziondolewe, na ziwe chini ya County Council. Uchaguzi wa Rais uwe kando na wa wabunge. Usichangaywe, ukiwa pamoja unavuruga wananchi. Rais atawake kwa muda wa miaka kumi, vile vile wabunge, na halafu kuchaguliwe wengine. Hayo ndio maoni yangu. Asanteni.

**Com. Ratanya:** Asante Bwana Maghanga, Bwana Jeffersom M Kalendo

**Jefferson Kalendo:** Kwa majina yangu naitwa Jefferson Kalendo kutoka Wundanyi. Mapendekezo yangu ni kuhusu mashamba. Wananchi wataita waliofikisha umri wa miaka kumi na nane, wakati wa kupatiwa kitambulisho, pia wapewe ardhi ya kiasi cha chini, kama acre 5, walipewa ardhi--------- (inaudible) ili waweze kujitegemea. Hii itapatikana kutokana na ya Wataita iliyokaliwa na wanyama. Na wale wote ambao pia hawana kazi wapatiwe ili wajiendeleze kupitia kilimo ili tuondoe umaskini.

Elimu: Elimu inapaswa kuwa ya bure hadi kidato cha nne. Huu mzigo ubebwe na serikali. Matibabu, matibabu yawe ya bure kabisa kutoka kwa serikali ya Kenya. Wafanyi kazi waliodhulumiwa, mahakama maalum iundwe ili iangalie matatizo ya wafanyi kazi hasa wale wa serikali kwa maana wengi wao wameteswa sana na serikali. Mbuga za wanyama, mbuga hizi zipunguzwe ili wananchi wa Taita waweze kumiliki kwa kiasi robo tatu ya ardhi yao na wanyama watengewe robo kumi. Yangu ni hayo kwa ufupi.

**Com. Ratanya:** Asante Bwana kalendo. Pauline Chao Kitato.

**Pauline Chao:** Majina yangu naitwa Pauline Chao Kitato. Maoni yangu ni juu ya urithi. Wanawake wawe na uwezo wa kurithishwa mali sawa sawa kama shamba, pesa, mali yoyote kwa jumla, baada ya kifo cha mumewe. Katika uchaguzi, uchaguzi wa bungeni, Rais awe ni mtu ana family. Rais akiwa mume, naibu wake awe mwanamke.

**Interjection**: From audience.

Bunge iwe na idadi sawa ya wanawake kwa wanaume.

**Interjection:** -----------------inaudible

**Pauline:** ehe? Bunge iliyo sawa sawa na idadi ya wanawake na wanaume. Kwa hayo machache, asanteni.

**Com. Ratanya:** Thank you Paulini Chao Kitato, sasa Bwana Nzae Mwandini. Nzae Mwandini? Hayuko? Wakilemba Mwachuma. Mwakilemba Mwachuma? Festus Mugambwa.

**Festus Mugambwa:** Mimi jina langu ni Festus Mugambwa, natoka Wundanyi sub-location na nina wazo moja tu kuhusu marekebisho ya Katiba. Ni jambo ambalo linanikera sana, nalo linahusu economic status ya common man, mwananchi wa kawaida. Kwa hivyo ningeomba kwamba wakati tunafikiria marekebisho ya Katiba, tusingatie sana mambo ya kuendeleza economic status ya common man na mimi nafikiria hii itawezekana kukiwa na regionalism, hasa katika district level nayo iwe huru. Hiyo ni kama serikali ya kibinafsi, County Council au regionalism lakini manufaa yake ni kwamba itamiliki rasilimali iliyoko katika nchi. Kwa hivyo mimi naona kwamba jambo ambalo tutazingatia zaidi ni proposal hiyo ya regionalism kutoka district level, na wananchi wa pale wapewe mamlaka ya kumiliki mali zao, sio watu kutoka Nairobi au mahali popote. Asante.

**Com. Ratanya:** asante Bwana Mughambwa na sasa namuita Bwana Ronald Mwakuruma.

**Ronald Mwakuruma:** Jina langu ni Ronald Mwakuruma kutoka Wundanyi location. Maoni yangu juu ya Katiba yetu mpya ya Kenya, ningependelea mamlaka ya Rais yapunguzwe ili akifanya kosa adhibiwe kama wengine.

La pili masomo kwa shule za msingi kuanzia darasa la kwanza hadi darasa la nane yawe ya bure, sababu watoto wengi wamekosa masomo kwa kukosa pesa.

La tatu, hosipitali ziwe za bure sababu watu wengi wanakufa kwa kukosa pesa za kununua madawa.

La nne, makanisa yamekuwa mengi sana na yanatatiza wananchi. Hata yamekuwa kama biashara. Ikiwezekana yapunguzwe.

La tano, misitu yetu irudishiwe wananchi wenyewe kwa sababu inalindwa, na bado miti inazidi kukatwa. Yangu ni hayo tu.

**Com. Ratanya:** Asante, na sasa namuita Bwana Joel Haji. Councilor Joel Haji.

**Councilor Joel:** Mimi kwa jina ni Councilor Joel Haji na nilikuwa na memorandum ya viongozi wa Mbale na nitajaribu kuzungumza na kutia mkazo yale ambayo tumetoa kwa Tume. Kwanza tungependekeza kuwe na utangulizi wa Katiba ama kusema *"sisi watu wa Kenya tutalinda na kutetea Katiba bila ubaguzi, kwa amani, mapenzi, na umoja wa nchi huru ya kenya"*. Ukuu wa Katiba, tunapendekeza bunge iwe na idadi ya asilimia 75 kubadilisha vipengele vyovyote vile ambavyo viko kwa Katiba na wananchi wahusishwe kikamilifu. Katika hali ya uraia. Raia wa Kenya ni yule mzazi wake ni wa asili wa Kenya. Mkenya awe na kitambulisho cha taifa na card ya kuzaliwa.

Ulinzi: vyombo vya usalama viundwe na Katiba. Kuwe na Tume ya kuchunguza mienendo ya majeshi. Mamlaka na uwezo wa kuaagiza vita yawe ya kikatiba na bunge iwe na jukumu la utekelezaji wakati wa hatari.

Vyama vya kisiasa: Katiba ielekeze uundaji uongozi na tabia ya vyama vya kisiasa. Vyama vipate sehemu ya fedha kuendesha

shughuli zao. Hii ikiwa ni kulingana na idadi ya wawaakilishi bungeni.

Muundo wa serikali: Tufuate serikali ya mseto na mamlaka ya nchi ya kugawanya baina ya Rais na Waziri Mkuu. Rais asiwe wa chama chochote na wala asiwe anawakilisha sehemu yoyote ya bunge. Serikali za mitaa ama Local Government zipatiwe mamlaka ya kuendesha shughuli kikamilifu kama elimu, afya na huduma za jamii.

Bunge: Tunapendekeza bunge iwe ikipiga msako madarubini maofisa ambao watakaoteuliwa kuendesha shughuli za serikali. Wananchi wawe na uwezo wa kurudisha mbunge nyumbani ikiwa mbunge huyo ameshindwa kutekeleza wajibu wake.

Tume ya uajiri iwe inaamua marupurupu na mishahara ya wabunge. Kuwe na idadi kama sehemu moja kwa tano ya wanawake bugeni. Rais asiwe na uwezo wa kuzuia sheria iliyopitishwa na bunge na pia asiwe na uwezo wa kuvunja bunge bali bunge iwe na calendar yake.

Mamlaka ya nchi: Mgombea urais awe na elimu ya chuo kikuu ama elimu inayolingana, na awe wa miaka arobaini na tano au zaidi. Vipindi vya Rais viwe ni miaka kumi mtawaliwa. Katiba itoe kibali cha kumuondoa Rais mamlakani kwa kitendo kisicho halali. Rais asiwe mbunge.

Mahakama: Tunapendekeza mfumo wa sasa wa mahakama hautoshi na uthibitishwe zaidi. Tuwe na mahakama kuu nchini. Maofisa wanaoshughulikia mambo ya mahakama, wawe wakithibitishwa na bunge na wawe na elimu ya chuo kikuu au inayolingana.

Serikali za mitaa: Mayor na wenye viti vya mabaraza wawe wakichaguliwa na wananchi moja kwa moja, na vipindi vya utawala viwe miaka kumi peke yake na isizidi hapo. Rais au waziri asiwe na uwezo wa kuvunja mabaraza kama ilivyo sasa. Serikali za mitaa zipewe mamlaka kamili, na madiwani wapewe mishahara au marupu rupu yao kutoka mfuko mkuu wa serikali, na wapate pension baada ya miaka kumi.

Muundo wa taratibu za uchaguzi: Mfumo wa uakilishi katika uchaguzi ufuatwe. Mwenye kura nyingi atangazwe mshindi. Wapiganiao na kushinda urais wapate asilima 25% ya kura kwa mikoa mitano. Uchaguzi wa wabunge na mabaraza ufanywe pamoja, bali wa urais ufanywe peke yake. Nikendelea kumaliza, haki ya ardhi na nchi, kuwe na haki sawa ya kumiliki ardhi kwa waume na wanawake. Kuwe na vizuishi vya haki ya kumiliki ardhi katika nchi hii. Kuwe na kiwango cha juu kwa ukubwa wa ardhi, atakayemilikiwa na raia na ni kwa sasa kunaweza kuwa na mtu mwenye hekari hata elfu moja lakini kuwe na sheria ya kuzuia hiyo.

Uongozi na matumizi ya mali asili: Mamlaka ya nchi yasiendelee kuthibitiwa na kusimamiwa na serikali. Yaani mali asili, fedha pamoja utaalamu wa wanadamu. Bunge liendelee na uwezo wa kuimarisha, kuhusu matumizi ya fedha ya umma. Serikali

inahitajika kikatiba kutoa faida ya rasilimali ambazo zinapatikana katika eneo, na wananchi kwa jamii ambayo rasilimali ile inapatikana. Nikimalizia ma-Commissioners, Tume la kikatiba za office na office zinatakiwa. Kwa mfano lazima tuwe na Tume ya haki za binadamu, Tume ya jinsia, Tume dhidi ya ufisadi, na Tume juu ya ardhi, na pia tuwe na ofisi ya mtu ambaye anapokea malalamishi ya wananchi yaani Ombudsman.

Mwisho haki za kimsingi: Haki za watoto na watu wote zilindwe kikatiba. Katiba ilinde haki za elimu ya bure hadi chuo kikuu. Mwisho kabisa, serikali iwe na jukumu la kikatiba, la kuhakikisha wananchi wa Kenya wote wanafurahia haki ya kimsingi kama usalama, afya, maji, elimu, na makazi na hata chakula na ujira. Asanteni sana ndugu ma-commissioners.

**Com. Ratanya:** Asante Bwana Joel Haji, na sasa Bwana Alex Mghanga. Alex Mghanga yupo? Alex Mghanga? Hayuko? Mrs Mary Mwamodo.

**Mary Mwamodo:** Kwa majina mimi ni Mary Mwamodo kutoka Mbale Location. Mimi nina mapendekezo yangu mwenyewe kuhusu hali za akina mama.

Kwanza ningeanza na kusema ya kwamba ingawa sheria ya mtu muasi ipo, haifuatwi kwa sababu walio na mali na uwezo na madaraka makuu wanageuza geuza hili ilingane na matakwa yao. Kwa hivyo pendekezo langu ni kuwa, kila mtu mke na mume awe chini ya sheria bila upendeleo. Hata kama ni Rais amekosa, ni mimi nimekosa ni nani, mtu achukuliwe hatua kulingana na sheria.

Pili, kuhusisha wanawake katika ngazi zote. Tunaona ya kwamba hata tukiaangalia Parliament ina watu mia mbili na ishirini na wanne, lakini wanawake sita tu ndio wanatuwakilisha wanawake wote. Kwa hivyo tungependelea katika kazi zote, kama ni serikali au bunge, kuwe na moja ya tatu ya akina mama. Kama ni County Council tuwe na moja ya tatu katika Council na katika kamati kama ya land, kamati ya vijiji, kamati ya kila kazi, kuwe na wanawake, moja ya tatu.

Affirmative action izingatiwe, ili kila upande akina mama wawe wanaweza kuwepo. Kazi ya urithi wa mali, tunajua katika utamaduni wetu akina mama wamesahaulika sana. Kule kwenu umezaliwa huna shamba. Kule umeolewa vile vile unaenda unakuta mambo kama haya. Kwa hivyo tunataka urithi uwe sawa kama mimi nina msichana na mvulana ikiwezekana wapate urithi. Pengine msichana ameolewa na huku ameolewa hakuna land au hakuna ardhi, tuwafikirie akina mama.

Tuende upande wa uzalendo. Utaona ya kwamba mvulana wetu hapa akioa Mwa-america, au Murussia au nani automatically anakuja anapewa uraia wa Kenya na watoto wao uraia wa Kenya. Lakini msichana wangu akiolewa akiwa hapa na huyo bwana, na wamekubali kuishi Kenya, inakuwa ni vigumu kupata uraia. Msichana akizaa mtoto na mtu kutoka nchi nyingine, watoto wa msichana wake hawapatiwi uraia. Sasa wataenda wapi? Kwa hivyo tunataka Katiba itiliwe mkazo, ya kwamba, mama akiolewa na yuko hapa na bwana amekubali kuishi Kenya, yeye na watoto wake wapatiwe uraia wa Kenya. Hiyo ndio

itakuwa haki. Lakini kamba tukiendelea kuwa vile tulivyo tutaumia.

Utawala: Tunaona ya kwamba, kuna sheria ziliondolewa kwa ma-chief wetu. Lakini kuna zingine zingali zinaendelea kunyanyasa wananchi. Utaona ya kwamba kwa sababu ya utawala ilioko, watu hawawezi kuanya mikutano bila kibali kutoka kwa utawala.. Kwa hivyo katika Taita Taveta, ningependelea kama inawezekana, County Council ipatiwe madaraka ya kutosha, ili iweze kuturuhusu kufanya mikutano wakati inapotakikana, bila kupita kwa utawala. Kwa hivyo ni lazima tuone ya kwamba Katiba imetulinda, imelinda siasa zote, yaani party zote zimelindwa. Ningependekeza pia wakati wa campaign ukifika. Party zote zipatiwe kiwango fulani cha pesa. Katika Katiba pesa za kufanya campaign ziwe controlled, maanake sasa watu wananunuliwa. Kwa hivyo kuwe na kiwango ya kwamba yule anayetaka kupigiwa kura, atumie pesa kadhaa. Pengine hapo tunaweza kupata wajumbe ambayo tumewachagua kwa kupenda kweli.

Tena napendekeza ya kwamba wakati wa nomination, watu wengine wana-nominate wale wa ukoo wao. Hakuna ile criteria nominations. Kwa hivyo ikiwezekana, wanawake wapatiwe nafasi ya ku-nominate wanawake wenzao katika Bunge na County Council. Kwa hivyo kwa sababu nimeandika memorandum yangu sina haja ya kusoma kila kitu maanake ni ndefu. Nimesema tu kwa mfano kwa hivyo asanteni sana.

**Clapping**

**Com. Ratanya:** Huyo alikuwa ni Mary Mwamodo ambaye ni mwanachama wa ile kamati inayo mobilizisha wananchi katika mambo haya ya Katiba, na sasa namuita mwenzake Mercy Mwamburi atoe maoni yake.

**Mercy Mwamburi:** Asante Bwana Commissioner, majina yangu ni Mercy Mwamburi. Ningetaka kusema kwa upande juu ya wanawake wa Pwani. Wanawake wa Pwani wamekuwa very loyal kwa ruling party ya Kanu lakini hawajafaidika. Na siku hizi tukienda Lamu, Kilifi, Malindi, Mombasa, Kwale, Taita Taveta utakuta tumekuwa na marginalization ambayo hatuipendi. Mpaka leo hatujakuwa na wanawake wabunge ambao wametuwakilisha huko juu, ni chama cha upinzani ambacho kimeweza kuchukua mwanamke kutoka Mazeras na hata leo miaka thelathini na tisa hatujakuwa na mwanamke mbunge.

Katiba: Katiba lazima iwe na utangulizi.

**Interjection:** --------- inaudible

Napendekeza kuwe na affirmative action katika Parliament ambayo itakuwa ni act ya kwezesha wanawake thelathi moja kuweza kuwa na kiti cha bunge

Utangulizi wa Katiba: Tungetaka utangulizi wa Katiba uwe Katiba ni ya wananchi wa Kenya, na inaonyesha maneno ya Kenya

ambayo ina maana, na watu maarufu ambao waliweza kuchangia Katiba, na kukumbukwa na wanawake na wanaume ambao wamepigania uhuru wa nchi hii. Kama mwenzangu alivyosema kusiwe na ubaguzi. Mwanamke au mwanamume ambaye ni Mwa wanakenya akizaa, mtoto awe ni mwananchi wa Kenya. Kama vile wanaume wakizaa na wanawake wa nje, watoto ni mwanakenya. ID itolewe bila ubaguzi, na ianze kutolewa kutoka shuleni watoto wakifikisha miaka kumi na minane.

Usalama au security: Constitution ituhakikishie usalama wa wananchi kila mahali. Kwa mfano wanawake wa Lamu na wanawake wa Tana River, wamelalamika sana, hawawezi hata kufundisha juu ya Katika, hawawezi kufanya chochote, hata hawawezi kwenda kutoka kijiji kimoja hadi kingine kwa sababu ya shifters na hali ngumu kama hizo, hata katika makambi wanapata mateso na hawawezi kwenda kutoka kambi moja hadi nyingine.

Political parties: Hivi vyama vimezidi hata havina maana tena. Viwe controlled. Constitution icontrol political parties na vinafanya watu wengine wamekuwa akikataliwa hapa anaenda hii, akitoka hapa anaenda hii na anaangaisha wananchi au akitoka hapa anaenda ni deni. Akitoka kule anaenda na lingine na hii anatubabaisha. Sisi tunataka watu wenye msimamo. Kama wewe ni Kanu, Kanu damu. Kama wewe ni DP, DP damu. Kama wewe ni President, President damu.

**Laughter**

Legislature, yaani muundo wa Parliament, hivi sasa wanawake ni tisa tu, na wanaume ni mia mbili ishirini na nne. Hawa wanake hata wafanye nini, kama agenda imekuja, imepinga akina mama na watoto watashindwa, ama nasema uwongo?

**Audience Responds**:

Kwa hivyo tunataka ile affirmative action ambayo nilisema kwanza na ile tu-nominate wanawake, utuezi. Pale mwisho kuna mwaka mwingine ulipita wanaume (inaudible?) tunashangaa, tukashindika

**Laughter**

Kwa hivyo nataka kama wanawake hawajafikisha 33%, ile balance, iwe ni akina mama wanateuliwa. Tena akina mama wenye wana elimu na mama wana adobu njema, akina mama ambao wameweka nyumba zao vizuri -----------(?)

Executive: President asiwe juu ya sheria. President awe ni mtu wa kawaida maana hapa kwetu na akifanya makosa awekwe kotini. President awe ni graduate. Tumesoma mpaka tuna watoto ambao ni ma-graduate hapa. Kwa hivyo wasiwe wanakunywa bhangi watajiharibia.

Local Government: Local Council nataka ipewe nguvu, itawale district. Sipendelei majimbo nisameheni. Mimi nataka Local

Government ipewe uwezo, na chairman awe ni mtu mwenye uwezo na ma-Councilor wawe na uwezo, wawe na "O" level certificate and above. Na nominated councilors pia iwe ni affirmative action ifanywe hivyo. Kwa parliament na Local Government, pia walemavu wapewe nafasi, na wawe na viti vyao, kama ni vitano na viwe vinawakilisha hata mikoa.

Electoral system and process: Hii electoral process iwe ina wanawake sawa na wanaume sawa maana wanawake ni 32% na wanaume ni 48%. Kwa nini wanaume ndio wako hapo tele na wanawake hawako. Kwa hivyo sasa, mambo hayo yaishe. Ballot boxes ziwe transparent. Counting of votes zifanyiwe station ile ile, hapana mambo ya kubebana masanduku na makamba na vitu vingine, hata zikifika card zingine haziko, ama imeingua ingine ambayo si ya hapo..

**Basic rights:** Tungetaka Education ya watoto kutoka standard one to mpaka eight iwe free. Na university ziwe kila mkoa. Wundanyi aina university kwa nini? Hicho ni kitu ambacho kinatusumbua. Health. Constitution ihakikishe tunapata medical services free na ------------(inadible). Chakula. Kila Constitution ihakikishe nchi yake ina chakula, ina shape, barabara yanapitika. Sasa barabara za Tana River hazipitiki, hata kwenda Lamu na Taveta akina mama wanang'ang'ana na mizigo na kupanda malori. Electricity, iwe kila mahali. Si, ukiwa mbunge basi unaipeleka kwako direct. Power ipite kwa kila mtu, rural electrification.

Affiliation Act: Hii ni kuwa sheria mtoto wa kiume akitia mtoto wa kike mimba amtunze mpaka amalize elimu.-----------------(inaudible). Tafadhali kama wanawake tumesoma tunataka mtoto aolewe akifika miaka kumi na minane au ishirini na moja na kuenda juu.

Watu walemavu: Walemavu wapewe haki yao na basic rights zao. Courts. Tuwe na protection za rights za watoto ambao ni walemavu. Na Kadhi courts. Hii court Kadhi achaguliwe na waislamu, apigiwe kura kama vile Machief mlikuwa mnasema, na tena awe na elimu ya kutosha na awe na -----------(inaudible) na yeye. Tuwe na afisi ya Jinsia, Gender Commission, kwa sababu, hii itaangalia akina mama mambo yao yote.

Employment, it is outlawed. Imekuwa outdated. Iangaliwe. Mtu mmoja, kazi moja. Hapa mtu mmoja kazi nyingi. Mtu mmmoja kazi moja na watoto wetu wamemaliza elimu wanarandaranda wamekuwa ni kama hawakuenda shuleni hata wengine wanaweza kukupiga. Nisameheni sana tungesema Constitution iwe ni amended ……(inaudible). Ni hayo tu …

**Com. Ratanya:** Asante Mercy Mwamburi kwa maoni yako na sasa namwita Bwana Juma Bakari Kayo.

**Juma Bakari:** Asante Bwana Chairman kwa kuja hapa kuchukuwa maoni, hii ni shukrani kubwa sana. Tangu Tumepata uhuru hii ndio mara ya kwanza kumuona ikiwa mumekuja hapa kuja kuchukua maoni.

Maoni yangu ya kwanza ni, hizi nursery ambazo zinazofundishwa watoto. Tunaomba katika nursery hizi, walimu wachukuliwe na serikali, wazazi waondolewe mzigo.

**Clapping**

Pili, tangu tupate uhuru Tumeambiwa kwamba, elfu mbili na Katiba ya zamani kwamba tutakunywa maji wakenya wote, hatukukunywa maji sisi wakenya wote. Tunaomba kwa jumla ikiwa ni Katiba kamili inapitishwa, ipitishwe kwa kila Mkenya na haki ikiwa ni ya haki juu ya haki. (*clapping*) Ikiwa kuna mashirika isitangazwe kwa kuuzwa, isikatazwe kwa wakubwa, itangazwe hata kwa wadogo na irudishwe kwa wananchi.

**Clapping**

Maana plot inaonyeshwa itachukuliwa na watu wa nyanja za juu maana katika court process sisi ni maskini wa kiwango cha chini zaidi. Kwa hivyo tunaomba ikiwa inauzwa irudishwe kwetu kwa Wataita na wa pwani, tuwe na shares za kukaa na hiyo plot. Isipelekwe kwa mtu yoyote katika angle za juu.

Rais awe na mamlaka madogo zaidi, mwananchi awe na mamlaka makubwa zaidi.

**Clapping**

Na huyo Rais apunguziwe kila kiwango, na akiwa anatembea kwa wananchi wowote pahali popote katika Kenya, asiangushe kwa sababu yeye ndio anatawala, aseme chama chake ndicho kinaongoza zaidi, yeye anasema mwananchi achague vile inavyopendekezwa. Tukirudi kwa Council, katika vyama vya opposition miaka iliyopita hakuna Councilor yeyote kwa upande wa opposition. Tunaomba ikiwa Katiba inapitishwa miaka ijayo opposition nao wachaguliwe ma-councilors, ikiwa mimi ni mmoja wapo.

**Cheering**

Kwa sababu tulitumiwa unyama ambayo ni unyama mkumbwa katika hall hii. Tukisema sisi ni opposition, tunapigwa mateke. Lakini afadhali hiyo opposition ilikuja na imemwerevusha mwananchi, na mwananchi amekuwa huru. Tukirudi katika upande wa police, sehemu ni ndogo sana hapa ya Wundanyi. Ni kama kumweka mguu wangu na upande huu hautoshi. Wananchi wakitiwa ndani wanazimia ndani. Tukiaangalia katika wilaya ya Taita Taveta, sisi hatuna daktari, je kama tuko huru, kwa nini tunanyimwa daktari? (*applause*). Na ikiwa ni mapango yanapangwa katika Kenya, madaktari tupangiwe katika kila wilaya zilozoko Kenya. Daktari wawe wakichukuliwa----- ----(inaudible) sisi wataita ambao Tumewekewa kiboko cha kufa. Tunaomba hayo mambo yaondoke kabisa.

**Clapping**

Uhuru hatukuomba mtu mmoja, tuliomba uhuru zote.  Maoni yangu ndio hayo.

**Clapping**

**Com. Ratanya:** Asante Bwana Juma Bakari Tayo kwa maoni yako na sasa Bwana Michael Mwalugha sorry Mwalugha. Bwana Michael Mwalugha.

**Michael Mwalugha:** Asante sana Bwana Chairman, maoni yangu-- majina ni kama hayo tu mlisikia na maoni yangu ni juu ya hizi powers za Rais.  Power za Presidents zinatakikana zipunguzwe mara unasikia ni Chancellor wa University za Nairobi na university zote Kenya, mara tena ni Chairman wa chama cha Kanu, tena ndio kiongozi wa taifa.  Hizo powers tunataka zipunguzwe, na tena maoni ningesema hii serikali kuwa Nairobi, haitufaidi chochote.  Tuwe na Federal System of government ambayo kama hapa Mombasa tuwe na Provincial capital ambayo ni Mombasa.  Kwa wakati huu, hizo serikali provision zake zinaendelea ingawa watu hawakuelewa tuko na ….(inaudible) Councilors in Mombasa.  Hii ndio zingekuwa serikali za majimbo, ambazo zinaenda kuangalia masilahi ya wakenya, maana serikali kuwa huko na Nairobi imetufinya hapa hasa mkoa wa Pwani, tangu tupate uhuru hakuna maendeleo yeyote tumefanya hapa Mombasa.  Tukiangalia kwa hali ya madini, kila kitu kinafanyiwa Nairobi.  Sisi hatuna kitu twakula makombo tu na kwa uchumi sisi tunafanya kila kitu, tuko na roads, tuko na railway, tuko na kila kitu.  Kwa hivyo tungeonelea tuwe na serikali ya majimbo.  Halafu kama tuna President, tuwe na ceremonial President kama vile Israel na Egypt.  Halafu serikali iwe ikiongozwa na Prime Minister na tena iwe -----------(?) yaani ni kama maanake tunatupa mbao kwa Katiba:

1. Ni wakikuyu
2. Kalenjin na kuna hawa waluyha na kuna wajaluo.

Iwe ikizunguka kwa kila mkoa kama Mombasa, Central Province itapata nafasi yao, na sasa Rift Valley itapata nafasi yao na sasa imeenda kwa province zingine.  …… (inaudible)  Ingekuwa sasa kama Katiba inavyoendelea, kungechaguliwa na wananchi, na sio Rais.  Na kitu kingine, nilikua nataka kuongea habari ………

**Interjection:** -------------------------------------- (inaudible).

**Michael:** Isiwe ikichaguliwa na President, iwe ikichaguliwa na wananchi.  Habari ya wageni, imekuwa ni jambo lingine la kushitisha sana, mwananchi wa kawaida hapewi ulinzi wa kutosha.  Na haki ndiye anayelipa kodi lakini sasa kunapo fanyika jambo kwa mgeni, unakuta hata ndege zinatolewa hadi kwake na kila kitu.  Mwananchi wa Kawaida anapofanyiwa kitu hakuna chochote yeye anawachwa tu namna hiyo.  Basi ningeomba sheria hiyo ilinde mwananchi pia.

Kwa upande wa elimu. Elimu hii ingefaywa bure kuanzia standard one mpaka university. Maana sasa wakenya wengi wako na shida, hata wengine hawasomi wako nje. Kwa sababu tulikuwa na Katiba sasa President atakuwa akitawala kwa kiti chake mwongo, miwili, hii Kenya currency isiwe na portrait ya President yeyote. Iwe portrait kama mlima Kenya uonekane katika noti au kama zile pembe za ndovu, Mombasa, iwe ikionekana katika hizo maana itakuwa ni gharama kubwa kwa mwananchi kila wakati kugharamia kiti cha Rais mwingine akigharamia kitambulisho cha pesa iwe ni alama moja. Kama ni Mlima Kenya, Pembe za ndovu Mombasa ziwe katika tarafa ya Kenya.

Jambo lingine ni habari ya police. Kuna vile tunavyoona kuna APs, tuko na Police na GSU. Hawa ukiangalia wanafanya kazi moja, na hiyo inakuwa ni gharama na ku-overburden mwananchi wa kawaida. Tungeomba hivi vikosi vivunjwe, viunganishwe viwe pamoja. Kama ni police, tuwe na police, tusiwe na GSU. Yangu ni hayo.

**Com. Ratanya:** Asante Bwana Mwalugha kwa maoni yako, sasa namwita Bwana Chando. Darius Chando.

**Darius Chando:** Pendekezo langu ambayo ningependa kusema Bwana Commissioners. Mapendekezo yangu kwa Katiba hii ya kurekebisha Katiba ni kama ifuatavyo:

Kwanza kabisa, Katiba hii lazima ihakikishe ya kwamba yale ambayo tunayotaka yanapaswa yapewe kipawa, hivyo basi iwe na utangulizi ambao utaonyesha historia ya Kenya na Kanuni za kimsingi, ambazo kila mkenya anafaa azingatie kwa usawa. Demokrasia, uhuru, maendeleo ya kiuchumi, haki, umilikaji wa rasilimali na kadhalika. Kwa kuwa dola hii ya Kenya ina kanzu tatu muhimu, yaani serikali, bunge na mahakama, tungependa kusema kwamba inafaa tuwe na kiongozi wa dola ambaye atakuwa akihudumu katika wadhifa huu kwa mihula miwili ya miaka mitano kila mmoja. Awe na umri wa miaka isiyopungua arobaini, na isizidi sabini. Awe raia wa Kenya kwa kuzaliwa. Awe amesajiliwa kama mpigaji kura na awe mwana chama wa chama chochote cha kisiasa ambacho kimesajiliwa. Awe ni mtu ambaye hajatajwa kwa kashfa yoyote ya ufisadi. Awe amehitimu elimu kupita kiwango cha kidato cha sita kwa elimu ya zamani na kidato cha nne kwa mfano kwa mfumo wa elimu ya sasa na pia awe amesomea mambo ya utawala. Awe ameteuliwa na chama chake kama mgombeaji wa kiti hiki na pia ateuliwa na watu asilimia 35 waliosajiliwa kutoka kwa kila mkoa. Awe ameoa, awe ameolewa. Asiwe na kosa lolote.

Kiongozi wa serikali atakuwa akihudumu katika wadhifa huu kwa kipindi cha mihula miwili ya miaka mitano kila mmoja, awe na umri usiopungua miaka 35, na usiozidi sabini. Awe raia wa Kenya kwa kuzaliwa. Awe ameungwa mkono na wabunge asilimia sabini na tano ya wabunge wote waliochaguliwa. Ateuliwe kutoka kwa chama kilicho shinda uchaguzi. Apeane taarifa kuhusu mali yake, awe ameoa au ameolewa. Awe na uwezo wa elimu ya juu ya utawala na usimamizi wa mambo ya umma au fedha.

Katika swala la bunge. Mbunge sharti awe na miaka isiyopungua miaka ishirini na saba na isiyozidi sabini. Awe na cheti ya kidato cha nne au zaidi. Awe hajafanya kosa lolote. Awe ameoa au ameolewa. Awe mwanachama wa chama kilichosajiliwa

na awe ameteuliwa na chama hicho.

Katika swala la mahakama, Judge mkuu awe ana umri usiopungua umri wa miaka arobaini na tano na isiozidi sabini na tano. Awe ni mkenya kwa kuzaliwa. Awe ameoa au ameolewa. Ikiwa tutakuwa na waziri mkuu, huyo atakuwa na wajibu wa kutafuta au kuunda serikali akichagua mawaziri kutoka kwa jamii. Mawaziri hawa lazima wawe wamehitimu chuo kikuu na wenya taaluma ambazo zinawezesha kuongoza wizara ambazo watapewa kusizimamia. Hata hivyo baada ya mawaziri kuteuliwa ni lazima majina yao yahidhinishwe na bunge na ikiwa na majina ya wabunge hawa, yatakuwa yamekataliwa na bunge kwa mara tatu, basi waziri mkuu huyu anafaa ajiuzulu kwani atakuwa ameshindwa kuunda serikali. Ikiwa mbunge atakuwa amefanya kosa, wakenya hawatangojea hadi miaka mitano iishe, bali watakuwa huru kupiga kura ya kutokuwa na imani na watu hawa. Ikiwa Rais atakuwa amefanya kosa bunge inapaswa ipige kura ya kukosa imani naye. Bunge, kwa vile ni sauti ya watu, lazima iwe na mamlaka makubwa kwa mfano, kuunda na kuvunja wizara, idhinishe matumizi ya serikali. Hata hivyo inapaswa kuwa na mswada ambayo bunge inapaswa kuhidhinisha na ambayo ni mambo yanayohusu wenyewe kwa mfano mishahara yao na marupurupu inabidi wakenya wenyewe wapige kura ya maoni.

Kunafaa kuwe na serikali za mitaa ambazo zinafaa. Ziongozwe na ma-mayor na mwenyekiti aliye na elimu ya kidato cha nne au zaidi, na wawe wana taaluma ya utawala. Hao ma-mayor na wenye viti lazima wachaguliwe na wananchi. Diwani lazima awe ameoa au ameolewa. Awe na umri wa miaka ishirini na tano au zaidi, lakini asizidishe miaka sabini. Awe ameteuliwa na chama kilichosajiliwaIli serikali za mitaa ziwe na uwezo, ni sharti ziwe zimetungwa na serikali kuu, na kupewa jukumu la kusimamia rasilmali zilizoko katika eneo fulani, linalosimamia madini na kupata mapato kutokana na wanyama wa pori. Kusimamia taasisi zilizoko kama mazahanati na ma-hosipitali ili hili likiwezekana hapa Taita Taveta, mbuga ya kitaifa ya Tsavo sharti ibadilishwe na kuwa Game Reserve, ili nasi pia tuwe tukifaidi vile wenzetu wamasaai wanavyo faidika na Masaai Mara Game Reserve. Kwa sasa hatupati mapato yoyote kutoka kwa mbuga za wanyama ya Tsavo. Katika serikali ---

**Interjection:** Samahani, uko karibu kumaliza?

**Darius:** Yes.

**Com. Ratanya:** Jaribu kumaliza

**Darius:** Ninamaliza. Yes ninamaliza. Katika serikali ya mitaa vikao vya maendeleo wilayani, DDC itabidi ziwe zikiongozwa na viongozi kama, mwenye kiti aliyechaguliwa na wananchi. Misitu ambayo iko hapa inapaswa imilikiwe na wenyeji, ili waweze kuifadhi wao wenyewe. Hivi ni kusema kwamba ikiwa itakuwa chini ya serikali za mitaa yaani, County Council na wenyeji kuhimiza kuhifadhi jambo hili litakuwa bora sana. Ikiwa nafasi za kazi zimepatikana katika eneo fulani, wenyeji wanafaa wapewe nafasi hizo kwanza, wakiwa na vyeti vinavyohitajika kwa kazi hizo. Kwa vile swala la mashamba ni swala, vyeti vinahitajika kuwa mwenye kiti wa halmashauri ya kusimamia mashamba, Land Control Board achaguliwe na wananchi na awe mwenyeji wa eneo atakayekuwa akihudumia, wasiwe ma-district Commissioners.

Kandarasi ambazo hutoka katika maeneo fulani fulani za nchi hii, zinafaa ziwe zikipewa wenyeji, na hata ile miradi ambayo hufuatiliwa na serikali itabidi wananchi waarifiwe na wahusishwe kikamilifu.

Haki za kibinadamu: Katiba hii itafaa iangaliwe, ili tume kwa kuwa tunaishi maisha bora. Haki zetu zote kwa kupata elimu, haki na kushirikiana haki za kutoa maoni, haki za kupata chakula, wafanyi kazi lazima sizingatiwe. Katika haki za kupata elimu na ya kupata matibabu, itafaa sana kwamba haya mambo ya kugawana gharama, cost-sharing ni sharti ziondolewe. Sheria za kazi ni sharti zibadilishwe na serikali iangalie sana swala la malipo ya uzeeni kwa wale wanaostaafu hasa kutoka kwa serikali. Tunasikitishwa sana kwamba kuna wazee ambao wametumikia serikali kwa moyo na mwishowe wakasahauliwa, maanake benefits wanapata kama elfu mia mbili sitini kama pension, Si pesa za kumsaidia mkenya kwa siku hata mbili. Mtu akistahafu alipwe haki yake bila kutatizwa mara kwa Chief, mara kwa D.C, au kwenda Nairobi. Hii inatatiza wananchi wengi. Wajane ambao waliachwa na mabwana wao walikuwa wakifanya serikalini, itafaa sana nao pia wapewe msaada wa kuwaezesha kulea watoto. NSSF mtu alipwe kwa hiari yake lakini asilazimishwe.

Katika haki za wanawake, inafaa tuwe na sheria ya kwamba ikiwa msichana amepata mimba, yule anayehusika alazimishwe kumuoa au kumlea mtoto huyo.

Marekebisho ya Katiba, yarekebishwe sawa na maoni ya wananchi wote wa Kenya. Asante.

**Clapping**

**Com. Ratanya:** Mercy Nyange, Mercy Nyange/

**Mercy Nyange:** Kwa majina naitwa Mercy Nyange. Yafuatayo ndio maoni yangu.

1. Rais: Ili tupate kiongozi ambaye ni wa watu wote, ninapendekeza kwamba isiwe lazima mgombea urais atoke kwa chama. Kwa hivyo Katiba iruhusu independent candidates.
2. Number two, uchaguzi wa Rais ufanywe kwanza halafu ule wa ibunge na udiwani ufuate, asigombee kiti chochote.
3. Kuchaguliwa kuwa Rais ni lazima apate 50% na zaidi za kura zote zilizopigwa nchini.
4. Kama Rais ni mwanaume, basi makamu wa Rais awe mwanamke.
5. Rais ashikilie kiti kwa miaka kumi yaani kipindi cha kwanza ni miaka tano na aweze kugombea urais tena kwa kipindi kingine cha pili kwa miaka tano. Kusiwe na mambo ya kusema ati arudishwe bila kupingwa.
6. Atakayechaguliwa kuwa Rais, awe mtu aliyekomaa, kuanzia miaka arobaini na tano na kuendelea, awe ameoa kwa maana tunataka first lady. Akina mama tutaheshimiwa zaidi na tutakuwa na mama ambaye ni mfano kwetu. Sasa hivi hatuna.

7. Rais lazima awe chini ya sheria kama wananchi wote.
8. Ubunge na udiwani. Kwa sababu akina mama ni baraka kwa kila jambo, ninapendekeza ya kwamba kuwe na one third ya akina mama kitika bunge hata udiwani. Kwanza akina mama ndio wanapiga kura. Tuko wengi zaidi. Kama haiwezekani, hata ni heri viti vingine viwe vvinahesabiwa ni vya akina mama na tuwapigie kura.
9. Kama Mgombeaji kiti ameshindwa kwa uchaguzi asipatiwe nafasi kama nominated. Mjumbe aliyeteuliwa kwa sababu haitakuwa na maana yoyote ya kufanya uchaguzi.
10. Chiefs na Sub-chiefs pia wachaguliwe na wananchi ili wafanye kazi vyema.
11. Wabunge na Diwani na Chiefs wapatiwe mihula miwili ya miaka mitano. Wabunge wakimaliza mihula miwili wanaweza kugombea urais.
12. Kura zihesabiwekatika kila kituo badala ya kupelekwa mahali pamoja. Hii itaondoa mambo ya rigging.
13. Registration ya kupiga kura iendelee muda wote kwa yeyote aliyetimiza miaka kumi na nane na amepata kitambulisho.
14. Kwa upande wa uchumi, rasilmali zinazotoka mikoani, 75% ibaki mikoani humo ili kuendeleza mikoa hiyo.
15. Bidhaa Zinazotoka nje zisikubaliwe kuletwa nchini, kama bidhaa hizo zinapatikana nchini. Hii itasaidia uchumi na watoto wetu watapata kazi.
16. Upunguzaji wa wafanyi kazi usikubaliwe. Kama ni lazima, basi wale wanaokaribia kustaafu ndio wanafaaa kuachishwa kazi. Sio wale watoto wadogo ambao hawajafikia umri wa kustaafu. Hii itapunguza uhalifu.
17. Wakati wa kugombea kiti, pesa zozote zisitolewe wakati wa kugombea. Wanahusika watumie radio, T.V na mikutano, ambayo itapangwa na Electoral Commision.
18. Upigaji kura wote ufanywe kwa njia ya siri, na usimamiwe na Tume ya uchaguzi.

Asanteni sana.

**Clapping**

**Com. Ratanya:** Shukrani Mercy Nyange, na sasa tutamwita Bwana Saisi, Thomas Saisi ambaye ni kipofu kama nilivyosema hapo awali Katiba hii inadhamini kwamba wale ambao wana taabu fulani lazima tuwazingatie kwa kuwapatia nafasi ya kutoa maoni yao.

**Thomas Saisi:** Wapendwa ninasikitika sana kusema kuna shida hapa Kenya tena kubwa sana. Watu kama sisi tunapata taabu, taabu tena kubwa sana. Huwezi kupata jambo la kujiendeleza wewe mwenyewe ikiwa kuna watu hapa hapa nyumbani wenye kijicho, na nasikitika sana kusema hilo jambo. Nasikitika watu kama sisi hatuangaliwi hasa upande wa kwetu hapa, hiyo ni shida moja. Kwa sababu gani? Mimi nasema hivi kulingana na yale niliyopata (kule 1968 na yale ninayaona), ninasikitika sana. Kwa sababu gani? Saa hii kile nichokipata kule hata ukiambiwa nilipata kitu huwezi kukubali. Nasikitikia sana. Kwa sababu gani? Unawezaje kuamua, uamue uaambie mtu nitakuona mwisho, halafu uwe kicked out, inawazekanaje. Nasikitika sana wapendwa kusema hilo jambo. Kwa hivyo tafadhali kuwe na referendum.

**Com. Salim:** Ungependa jambo maalum lifanywe?

**Thomas Saisi:** Ningependa jambo maalum lifanywe.

**Com. Salim:** Jambo gani?

**Thomas Saisi:** Kama ingewezekana kama ni mchango tufanyiwe. Kwa sababu gani? Hii maisha imenishinda kwa sababu gani kile kichokuwa kikinisaidie, hakuna sasa.

**Com. Salim:** Msaada gani?

**Thomas Saisi:** Msaada aina yoyote lazima tufanyiwe kwa sababu gani saa gani saa hii maisha hatujiwezi, niko na bibi na watoto. Lakini kile ambacho kingenisaidia kimeuawa.

**Com. Salim:** Tuko ------------- inaudible

**Saisi:** Hata kama ni Fundraising, tuko ready sana

**Com. Salim:** Kitu gani:

**Saisi:** Hata kama ni fund raising, I am ready. Sasa nimeshindwa -------------(inaudible) mpaka kile ambacho kinaweza kutusaidia. Kwa hivyo nasikitika kusema saa hii hata kulea watoto umeniletee taabu, taabu niombe msaada nje ndio nikule nyumbani nawatoto.

Jambo lingine ni kwamba mimi ninashangaa kwa sababu hata kwa upande wa blindness, sisi huwa hatuangalii kwa upande wa kazi za kuandikwa hivi. Sasa kazi kama tuseme kama Operator. Those are the jobs we can be able to do. Lakini utashangaa kukuta kazi kama hizi zinapewa watu wenye uwezo wao. Sasa ninashindwa itakuwaje. Kwa hivyo nasema asante sana kwa kunipatia nafasi.

**Clapping**

**Com. Ratanya:** Asante Bwana Thomas Saisi kwa maoni yako, sasa tutamwita Bwana R. M. Shako. R. M. Shako?

**Ronald M. Shako:** Majina yangu naitwa Moshambo Shako, natoka Umingo Location. Ningependa kwanza kuwapongeza ma-commissioner kwa kazi ambayo mumefanya kwa muda mrefu, ninafahamu kwamba mnachangia kitabu kimoja cha Katiba, kwa hivyo nitajaribu sana nisirudie yale ambayo yameshazungumziwa. Lakini kitu nitazungumzia ni kuhusu taratibu za utawala wa kitaifa. Ningependekeza tuwe na Rais, na kuwe na makamu wa Rais, lakini makamu huyo awe amechaguliwa na wananchi ili kwamba awe na ukakemavu wa kujua kwamba (…..inaudible). Watu wamezungumzia mambo ya Prime Minister,

ningependa kuzungumzia kwamba singependekeza kuwe na Prime Minister kwa sababu ninalolifikiria nitatizo sasa hivi, sio ukosefu wa Prime Minister, isipokuwa kitu kinacholeta matatizo ni uadilifu, yaani accountability ya wale walioko kwenye mamlaka. Kwa hivyo badala ya kuwa na Prime Minister ambaye itaongeza gharama ya utawala, na uchumi wetu hautaweza kubeba gharama hiyo, nguvu za Rais zipunguzwe na tupatiwe Statutory offices ama ---------(inaudible) offices. Hivi kwamba basi Rais awe accountable to the Parliament and all regulatory Statutory institutions zipewe nguvu zaidi ili waweze kukosoa wale wanaotawala. Katika hali za uchaguzi, ningependekeza kwamba, Katiba ishurutishe kwamba, kila uchaguzi ufanywe kwa secret ballot.

Kuna swala la ardhi limeshazumguziwa lakini nitasisitiza tu. Lazima kuwe na kiwango cha ardhi ambacho mtu mmoja anaweza kumiliki. Sasa hivi tuko na wafalme wa mashamba. Ukimjua Commissioner wa land unakuwa na shamba Lamu hulilimi, unakuwa na shamba Kwale ulilimi. Umeweka tu aidha ni barua ya kupatiwa hiyo shamba au Title Deed, na wale wanaopakana na hiyo shamba ambao imekaa hailimwi, wanalala njaa, na hawana hata kipande cha kulima. Kwa hivyo ningependa Katiba ishurutishe kwamba, kuwe na kiwango na mtu yeyote asiruhusiwe kuwa na ardhi ambayo inakaa bila kutumiwa.

**Interjection:** Kiwango gani?

**Shako:** Ningependekeza kiwango kama maximum 10 acres maanake watu wanaongezeka, ardhi inapungua na watu wanyakuzi wanachukua ardhi kubwa ambayo hawaitumii. Ningependekeza pia na nyinyi ambao mnaelewa kisheria mtatumia lugha yenu wenyewe to delink the public servants from political influence. Sasa hivi naweza kutoa makosa Rais na pengine anatawala na Public Service, ambayo haiko loyal to him, or aiko patriotic in any case. Kwa sababu wale ambao wanakaa Nairobi, 90% of Nairobi voted for the opposition. Therefore, majority of the Public Service are in the opposition, in the way they think and it should form a political government and you are the ruling with a Public Service that is not loyal to you, how can you deliver Public Service? How can you do the business of the State using a Public service that has got a different political agenda? I would wish to suggest mtumie lugha yenu ya kuhakikisha kwamba Public Service is completely clean from politics.

Ningependa kuzungumzia jambo fulani, nitazungumza kwa kingereza ndio ieleweke vizuri, hii inahusu human capital. Ningependekeza kisheria na kikatiba, serikali ya wakati wote ule, ishirikishwe kwa kuhakikisha kwamba, human capital imekuwa developed. Kwa sababu ya gharama tu, ninapendekeza elimu iwe ya bure kutoka class cha kwanza mpaka cha nane. Na ningependekeza kwamba serikali ishurutishwe kikatiba kutafuta njia ya kuwa-develop watoto tanga tanga. Wale watu tunaokaa mijini, tunaona kwamba hawa ni binadamu, hawana watu wa kuwaangalia, na wanapokuwa watu wazima wanakuwa wahalifu. Kwa hivyo nataka Katiba, ningependekeza kikatiba serikali ya wakati wote ule ishurutishwe kuhakikisha kwamba kila raia amekuwa developed ili kwamba aweze kujalisha, manaake wasipo zahisha wataongoza umasikini.. Nafikiri sitarudia yale ambayo yamezungumzwa hasa na Mercy Mwamburi, na Councilor Haji wamezungumza vizuri mambo mengi, nimebadilisha sana maoni yangu niliyokuwa nayo, lakini ningesizitiza tu, ili serikali ya wakati wowote iwe na uwezo wa kutumikia

raia, lazima public servants wawe de-linked with politics before because that's the only way the public can be served without bias. Asante.

**Com. Ratanya:** Asante Bwana Shako, sasa namwita Andrea Mulango. Andrew Mlango? Hayuko? Darius Kazungu. Darius Kazungu? Hayuko. Meshack Mwaito? Jamaa wanaanza kuondoka. Edward Mghengi.

**Edward Mghengi:** Kwa majina mimi ni Councilor Edward Mghengi kutoka (…..not clear). Yale ningezungumza mengi yamegusiwa lakini nangetaka kusizitiza pale hasa, iliyonifanya nifike mahali hapa. Mtaita kwa jumla ni mtu aliyebarikiwa kupatiwa rasilmali na mwenyezi Mungu, lakini Katiba inayoundwa sasa inamfanya Mtaita aendelee kubaki maskini na mwembamba. Hasa nikiguzia mambo ya East African Wildlife ambaye imechukua ardhi kubwa ikiwa ni East and West, Tsavo National Park. Kwa maoni yangu kwa muda mrefu jambo hili limeongewa na viongozi kwa uzito lakini halijazaa matunda. Ni maombi yangu kwamba kwa wakati huu Katiba itupatie mojawapo, kwa jina la Game Reserve, ili imilikiwe na Local government ya Taita Taveta, kwa manufaa ya Mtaita. Kwa sababu kwingineko kwingi, sehemu hizo ambazo zimepakana na hawa wanyama, Mtaita ameendelea kupoteza maisha na mali. Na inapofikia mahali kwa fidia, wale walio katika uwezo wa kuangalia jambo hilo wametupatia kisogo.

Ili, Katiba hii itusaidie, basi singetaka kuomba a certain percentage, lakini ningeomba sehemu fulani tupewe, kwa maana ni haki yetu, na hii itaweza kutufanya tuone haki yetu imerudi. Na hawa wanyama tuwapende. Upande mwingine ningetaka kuzungumzia, ni juu ya mgao wa mapato katika nchi yetu. Utakuta kwamba Coast as a whole, tumebarikiwa kuwa na viwanda na njia nyingi za employment lakini msimamo ule ambao tunaopata katika intake ya Provincial schools, kama ungeweza kuwekwa katika upande huu kwamba a higher percentage iwe ni wale watakaotoka katika eneo hizo kuajiriwa, basi watu wa Coast Province na Wataita hasa hatungeumia kwa uchumi. Lakini hivi sasa tumeumia kwa jambo hilo, na tungeomba iwekwe maanani kwamba kama kiwanda Voi, basi wataita wapatiwe nafasi huko. Vile vile Kenya Ports Authority Mombasa, vile vile Coast, watu wa Coast wangepatiwa nafasi kubwa, ili hii ikiwa rasilmali ambayo hawakuipigia kura Mwenyezi Mungu akawapatia, basi iwafaidi. Nikija katika hali ya maisha na ulinzi. Ningeomba Katiba ya leo ichukue na kuweka mkazo katika mambo ya dawa za kulevya. Haya yameangamiza watoto wetu. Ikiwa sheria ambayo iko sasa ni hafifu, tungetaka sheria iweko kwa wale wanaofanya biashara hiyo, wafungwe kifungo cha muda mrefu, akitoka pale basi kuwe upepo mzuri umewapiga wale ambao wananyanyaswa na hali hiyo. Kwa sababu visa vingi na jina la Kenya kwa jumla limeharibika kutokana na tabia ambazo watoto hao hawakupenda lakini wamelazimishwa. Kwa hivyo sheria hiyo ya mtu akipatikana na madawa ya kulevya, ningetaka kama ilivyo iongezwe mara dufu.

Nikija kwa upande wa utawala wa mikoa, ilizungumzwa lakini mimi napendekeza hivi, tunapopata nafasi ya kumchagua Assistant Chief au Chief zitangziwe nafasi hizo na viwango vinavyotakikana kiutawala, wenyewe wafanye application, halafu itakapofika wakati wa kuchagua, tupatiwe majina either matatu au manne, ambayo yameonekana hawa wamefaulu kulingana na kiwango kinachotakikana na utawala. Halafu majina hayo turudishiwe ndio tupige kura tumchague yule tunayetaka. Awe ni

Assistant Chief au Chief. Kwa njia hiyo, hao ndugu zetu hawa watawala wetu, kwa vile hawana transfer iwapo ameshindwa na kazi, basi tutakuwa tukipata watu ambao wanaweza kutoa huduma ambayo inatazamiwa na watu wake. Na vile vile kadri madiwani na wabunge walivyo na time limit, pia na hawa, ikiwezekana wawe na time limit. Nafikiri singekuwa na mengi zaidi ya hapo, nataka kuwashukuru macommissioner. Asanteni kwa kunisikiza.

**Com. Ratanya:** Asante sana Bwana Edward Mghangi kwa maoni yako, huyu ni Councilor katika eneo hili, na sasa tutamwita Bwana Aren Mwangima. Aren Mwangima? Samahani.

**Robert Mwangoma:** Kwa majina naitwa Robert Mwangoma kutoka hapa hapa Wundanyi. Kwa maoni yangu mimi moja binafsi, mimi ningetaka tuwe na Prime Minister, na President awe ceremonial. President awe ceremonial in that, awe ni mtu kazi yake ni kusign majadiliano yale ambayo yamewasilishwa na bunge, asiwe na mamlaka juu ya bunge. Yeye awe ceremonial President, a-observe kama Labour Day, Madaraka Day, Kenyatta Day au Jamuhuri Day. Asiwe na mamlaka juu ya bunge. Asiwe decision ambayo imefanywa na bunge au anaweza kui-revoke. Aheshimu mamlaka ya bunge.

La pili, hii ni kwa maoni yangu mtu ambaye amefika miaka zaidi ya themanini sioni haja kama ana lazima ya ku-vote. Kwa sababu mtu kama huyu, hii ni exercise ambaye inataka mtu awe katika sober mind. Aelewe ni kitu gani kinaendelea. Mtu kama huyu ukimpatia nafasi ya kupiga kura na tunaona nchi vile ilivyo kuna watu wengine ni maskini, anahongwa anapewa pesa, anasahau vile anatakikana kufanya ni very important kwa miaka tano hatutapata mtu kama yule. Mtu kama huyo anadanganywa kwa sababu ya umri wake na kufanya mambo hayaeleweki, anafanya kitu ambapo, ni ile kura yake ni very important, inapitisha mtu ambaye hatakikani na yule anatakikana anakosa. Kwa hivyo hatupendi mambo kama hayo. Mtu kama amefika zaidi ya miaka themanini, hana lazima ya ku-vote, tunaweza kumwaambia apumzike. Vile ninavyoweza kusema ni kwamba wakati kama huu wa mfumo wa vyama, tunaona kwamba, chama kimoja kikipewa utawala zaidi, tutapata wale wengine ambao wanapata nafasi katika upande wa upinzani, tuna ona kwamba wanapata huduma hafifu katika serikali. Tunataka serikali au Katiba itengenezwe ambao inasema level ground, kwa viwanda vyote na huduma zipeanwe kwa watu wote bila kuchagua mtu anatoka chama gani, ama yupi anatoka chama kipi. Tunataka level ground kwa vyama vyote na huduma zipeanwe kwa serikali kwa watu, kila mtu awe hakuna kubaguliwa kwa sababu anatoka chama fulani au vipi. Hayo ni maoni yangu hayo.

Mengine mengi ambayo nilikuwa nataka kusema pia yameshazumgumzwa na wenzangu. Kwa hivyo lingine ambalo ningetaka kutilia mkazo tu kidogo ni kwamba, kwa sababu sitaki President awe above the law, mimi kwa upande wangu ninapendekeza kama wenzangu kwamba akifanya kosa apelekwe kotini kama mtu mwingine yeyote. Hayo ndio maoni yangu.

**Com. Ratanya:** Bwana Herdson Kaniki. Herdson Kaniki? Hayuko. Kuna Mwanyika, Reverend yupo? Karibu.

**Rev. Mwonda:** Jina langu ni Rev. Ndika Mwonda, mimi ni kasisi wa kanisa la kiangilikana. Nashukuru kwa nafasi hii. Mwanzo ningependekeza kwamba, Katiba ya Kenya iwe na utangulizi unaoeleza kinachounganisha watu wa Kenya. Kwa

mfano iwe kwamba sisi watu wa Kenya tumeunganishwa na common struggle, ili kuondoa bila la kusema kwamba kuna kabila fulani waliopigania uhuru au pengine wanafaa zaidi.  Iwe kwamba it is a common struggle.

Pili, iwe utangulizi ambao unatueleza national pride.  Sisi furaha yetu kuwa wakenya ni nini?  Jambo la pili ningependa tuende kwa urais.  Rais mamlaka yake, nguvu zake zipunguzwe maana ni nyingi mno.  Tena Rais asiwe anaonekana kama ni mzee wa kijiji kwa mfano KBC au vyombo vya habari vinapomtangaza Rais, kwamba amehudhuria mazishi kwa kijiji chake, amehudhuria arusi kwa kijiji chake, ameenda kanisani kwa kijiji chake, lakini Rais aonekane kama a national figure.

Na jambo lingine, linalohusikana na urais, Rais tunataka awe ni mwanakenya, mwenye miaka arobaini na tano au zaidi, na asizidi miaka sitini na tano.  Na tena Rais awe na kiwango cha juu cha elimu, awe graduate.  Pia napendekeza wabunge wawe na kiwango cha juu cha elimu.  Ma-councilor pia wawe na kiwango cha juu cha elimu, at least form four, lakini lazima wawe wameenda college fulani.  Wasiwe watu tu wamepotelea form four halafu wakaachia hapo.  Wawe wamesoma college.

Jambo langu la tatu linahusu familia.  Nataka Katiba mpya itetee haki za kifamilia.  Ijue kwamba kifamilia is the basic human unit, ambayo inajenga nchi nzima.  Kwanza, katika familia nataka niseme haki za akina mama na mabwana zote lazima zizingatiwe.  Na Katiba isigawanye nchi ya Kenya iwe kama kuna nchi mbili, nchi ya wanawake na nchi ya wanaume lakini ijenge nchi moja ambayo imeungana.  Maana tunaposema haki za wanawake, haki za wanaume inakaa ni kama nchi mbili tofauti.  Haki za watoto lazima ziangaliwe, maana kuna shida kubwa hasa, watoto kudhulumiwa, yaani kwa mfano kuna sexual exploitation ya watoto, na ambaye atapatikana na sexual exploitation ya watoto iwe ni mhubiri, iwe ni nani, lazima afungwe kifungo cha maisha.  Katika familia pia wanawake wasichukuliwe kama vitu tu vya kuwa-possessed yaani wanawake wamechukuliwa kama vitu vingine kama mashamba, vitu kama ng’ombe, mara wanapofikia wakati wa kuolewa, wanawake hupewa gharama, kama hakusoma hata nursery wazazi wake watasema basi leta shilingi elfu ishirini, maana anafananishwa na elfu ishirini.  Kama alisoma primary itasemekana leta elfu thelathini, kama alifika form four hamsini, kama alifika college mia moja, kama ni university mia mbili na kadhalika, yaani mahari yasitolewe kama alama ya kuwafanya wanawake kama vitu tu vya gharama.

**Com. Salim:**  Badala yake

**Rev. Mwonda:**  Badala yake watambuliwe kama wanadamu wenye heshima.  Chochote kile kinafanyika kifanyike kama watu wanatambuliwa kama wenye heshima.  Jambo lingine la watoto tunao watoto wanaoitwa disabled.  Ningependekeza kwamba hawa watoto wanaoitwa disabled wasiitwe disabled kabisa maana si disabled maana wana special talents.  Tuseme watoto walio na talanta tofauti lakini jina la disabled lisitumike hapa Kenya hata ikiwezekana dunia nzima.  Wengine wamebadilisha. Na hawa watoto ambao ni special talented wawe intergrated kwa shule za nyumbani mwao, badala ya kusafiri mbali kupata elimu, kwa mfano kama ni kipofu asafiri Thika au asafiri Mombasa, lakini akae pale pale kwa mazingara ambaye yeye anayaelewe na afundishwe vizuri na waalimu wasim-harass huyo special talented child.  Na hii itasaidia kwa sababu

wanaposoma kwa kufikia chuo kikuu wanapata shida kubwa kwa sababu walizoea kuwa in special schools.

Jambo lingine, linahusu elimu, elimu ningependekeza Katiba hii iweke mzigo zaidi kwa elimu yetu kwa sababu watoto wanaoenda nursery school mara nyingi wanafundishwa na watu ambao hawajahitimu masomo ya kufundisha, kwa hivyo napendekeza kwamba nursery school zote zifundishwe na P1 teachers, ambao wataingia moja kwa moja kwa TSC. Pia primary schools, ningependekeza Katiba iwezeshe watu wenye elimu ya juu zaidi pia wafundishe primary schools kwa mfano graduate pia waweze kufundisha primary schools ili tuendelee kuimarisha viwango vyetu vya elimu kama nchi zingine. Najua wengine watakasirika lakini huo ndio ukweli wa mambo kwamba graduate pia wafundishe primary schools.

Mwisho namaliza, tunayo freedom of worship. Tunafurahia hiyo lakini tungependa hii freedom of worship, iweze kuekewa vipengele fulani, ili mtu akiwa na uhuru wake wa kuabudu asiweze kuwatatiza wengine. Kwa mfano kama utapiga makelele usiku sana ukiwa unaomba na wengine wamelala kwa estate, basi mtu huyo achukuliwe hatua. Tafadhali samahani sana Local Government ningependekeza kwamba wasimamie pia mambo ya elimu na barabara pamoja na health. Asanteni sana.

**Com. Ratanya:** Asante Reverend kwa maoni yako na sasa tunamuita Lucy Mkamburi.

**Lucy Mkamburi:** Kwa majina mimi naitwa Lucy Mkamburi, ninatoka hapa Wundanyi. Mimi ni mfanyi biashara ya mitumba. Ningetoa pendekezo langu kwa upande wa biashara hii ya mitumba, biashara hii ninaona kama imedharauliwa sana na watu wa County Council. Katika County Council sijui ni hapa Kenya peke yake, ni Wundanyi peke yake ama ni Kenya nzima. Zaidi huwa tunaotoa license ya elfu moja na mia mbili na hamsini halafu na pesa za ziada zingine zinakuja kukusanywa. Umeuza, hujauzwa unachukuliwa nguo zako unanyanganywa na kupelekwa ofisini kama huna hiyo shilling hamsini. Na ambapo tukihesabu hamsini kwa kila mwaka ni shilling elfu kumi na nane. Hiyo Tumeona ni unyanyazaji.

Pili, usafiri kwa upande wa barabara hii ya Taveta. Wafanyi biashara sisi hapa Wundanyi akina mama tunapata taabu, sana kwa upande wa biashara, maana tunanyanyaswa sana. Kama kuna kifungu kinachoonyesha tufanye hivyo, tafadhali iondolewe maana unalipa license na kuna pesa zingine zinakuja kuchukuliwa hapo tunaumia na wewe ndio unayetegemewa nyumbani. Wengi wetu hapa hatutegemei mabwana zetu maana bwana akipata pesa haangalii nyumba. Bibi mwenyewe ndio anayetegemewa ndani ya nyumba hiyo. Tena biashara ya kuenda Taveta hadi Wundanyi. Barabara hizo zimetengewa pesa kwa muda mwingi lakini hizo pesa hazitengenezi hiyo barabara. Nataka ikiwa kuna mtu amepitiwa pesa na hajatumia katika barabara hizo na hataki kutengeneza barabara hizo tafadhali mtu huyo achukuliwe hatua na ashitakiwe na kulipa hizo pesa.

Kwa upande uchumi, kwa mfano mikopo. Mikopo itolewe ya kusaidia akina mama, na asilimia ya hali ya chini. Mikopo inatolewa na iko juu sana hata akina mama tunashindwa kuchukua mikopo na kwenda kujisaidia kwa upande wa mashamba.

Upande wa matibabu yaweze kuwekwa free, yawe na madawa ya bure. Clinics za watu binafsi ziondolewe na kutupiliwa

mbali. Tuwe na kutegemea hospitali peke yake.

Kwa upande wa ma-chiefs, wawe wakichaguliwa na wananchi peke yake. Na tusiwe na sub-chief. Chief mwenyewe anatosha peke yake. Raping. Mwanamume au mama akipatakana amenajisi mtoto mdogo, tafadhali achukuliwe na ashtakiwe na kifungo chake kiwe ni kifo au kufungwa maisha. Traffic barabarani. Traffic Police barabarani hasa barabara ya kutoka Wundanyi kuelekea Mombasa wamezidi. Tuwe na kituo kimoja cha traffic, na hao traffic wasiwe ni watu wa kuhongwa hongwa. Wawe ni watu wameandikwa kazi na wasiwe wasitegemee hongo. Mshahara wake unatosha. Mwenye matatu tafadhali asiruhusiwe kutoa pesa na kumuhonga traffic.

Upande wa uchumi wa hapa Kenya. Mwanakenya yeyote, Rais au wabunge au mawaziri au kuna waziri au mkenya yeyote asiruhusiwe kuwa na account katika nchi za nje. Account zote zifunguliwe hapa Kenya. Asanteni.

**Com. Ratanya:** Sasa namwita Bwana Samuel Mwamburi, Samuel Mwamburi? Yuko? Richard Mwangi, hayuko? Philip Mbale? Ametoka? Nasikia ametoa memorandum akaondoka kwa hivyo tutampatia alama ya kukuweko. Tutamwita Hassan Mukara, Hassan Mukara? HarrisonMwachala, HarrisonMwachala? Huyo ameondoka. Victor Mkanguo? Hayuko. Dorothy, Dorothy yuko? Dorothy Mwadio sasa tuko na taabu ya kusoma majina. Yuko Dorothy hapa? Ameondoka? Alright. Esther Chovu yuko, karibu Esther. Olefiwa Risanga, Olefiwa Risanga? Yuko? Karibu. Edwin Lenjo? Hayuko?

**Raymond:** Commissioners wa Katiba, masame coordinator, na Waisanga wose mwasinda mana? Nashukuru wote ambao mumekuja, kuchangia hii mambo ya kugeuza Katiba, hasa nashukuru akina mama kwa mfano Mary Mwamodo, Mwamburi na wengine, wazee na vijana na walemavu wote. Walemavu mimi niko na personal views, ndio maana nasema nasikiza sana walemavu maanake mnajua kijana wangu vile wengi wenu mnajua, ni mgonjwa na yuko blind kwa hivyo ninasizitiza sana walemavu pia wawe kwenye hii Katiba. Kwa sababu ya muda mchache nitasoma memoranduma ya wazee, Council of elders ya Taita Taveta ambao wamenitumia mimi kama mjumbe wao. Mimi kwa majina naitwa Raymond Mwangola, natoka Mbale, Wundanyi Constituency. Kwa sababu ya muda nitafupisha maneno hapa ingawaje memorandum yetu ni ndefu kidogo, lakini niwie radhi kidogo nitoe dibaji ambaye ni introduction ni wasomee kidogo muelewe ya kwamba vile tulivyokutana na tumekubaliana.

Dibaji ni kwamba sisi wajumbe wa Waisanga tukiwa watu kadhaa, ni kwamba na tukiwa tunawakilisha wilaya yetu yote ya Taita Taveta na pia tukiwa tunawakilisha sehemu mbali mbali hasa viongozi wa vijana, wazee, wanawake, dini, siasa, elimu, wafanyi biashara, wafanyi kazi na walemavu. Those people who will interfere kwa sisi watu wa mkoa wa Pwani, tuna utajiri mkubwa sana, na kwa karne nyingi za kihistoria na wa utamaduni. Tukitambua kuwa kwa miaka thelathini na saba tumeonewa sana, tumenyanganywa sana, tumeporwa sana, tumepuuzwa na kudharauliwa sana, tumenyanyaswa sana katika nyanja zote za kisiasa; kijamii, kiuchumi, kielimu na kwa kila hali. Huko tukiwa na nia ya kuunda umoja na ushikamano wa kupambania haki, usawa, maisha, na kiutu na maendeleo. Tukizingatia kuwa kuna haja kubwa sana, ya kuwa vuguvugu la mageuzi na Katiba

mpya ya kitaifa na kutushirikisha kikamilifu kama wananchi na kama binadamu katika harakati za kuleta Katiba yenyewe. Huku tukitambua kwamba kuna njama ya kuwazuia wananchi, kushiriki kikamilifu katika kuandika Katiba ya kitaifa ambayo inahusu kila mtu nchini. Katika kongomana hili, la kihistoria hivi leo tunaafikiana na kuazimia ifuatavyo. Azimio kuhusu swala la Katiba mpya. Mtanisamehe sana ni ndefu lakini nimechukua point mbili tatu ili ya kwamba tufupishe kulingana na wakati na watu wamechoka na najua watu wamekuwa na njaa sana hata macommissioners naona wamechoka choka sana wanaharakisha watu. Haya basi asante.

Azimio kuhusu Swala la Katiba mpya, ni kwamba tuwe na Katiba ya mfumo ya utawala wa majimbo Kenya ikiwa na maana hii ………

**Interjection:** ------------- inaudible

**Raymond:** Kwamba kila mwananchi wa Kenya awe na uhuru wa kuishi na kuwa na mali popote nchini atakapochagua yeye mwananchi. Katiba mpya ihakikishe, kwamba kiongozi yoyote yule wa kitaifa kuanzia Rais, Waziri Mkuu, mawaziri, wabunge, madiwani, mabalozi na kila anayeshikilia wadhifa wa umma, watatolewa kutoka kwa nyadhifa zao wakati wowote ule, ikidhibitishwa kuwa wanashindwa kutimiza majukumu yao ya kazi ya umma.

Katiba mpya ihakikishe wananchi wana uwezo wa kuwashtaki na kuwanodoa madaraka Rais, waziri mkuu, mawaziri, wabunge pamoja na kila anayeshikilia wadhifa wa umma, punde wapatikanapo na makosa.

Azimio kuhusu ardhi na rasilmali yetu. Pwani imetunukiwa rasilmali nyingi ambazo zikitumiwa vizuri kwa manufaa ya watu wa Pwani na ya kitaifa, zitasaidia kuondoa umaskini na kuleta maendeleo na ufanisi mkubwa nchini. Rasilmali hizi ambazo tuko nazo hapa Pwana ni wananchi wa Pwani wenyewe, utamaduni, ardhi, madini, mbuga za wanyama wa pori, misitu, mimea na mazao ya ardhi, viwanda, maandari, mahoteli na utalii, mifugo, masoko, bahari na rasilmali zake na bandari na kadhalika. Rasilmali zilizoko Pwani ni haki ya wapwani na hivyo wapwani watapambania haki za kuhakikisha kuwa, wanafaidi ipasavyo kutokana na rasilmali zao. Azimio kuhusu maswala yao, huduma za afya---

**Interjection:** ------------------------------------ ( inaudible)

**Raymond:** Sisomi yote nasoma point, haya ni point mimi nasoma. Huduma za afya. Kuwe na matibabu na madawa ya bure. Naona vile ninaharakisha Bwana commissioners. Wacha nipunguze kidogo. Kuhusu elimu. Kuwe na elimu ya bure kuanzia shule ya vidudu hadi ya msingi. Kwamba mfumo wa elimu ya 8-4-4 uondolewe na badala yake tuwe na mfumo wa 7-4-2-3. Walemavu wapewe elimu bure kuanzia vidudu mpaka chuo kikuu. Lingine ni swala la wakulima. Wakulima tunasema ya kwamba serikali itoe kikorobezo na kuendeleza kilimo kwa kuhakikisha wanatekeleza michango ya kuhakikisha wakulima wana ardhi ya kutosha, mbolea, mbegu bora, vifaa vya kisasa kama sector na ushauri kuhusu kilimo bora. Kuhusu fedha.

Serikali atakayepatika amekwepa kulipa ushuru wataifa, akamatwe ashtakiwe, ahukumiwe na mali yake itaipishwe mara moja.

Mazingira: Tuwe na sera na mkakati wa kimaendeleo na kulinda na kuifadhi mazingira kwa ajili ya vizazi vya leo na vijavyo. Mali asili, kwamba mali ya asili inufaishe kwanza mwananchi wa sehemu mali asili hizo zilipo. Kisha na taifa lote kwa ujumla.

Azimio kuhusu maswala ya utawala na uongozi. Kwamba wananchi kutoka mashinani washirikishwe katika kuhifadhi na kusimamia rasilmali, ulinzi, na usalama, mahakama na kuathiri sera za kitaifa. Pia kwamba wananchi kila pahali na kila kiwango wahamasishwe kutetea maslahi yao, utawala wa kidemocrasia na uhuru wa kitaifa. Azimio kuhusu Kenya tuitakayo, kuwe na kuelimishwa kuhusu Katiba, kwa mikutano ya hadhara. Kuwe na kuelimishwa kuhusu Katiba katika makundi au mashirika yaliyoko, kama kadhalika ya vijana na kadhalika.
Azimio kuhusu nyongeza. Kusiwe na ubaguzi wa kikabila, kirangi kidini au kijinsia katika kupeana hati za kitaifa kwa wananchi kama vipande, card za kura na passport. Azimio nafikiri la mwisho ni kwamba baraza la …(inaudible) Waisanga, Council of elders, elders Taita Taita, pamoja na washiriki wake wa Taita Taveta tuna laani chama zozote zinazofanya na kuwapora wananchi wa Pwani na wakenya haki zao ya kusiriki kikamilifu katika uandaji wa Katiba mpya ya kitaifa. Na pia kwamba kwa sababu hii, sisi wataita tuliokusanyika hapa leo, tunaunga mkono juhudi zozote zinazofanywa na mtu yeyote yule au shirika lolote lile, kupigania Katiba mpya ya kitaifa tuitakayo. Katiba itakayoundwa na wananchi wa Kenya wenyewe. Azimio hili limejadiliwa na limeshirikishwa na kongomano la kwanza la council of elders Taita Taveta mnamo tarehe kumi na moja, mwezi wa kwanza mwaka wa 2002. Asanteni sana.

**Com. Ratanya:** Asante sana Bwana Mwangola kwa maoni yako kwa niaba ya chama chako na tukiendelea mbele, tutamwita Bwana Michael Mwandembo. Yuko?

**Michael Mwandembo:** Kwa majina mimi naitwa Michael Mwandembo kutoka hapa Wundanyi. Mapendekezo yangu ni kama ifuatavyo. Katika Katiba mpya ambayo tunayoitayarisha ningependelea kuona kwamba pombe hii ya kienyeji, lazima imehalalishwa na pia license kutolewa ili kufuatia mawazo yetu ya kitamaduni tuchanjie katika uchumi wa jamii yetu. Pia ningependelea kuona kwamba, tungekuwa na serikali ya Local Government instead ya Administration, Provincial admninstration. Pia Rais, ningependelea kuona kwamba hangejihusisha na siasa za vyama, bali angekuwa ni Rais ambaye si wa chama chochote cha kisiasa.

Katika swala la umilikaji wa ardhi, ningependa kuonelea kwamba wananchi wa kawaida, lile shamba lake ambalo amemiliki, basi liwe ni lake na wakati kama serikali iko na mipango ya kulitumia, asije kutatizwa. Serikali lazima iafikiane na mwananchi, huyo na wakubaliane, ndio wawe njia ya kuchukua shamba lake. Katika Katiba pia ningependa kuonelea kwamba kuna inalinda sana na kuchunguza viongozi wa serikali. Yeyote ambaye atakaye afikiwa, au atakayehusika na kashifa zozote za corruption, basi asiruhusiwe kuchaguliwa kuwa President au nominated, an elected katika ofisi yoyote ya kiserikali. Halafu kwa shughuli za kisheria, ningependa kuanzishwe tume ya kusimamia shughuli za kisheria, Judicial Council, ambaye itahusika

kusimamia mienendo ya ma-judge na pia kuwadhibu wakati wamefanya makosa, wameenda kinyume na sheria. Pia kutakuwa tuseme Judge mkuu, ambaye atachaguliwa na Rais, sasa hiyo inakuwa anachanganya shughuli za kiserikali na shughuli za kisheria ambapo sasa haijulikani. Halafu adhabu ya Chief kama ingewezekana tafadhali, Katiba siku ijayo adhabu ya Chief itolewe. Na Katiba lazima ihakikishie raia, ipatie mwananchi raia uhuru wa kutembea na kuongea kama kutoa maoni.

Katika mambo ya elimu, elimu ingetakikana iwe ya bure kuanzia kiwango cha nursery school, ikiwezekana mpaka primary level. Hayo ni mapendekezo yangu na asante sana.

**Com. Ratanya:** Asante, sasa tutamwita Bwana Julius Mwanyia. Julius Mwanyia? Ashaondoka. Tunaomba wale wajamaa ambao wataondoka wajua kwamba kesho tutaendelea kuwa hapa Wundanyi pahali pengine na tunaomba watafika kutupa maoni yao huko. Sasa tamwita Bwana Yuta Mwambugu. Oh kabla ya hapo samahani kuna jina hapa limecharazwa kama sign. Tony Tole, Tony Tole yuko? Karibu.

**Tony Tole:** Hapa nina maoni yangu binafsi hapa ambaye inasema kwamba mamlaka Rais yapunguzwe.

**Interjection:** -------- (inaudible)

**Tole:** Mimi kwa maoni yangu ninaona mamlaka ya Rais yapunguzwe, na tena ningependelea awe chini ya sheria, na akifanya kosa lolote ashtakiwe, apelekwe mahakamani kama mwanadamu yeyote. Na uhuru na maamuzi ya Rais kutumia mamalaka ya (inaudible) uhuru wa (inaudible) kuwa wanasheria na sasa tunaagizwa. Mkuu awe ameteuliwa na Tume ya serikali.

**Interjection:** ----------- (inaudible)

**Tole:** Jambo lifae kuwa mkuu wa sheria atabaki kuwa afisa aliyeteuliwa na Tume kwa kufanya kazi zake za mshauri mkuu wa kisheria wa serikali. Rais apokonywe mamlaka aliyonayo, kuwafuta watumishi wa umma. Jukumu lake ni kuwa futa kazi au kuwaadhibu watumishi wa umma, awachiwe Tume ya utumishi wa umma. Mamlaka ya Rais --

**Interjection:** -----------inaudible

**Tole:** Jukumu ya kuwafuta kazi ama kuwaadhibu watumishi wa umma kuna paswa kuachuwe badala ya Rais kufuta Tume ya utumishi wa uma. Bunge linapaswa kuwa na staff maalum, au linahitaji kujiaangalia ratiba ya vikao vyake. Wadhifa wa sasa wa Rais, kwenye mamlaka, unapaswa kuvunjiliwa mbali, na mahali pake kuchukuliwa na waziri mkuu. Rais nafasi yake itachukuliwe na waziri mkuu. Rais atakayechaguliwa na wananchi atakuwa baba wa taifa asiwe na uwezo wa kuendelea, asiwe na uhusiano wa chama chochote cha kisiasa. Mamlaka ya Rais yatakuwa ni ya kisherehe kama vile kuwalaki waeni mashuhuri, kutoa tuzo za kiheshima, na nishani, na kuongoza ufunguzi rasmi wa vikao vya bunge. Kuna haja ya kulipatia bunge mamlaka

ya kufunguliwa mashtaka Rais, na ikiwa anapakipatikana na hatia tumlazimishe kujiuzulu kwa sababu ya kufunguliwa mashtaki ya rais ni pamoja na ukiukaji wa sheria, au Katiba au kuhusika na ufisadi wakati wa utumishi wake. Waziri mkuu, mwenye mamlaka makuu atakuwa kiongozia wa chama cha kisiasa kinachopata ushindi mkubwa wakati kura zikipigwa. Wabunge watakuwa na uhuru wa kumfuta waziri mkuu akiwa hasimamii serikali.

Jambo lingine ni juu ya sheria. Sheria lazima imulinde mwananchi yeyote mkubwa hata mdogo na rasilmali za wataita hii zinufaishe wataita wenyewe. Madini, National Parks, gate fees, land ownership. Yaani ninasema kwamba sisi hapa wataita tumenyanyaswa kwamba 62% ya National Park, gate fees hatupati, yote inaenda Nairobi. Kwa hiyo tunaona ni haki, hii mali, hizi pesa zetu ambazo zinakusanywa hapa, turegeshewe sisi at least if we can get 75%. Jambo lingine ambalo linaharibu uchumi wa taifa, ni kwamba serikali imetunga mambo ya VAT, ndio naona biashara zikaporomoka namna hii, unaeza kuta mtu amefanya biashara analazimika kulipa VAT na anakuja anafanyiwa assessment yake, pengine unakuta ameshikiwa vitu vyake anataka kuna diwa. Kwa hivyo mimi naomba Katiba ya VAT iondolewe, na itafutwe njia nyingine ya kukusanya kodi kuliko kuwekelea wananchi VAT. Na kusema mgawanyiko wa cost-sharing katika hospitali, unaona hauna maana yeyote kwa sababu, unakuta wananchi wanatoa pesa kwa hospitali, wanalipa kisha akifika kule anaambiwa hakuna dawa, anaagizwa aende kwa private clinic. Kwa hivyo aina maana. Tungeomba kulingana na serikali ya kale ilikuwa inatwambia ati madawa ni bure kula ni bure, ninaomba wakati huu wanapojiita new kanu ------ (**tape Stopped**). Tungeomba pia tuletewe daktari hospitali maana hatuna madaktari na watu wetu wanakufa usiku na mchana. Ni hayo nilikuwa nayo.

**Com. Ratanya:** Asante Bwana Tole, sasa Bwana Nyusa Mwambuku? Ameondoka. Andrew Malago.

**Andrew Malago:** Kwa jina naitwa Andrew Malago kutoka Mgange Location. Mapendekezo yangu kuhusu urekebishaji wa Katiba, kitu cha kwanza mimi napendekeza majimbo. Majimbo tunayo nahitaji kwa sasa ni kusimamia rasilmali na kushirikisha kwa mwananchi mdogo kuanzia chini, uamuzi upewe mwananchi, hasa kwa kusimamia rasilmali zake, kama vile tulivyo na mambo ya Tsavo National Park, tuwe na mambo ya madini, ardhi na maji, na uajiri tunajua ya kwamba uajiri umekuwa haba sana kwa mikoa hasa huku Pwani na wilaya ya Taita Taveta, kwa hivyo ningependekeza kwamba utaratibu wa kusimamia rasilmali tupewe uajibikaji kuanzia wilayani.

Jambo la pili ni kuhusu mamlaka au uwezo wa Rais Moi. Rais wetu yeyote yule atakayekuja kesho awe chini ya sheria, asiwe juu ya sheria. Lazima sheria iwe kwa kila mtu, mtu akifanya kosa fulani, sheria ichukue wadhifa wake. Utawala, kuhusu mambo ya utawala, ningependekeza tuanzie uchaguzi kama ni Assistant Chief, achaguliwe na wananchi kama vile tunavyochagua wazee wa vijiji. Chiefs wachaguliwe na mwananchi, D.O. achaguliwe na mwananchi, D.C. achaguliwe na mwananchi pamoja na P.C, ili kusudi kama mambo ya maendeleo ya wilaya ianzie kwa mwananchi wa Kenya kabisa. Mambo ya maofisa ama mfanyi kazi mstaafu ningeomba kwamba serikali iwe ikizingatia malipo ya yule mtu ambaye amestaafu vila anapewa notice, barua ya notice iambatane na malipo yake alipiwe mahali amefanyia kazi. Retirement, siku ile anenda ku-sign anatoka kazi basi apate cheki zake hapo hapo, bila kushurutishwa kwenda Mombasa, Nairobi, au mahali pengine, isipokuwa

kulingana na ile ofisi yake mahali anafanya kazi. Halafu ni kwamba akisha-retire asiruhusiwe kupatiwa nafasi yoyote ya kazi. Kuna vijana wengi ambao hawana kazi, mtu akisha-retire apatiwe nafasi ya kupumzika nyumbani, asipewe uwezo wowote, wala ashishughulikiwe.

Mambo ya ufisadi: napendekeza kwamba mtu yeyote atakayepatikana na ufisadi, kama ni ofisa anafanya kazi ofisini, ameomba kitu kidogo ashtakiwe na alipie jina la serikali kwa kulichafua, agharamike kwa kufungwa isiyopungua miaka miwili au mitatu, kwa ufisadi, na yule ambaye anachelewesha kama ni malipo ya mtu fulani, naye ashtakiwe kwa kuharibu jina la serikali ama la ofisi maana tayari amechafua jina la serikali kwa ufisadi na kutumia njia mbaya kwa wadhifa wake pale.

Mambo ya police, na ma AP na GSU, tunaomba ishirikishwe ziwe pamoja badala ya kugawanya GSU, CID, AP, iwekwe kuwa kitu kimoja. Mambo ya elimu, ningeliomba elimu isimamiwe kikamilifu, maana elimu imezoroteka sana, na hatuoni dalili zozote nzuri na manufaa ya elimu kesho. Usimamizi umekuwa mbaya, kwanza hasa usimamizi wa B.O.G na PTA, wanapochaguliwa kupitia uwezo wa wabunge, hawa wanasiasa ndio wanazorotesha elimu maana wamechagua mtu ambaye yeye anakusikiza lakini haizingatii elimu ama manufaa ya watoto au ya elimu. Kwa hivyo ningezingatia kwamba BOG na PTA iwe ikichaguliwa direct na wazazi wenyewe wanaohusika na shule hizo. Mambo ya usimamizi wa pesa umekuwa mbaya kwa sababu waalimu wakuu wamekuwa na nafasi kubwa ya kusimamia pesa za shule na imekuwa badala ya kutekeleza wajibu wao wa ualimu au elimu, wanazingatia kuangalia hazina ya shule iko namna gani, badala ya kutekeleza wadhifa wao wa elimu, wanatekeleza corruption na utumiaji mbaya wa pesa. Kwa hivyo elimu, BOG ingesimamia hizo pesa wao wenyewe, ningependekeza BOG isimamie, kuanzia mwenye kiti achaguliwe na wazazi, chairman, secretary na treasurer awe ni mzazi amechaguliwa na wazazi wenzake. Kwa hayo machache, yangu ni hayo tu. Asanteni.

**Com. Ratanya:** Bwana Holliness Wakesho. Holliness Wakesho? Ameondoka. Robert Mwamburi?

**Robert Mwamburi:** Mimi ni Robert Mwamburi kutoka……(inaudible) location. Mengi niliokuwa nayo yamesemwa na wengine na nitapitia tu, kwa mara moja yale ambayo ni ya msisitizo. Pesa za Taifa, ningependekeza pesa za Taifa ziwe na jina la mwanzilishi wa taifa. Lisiwe linabadilika badilika.

**Interjection**

Habari ya Katiba, urekebishaji wa Katiba, ningependa Katiba hii pia igusie ile nyingine ya mwanzo kabisa kutoka Lancaster House ambayo inazungumza juu ya majimbo, yale ambayo yangeondolewa ya majimbo ama kwa mfano President. Majimbo tuseme hiyo ingerudishwa. Regional assembly tuwe na nyumba mbili.

Katika wizara za serikali, kusiwe na wizara moja na mawaziri wawili. Iwe ni wizara moja waziri moja na naibu wake. Iwe ni mtu mmoja, kazi moja isipokuwa kazi ingine mtu anaweza kufanya iwe kama ya binafsi, ya kilimo au ufugaji. Lakini katika kazi

za serika ni kazi ya mtu mmoja. Bei za vitu nafikiri zirudishwe na bei iwe ikisimamiwa na serikali kwa mfano nyama, karo na mambo mengine kama hayo. Kila kabila la Kenya lina uhuru wa kukaa au kuishi mahali popote na kabila lile na pia mahali na kabila akipatiwakibali na kabila hilo. Uhuru wa kuabudu uweko, lakini uwe uhuru wa kuabudu Mungu. Uhuru wa kuabudu mashetani, upigwe marufuku kabisa.

Siku za kitaifa ziwe tatu; Madaraka Day, Kenyatta Day na Jamuhuri Day. Serikali za wilaya ziwe chini ya regional Government pamoja na land committee. Hiyo ingine imekwisha semwa. Kila mkenya awe na uhuru wa kupata matibabu ya bure. Halafu kuna huduma zingine zimeondolewa kama katika kama katika Posta. Ningependekeza ile Telegram, irudishwe, na …(inaudible) certificate iandikishwe. Hizo huduma mbili zimeondoka na ni za muhimu hapa nchini. Kuhusu Post Bank. Ningependekeza ingerudi kama kitambo iwe katika Africa ya mashariki, Mtu anaweza kutoa pesa Uganda, anaweza kutoa pesa Kenya, anaweza kutoa pesa Tanzania.

Mara nyingi tunazungumzia habari ya Chief, lakini Katiba ile ya mbeleni hii huduma ya Chief haiko. Ningependa pia katika urekebishaji huu pasiwe na huduma za Chief. Basi kwa sababu ukulima ni uti wa mgongo wa Kenya, idara ya ufugaji na ya kilimo ipewe jukumu hata kwa kujitungia sheria za kuporesha kilimo nchini, au kwa mfano sheria ya milulu kama wakati wa mkoloni kulikuwa na watu wakupima milulu, na ilikuwa inaonekana kwamba hiyo isibomolewe mweleo ili ilete sura nyingine kabisa ya kilimo. Kufanya kazi iwe raisi ya utawala. Nafikiri kama Councilors waliochaguliwa, pamoja na wafanyi kazi wa kilimo, halafu washirikiane na viongozi wa kijiji. Kama kijiji kimekuwa kikubwa basi tutumie mtindo au nyumba kumi kumi kama jirani wetu wa Tanzania.

Hivi leo pombe za kienyeji zingerudishwa, lakini kwa mtindo mwingine. County Council ijenge vilabu, kuwe na saa kama zile za mwanzoni, tuwe tukitoka asubuhi mpaka jioni, kutoka saa sita mpaka saa mbili halafu wale wanaotengeneza wapelekwe huko kama majirani wetu wa Tanzania, wawe wakija huku na kununua. Kama wanawake ambao wanauza, au wanaume wanaosimamia huduma hiyo wapelekwe huko sokoni au kuliko jengwa wauzie huko, badala ya kuuzia nyumbani.

Vitu vya anasa, vingefaa vichunguzwe. Kuna vitu vingine vya anasa vyakwazana vijana au watoto, kama video. Pakitolewa license iwe hata zile zinazofaa kwa watu wazima ziwe restricted kwa watu wazima. Lakini isiwe picha nyinginge zinaonyeshwa watoto ambazo zina wakwaza. Hata vitu kama kwa mfano condoms Kenya hazingefaa kuuzwa kiholela. Pangekuwa labda katika kila sub-location duka itawekwa lazima wawe ni watu wazima, sio vijana au watoto. Zingine zina swali. Elimu kwa maoni yangu, ningependa Tume ya kuajiri waalimu iwe inachunguza haki za walimu, mishahara yao, lakini elimu isimamiwe na wamishenari kama zamani. Halafu elimu ya uraia, pia iwe inafundishwa madarasani. Iwapo Katiba hii tutakayounda itataka au inapaswa kurekebishwa, ningependekeza iachiwe miaka kumi na tano ifanywe kazi kwanza, halafu baadaye kama upper house itapishwa kura 75%, na senate kwa 90% halafu ndiyo tuweze kuwakisha Kenya lakini ichukue mtindo huu irekebishwe na kila mtu.

Langu la mwisho ni uhai. Uhai ni Zawadi ya Mungu. Ningependekeza pasiwe na adhabu ya kifo adhabu ya maisha, mwisho kabisa, hukumu ya maisha. Ingine ni kuhusu ndoa. Kwa sababu tuliambiwa hawa warekebishaji wa Katiba wanaweza kuchukuwa jambo (inaudible) hilo ningependa liwe jambo (inaudible) Asante.

**Com. Ratanya:** Asante sana kwa maoni yako, na sasa tutwamwita Bwana Wisdom Mwamudua, Wisdom yuko? Fred Mwarabu? Fred Mwarabu.

**Fred Mwarabu:** Mimi vile mumesikia majina yangu ni Fred Mwarabu kutoka hapa Wundanyi. Tayari kuna moja ya yale ambayo nimeyaandika naona yashazungumzwa lakini pengine nitagusia. Katika utumishi wa umma, utaona kwamba wazee wengi ambapo wanapostaafu, hupata bughudha sana wa kuenda Nairobi, kuenda kudai malipo yao ya miaka. So pengine ningesema hivi, wakati Katiba hii inapotengenezwa upya, wakati mtu anapokaribia ku-retire au kustaafu, huyo mtu tayari mambo yake, file yake, kila kitu chake kirudishwe kwenye idara yao ili kwamba malipo yake yasimtatize maana wengi wao wanapata bughudha kuenda Nairobi, na hata Nairobi huko hawakujui.

La pili ni hiyo pension basi. Pengine itayarishwe baada ya mwezi mmoja, maana watu wengi hupata dhiki. Mtu akikuja ku-retire, hakuna, asahatolewa kwenye payroll, halipwi chochote, atakuwa akingoja pesa zake miaka nenda miaka rudi, wengine hata huenda wakafa hata kabla hawajaona hizo pesa zao. Kwa hivyo kama baada ya mwaka mmoja alipwe.

Kuhusu training ya police na prisons. Ningeomba kama ile syllabus yao yaweza kubadilishwa kidogo kwa sababu most of them wako na ile brutality sana. Kwa hivyo kama yaweza kubadilishwa ya police na prison, ndio public relation yao pia iangaliwe.

Langu la nne ni katika mambo ya passport na driving license. Ningeomba kama vitu hivi viwe vikitolewa katika wilaya, sio tuvifuate Nairobi. Sisi huwa twatatizika sana kutafuta passport, na driving license. Itakubidi kwenda Nairobi, huna pahali pa kulala, hujui uwende kwa nani, halafu tena inachukua muda mrefu zaidi.

Langu la tano ni shule za kitaifa. Jambo la kusikitisha katika mkoa wa Pwani hakuna shule hata moja ya kitaifa. Ningeomba kwamba shule za kitaifa ziwekwe katika kila wilaya at least one in every district. Jambo lingine hapa ambalo limesemwa semwa lakini pengine nitalizungumzia kidogo. Katika kila sehemu nchi ambapo kuna rasilmali, ingekuwa vyema igawanyiwe kiwango fulani. Pia rasilmali sio ni mambo ya wanyama tu wa porini mbuga nini na nini. Utaona hasa katika mkoa wa Pwani, kuna Msinga Spring ambao ndio nafikiri ndio inapatia watu maji huko Pwani hapa Mombasa. Tungeomba kwamba kiwango fulani pia katika hiyo revenue ambayo inatoka katika rasilmali za maji, iletwe katika district hii, na pia sehemu zingine ambazo zina rasilmali kama hizi, wawe wakigawanyiwa, automatically bila mambo ya kupitishwa bungeni nini, nini, hiyo si namna hiyo.

Langu la mwisho ambalo ni la saba, wabunge na mawaziri wawe wakiwa penalized, wakati hawaudhurii vikao bila sababu maalum. Tukawachagua and they are earning a lot of money, and they are not representing us properly. Wawe penalized.

They should be deducted their salaries for the days ambapo hawa-attend hizo meetings. Asante sana.

**Com. Ratanya:** Asante Bwana Mwarabu, tutamwita Bwana Alex.

**Alex:** Nashukuru Commissioner, Chairman, Vice-Chairman yuko hapa, ndugu zangu wote ambao mko hapa. Mimi kwanza nataka kuuliza Bwana ma-commissioners kabla sijaanza jambo lolote, hii Commission kamili is it biased ama haya mambo tutakuwa tukitoa kweli yatazingatiwa. Ningeuliza hilo swali kwa sababu kama kweli kama (inaudible) kidogo. Naomba kwamba, nauliza kwamba tuseme haya maoni tunatoa kuhusu Katiba, ile ukweli mnaweza kutuhakikishia kwamba yataweza kufika huko na kuzingatiwa kweli ama tunasema tunaweza kushinda kutwa hapa lakini kumbe yote tunayoongea yakifika huko hayana maana yoyote. Ningeomba kidogo mnithibitishie kabla sijaongea.

**Com.:** ---------------- inaudible

**Alex:** Asante sana maana nilikuwa na wasi wasi kidogo kwa sababu mwajiri wenu pengine mnaeza kuwa mnazingatia zaidi. Okay sasa mimi ningetaka mambo fulani lakini nimeona kwa sababu tumekaa sana sisi ambao tumeshinda hapa kutoka asubuhi lakini vile time yetu imefika, naona kama mengi yameshaongewa na ndugu zangu wengine. Ingawaje nitapitia kidogo kidogo pia kuongezea, basi yangu ni kama haya; mimi ningependa kitu cha kwanza kuongea juu haya madini yetu, ambaye yako katika wilaya ya taita Taveta. Haya madini yetu ningetaka kwamba ingekuwa kabla mtu yeyote hajafanya ile prospect yaani kuanza kuchimba, ama shughuli yeyote, kwanza apitie kwa kamati maalum ambayo iliyoteuliwa na wananchi wa Taita Taveta, kwanza aongee nao na waweze kumkubali, na hiyo barua ndio wanaweza kuenda nayo katika ministry ya Natural Resources Nairobi, ili apewe hiyo exploiting license. Lakini hawezi kupewa kabla hajaonana na hawa elected committee ambayo itakuwa inahusiana na mambo kama hayo.

La pili mengi ni kama imerudiwa sana lakini ni kama haya mambo tunayasema kweli kila wakati watu wa kwetu hasa wanaoishi huko chini, karibu na mbuga za wanyama wa porini na wale wanaishi areas kama Mgange, Mwakitaua huko kwote, hao watu hasa wanapata shida sana. Mara nyingi wale wanyama wakiharibu mimea yao, wao wenyewe hawalipi chochote lakini ikitokea tu ka-dik-dik kameruka hadi shambani mwake. Pengine aliweka mtego kwa sababu sasa mara nyingi kwa kawaida vile wanakula vyakula vya watu pale, watu wengi wanaweka mitego ya wanyama, sasa basi anaeza hata amepata mboga akatengeneza, basi inakuwa shida haswa sana hawa watu wa Game reserve wakija pale wanaweza kukusumbua sana na hata kumlazimisha pengine kama mama mwingine alipoongea hapa kwamba atakula nyama hiyo mbichi. Hiyo mambo tungeona kwamba wanyama wale wadogo wadogo ambao wameruka kwa bahati mbaya wakaingia shambani kwako, yule unaweza wachiwa tu ukafanya mboga badala ya kuchukuliwa na sheria.

Mambo ya corruption. Tuseme katika Civil Service, civil servants actually na mimi naamini kabisa kwamba motive wa civil servants ni watu wanaweza kufanya kazi kwa bidii na bila shida yoyote. Lakini shida kubwa hii ni hasa corruption imeingia,

kwa sababu civil servants wanakuwa lowly paid. Mishahara ya wafanyi kazi wa serikali iko chini sana. Hiyo mishahara ni duni sana kwa mtu ambaye pengine kama miaka iliyopita kabla family planning, maana hata mimi nikisema familia yetu tuko football team, in total watu kumi na moja, ukiongeza baba na mama tutakuwa kumi na tatu. Sasa kwa hivyo hiyo kweli kwa mshahara ya civil servants hauwezi kweli kulinda hao watoto wote kama ilivyo. Mimi ningeweza kusema kwamba, kama ingewezekana mshahara wa chini sana wa wafanyi kazi wa serikali ungekuwa shilling elfu kumi.

Pia lingine ambalo limegusiwa pia na msemaji hapa, pia nitaliwasilisha kwa kulitia mkazo ni about hizi private commodity prices, prices za commodity ambazo tunatumia. Kama mimi tuseme uwezo wangu uko chini, na kulingana na mapato yangu siwezi kununua sukari ya hamsini. Kuna mwingine anaweza lakini mimi sijiwezi, pengine mimi uwezo wangu ni wa shilling kumi. Basi kila viwango vile vya bei viwe kwamba vinazingatiwa na zinakuwa controlled na serikali, ili kila binadamu aweze ku-purchase kitu chochote kile anachotaka. Iwe katika bei ambapo kila mwananchi anaweza kununua sukari na kula chakula vizuri na kuishi mahali pazuri. Pia mimi ningesema kwa Tume ningetoa pendekezo moja kwa hii hii Tume yenu, kwamba mara nyingi tunakuja hapa, tunakuwa kweli wengi na tunaongea lakini saa nyingine pia kuna wengine pia wanashindwa kufika. Kitu ya kwanza ningeomba, hii civic education, hii elimu ya jamii katika kuelezana mambo ya hii Commission na mambo ya Katiba. Nimeona kuna wengi sana mpaka leo hawajaelewa, na hata hawajui kwamba Katiba ni kitu gani. Ni aibu sana tunakaa sana tunafanya hii mambo hapa lakini mimi ningesema katika constituency ya Wundanyi, sijaona hiyo elimu ikifanywa mahali popote. Kwa hivyo kuna wengi sana hawajaelewa hii maneno mpaka leo.

Tena jambo lingine ningesema ni kwamba hii Review Commission, kama ingekuwa mapendekezo yangu, ingekuwa vizuri zaidi, kwa sababu katika kila kijiji tuko na vyama na kamati, ambazo tumezichagua kabisa. Tunaweza kukaa kwa kila kijiji tukajaribu kuunda memorandum yetu moja tupitishe ule mkutano wa kijiji, ambapo tunaeza kuchukua maoni ya kila mwenyeji wa kile kijiji na tukaja sublocation level mpaka Locational level, mpaka sasa tunapofika constituency level. Ili zile memorandum zetu zote tuziweke pamoja, na tutatoa jambo moja hata macommissioner nyinyi hamtakuwa na njaa kama hii ukishinda kutwa hapa bila kula chakula chochote kutoka asubuhi. Tungekuwa na mambo, tungemaliza mapema zaidi, na pia itakuwa kwamba representation, dhabiti itakuwa mzuri zaidi kwa sababu right now I can see kwamba nyingine presentation ndio katibu. Kwa hivyo kitu ingekuwa muhimu sana ningeona kama ingewezekana kwa upande huu kwamba tuanzie kutoka kijijini na pia Commission itusaidie kwa mambo mengine watume wao pale ili wazidi pia kuwaelezea wale watu na vile jinsi tunaweza kutengeneza hii Katiba kuanzia kijijini.

Pia ningeona kwamba hii Tume inavyoendelea kuna maneno mengi yanaongelelewa kwamba pengine haitaweza kumalizia kazi yake kufikia wakati wa uchaguzi. Kama haitafanyika ---

**Interjection:** Samahani Bwana Alex, tupe maoni ninaona kwamba hatumaliza. Tupe mapendekezo.

**Alex:** Kama mtakuwa mumemaliza tuseme kwa upande huu nilikuwa nasema tu pengine kwamba tunaeza kufanya only niseme

the minimum reforms ambazo zina uhusiano na uchaguzi kwa hivyo tuone kwamba zimemalizwa mapema.

**Com.:** -----------inaudible

**Alex:** Asante. Sasa naendelea na lingine nimeambiwa na ndugu yangu ya kwamba lazima Katiba itakuwa imemalizwa wakati huo. Hasa tuseme kwa Taita mimi ningeongea jambo lingine ambalo linatutatiza sana limetukwaza miaka mingi, na hata Wajumbe wetu washajaribu bungeni, tushasikia haya maneno mara nyingi about underground water katika hii lowland. Hizi sehemu za chini za Wundanyi hapa chini tuseme ndio hasa mahali sisi watu wa Pwani tunaeza kulima kwa sababu wajua hatuna mashamba hapa utakuta watu wako na kama robo heka, saa zinginie nusu heka, hasa kule chini ndio tunategemea zaidi, na hasa kufanya uchumi wa Wataita kuendelea. Serikali kama ingewezekana ifanye itusaidie hii mambo ya underground water ili tupate maji huko chini ingekuwa vizuri sana.

About Presidential powers, pia ningeona kwamba iwe reduced to the minimum. Iwe kwamba yeye ni kama mimi, tunatoshana na yeye. Halafu mshahara pia wa wabunge, huu mshahara wa bunge umezidi sana, lakini wengine walipoongea sitaki kuongea. Kuna msemaji mmoja ambao pia ameongea mambo mengine kama hii ya print pesa. Mimi naona ni kama tunapoteza pesa nyingi sana nchini, kwa print pesa kila baada ya President akiondoka. Tungefanya kitu kimoja, either tufanye kwamba kama ni mwanzilishi wa taifa tuweke ile picha yake ama sivyo tufanye kama tuangalie hawa patriotic people who fought for our country whatsoever au freedom fighters, tunaweza kuweka mmoja wao atakaa pale, kwa sababu sioni kwamba ina maana sana lazima kichwa cha mtu yule aliyeko hapo kiondolewe. Halafu hapa, kitu kingine naona kama Game Reserve, ningetaka Game Reserve pia iwe Taita na iwe National Park.

Employment: ingekuwa muhimu kwamba kila mmoja ambaye amesoma na akahitimu, kama ni college ameenda, kama ni shule ameenda, akasoma akahitimu, ni lazima ihakikishe kwamba mtu kama huyo ameajiriwa. Halafu tena mambo mengine, kama haya ya kupeana vyeo. Vyeo kama vikubwa vikubwa kama vile inavyokuwa katika Provincial Administration na nini whatsoever District level, zote zingekuwa zinaangaliwa kulingana na community. Every community should have have a fair share of the cake, maana naona hapa Taita sisi hatuna hiyo cake, ni kama wametunyima kabisa, hatuioni. Halafu tene lingine limeongewa ni about this local brew. Hii local brew ambao inaitwa muratina ama Matingas, kikwetu ni Matingas, wengine wanaiita mkangara na nini, lakini hiyo pombe mimi nishaionja na ninaijua vizuri sana, haina madhara yoyote na kulingana na zile pombe zingine ambazo tunaletewa kwanza kutoka huku juu, sehemu za Rift Valley, sehemu za Central zinakubaliwa, kuja kuuza hapa. They bottle them na tunaletewa. Mimi ningeomba kwamba Kenya Bureau of Standard wa-caution, waje wapime ile pombe na watuhakikishie kwamba kweli haina madhara yoyote. Na kama haina madhara, basi ifanyiwe mara moja iwachiwe watu waanze kunywa pombe yao. Na tuna Public Officers pia, ambao wanaweza ku-inspect pia, na wakathibitisha kwamba haina madhara yoyote kwa binadamu.

**Interjection (Com. Salim):** Samahani

Ningependa serikali ya majimbo. Halafu tena mshahara kama wa Local Authority. Councilor wanapewa mshahara mdogo ukilinganishwa na wa wabunge, Councilors wamekuwa victimized sana kwa kupitia wa upande wa pesa, hata wengi wao wanatusumbua hapa kwa sababu hawana pesa ya kujisaidia wala kufanya mchango wowote. Elimu, education, health na mambo mengine, ningeomba kwamba yawe free kwa kila mwananchi, maana vile tuliyoambia kutoka mwanzo wa serikali kuundwa Kenya, kulikuwa na free education na health facilities. During the National Convention, ambayo mtaifanya juu ya Constitution ambaye mumeandika pale katika kitabu mumetupatia cha Katiba, inaeleza kwamba only 25% wale ABC ndio watakuwa katika hilo eneo la huko juu kumalizia. Mimi ningeona hii namba, hii idadi ni kama ni kidogo. Ingeongezwa iwe around 50% whatsoever,r ili kwamba kuwe nawatu wengi wamewakilishwa katika nchi. Mimi ningeomba tena pia hawa nominated candidates, Parliamentary or civic candidates, hawa ningeona nominee zao badala ile pesa ambao wangelipwa kama nominated members, tupewe nafasi hapa, local people wachague hawa watu, wengine watakuwa kama ni extra na hiyo pesa ipewe hao watu kama mshahara. Lakini isiwe kwamba wamekuwa nominated by members of Parliament ama President. Ingekuwa kwamba wale walizaliwa kule wawachiwe nafasi wachague mtu ambaye ni nominated kama …….(inaudible) members na ile pesa ambaye nominated member alikuwa analipwa, alipwe huyo mtu.

Pia ningeona kwamba kuna wazee wa kijiji hapa, ma-chairman, na nini wanafanya kazi kubwa sana, hao pia ningeona Local Authorities ingepewa nafasi kwamba ipewe pesa fulani itengwe kwa wazee kama hawa ambao wanafanya kazi kubwa ambao wanaharakisha sana na maendeleo kwanza wao hapa ndio wana kazi kubwa wanafanya kwa vijiji na maendeleo yote ya vijiji hivi. Kwa hivyo wawe at least kitu kidogo kama (inaudible) -a up-keep yao. Pia ningeona lingine kwamba---

**Interjection (Com. Salim):** Samahani

**Alex:** Imebaki mbili tu. Wazee ambao wame-retire ama hawaku-retire, hawakufanya kazi ya serikali ama alikuwa kwa serikali, mzee yeyote ambaye amefikisha miaka sitini na kuendelea, huyo lazima aangaliwe na serikali, kulingana na maisha yake maana hajiwezi, huyo ni kama mlemavu kwa hivyo serikali izingatie kwamba inaweza kumsaidia ili aweze kuishi. Wanawake ambao mabwana zao wamekufa, na wako na watoto ambao bado wanasoma shuleni ama hawajaanza kusoma shuleni, na amekufa especially na ugonjwa wa HIV/AIDS, ningeomba kwamba serikali ichukue jukumu kwamba, hawa watoto walewe na maana mara nyingi both parents wamekufa. Kwa hivyo walewe na serikali na waweze kusomeshwa ili waweze kupata elimu maana makosa haikuwa yao. Hawa retrenched Officers, ningeomba kwamba anytime government ina-retrench watu, wawapatie pesa ya kutosha, maana hata wale waliopewa, sasa hivi wengi wameshamaliza hizo pesa hata wako na shida sana. Nafikiri kwa hayo nitamalizia hapo kwa sababu naona time imeisha. Asanteni.

**Com. Ratanya:** Asante Bwana Mwachio samahani. Sasa Bwana Jackson Mwangemi. Bwana Jackson utaongea kwa ufupi sana kabisa ukijua kwamba kuna wenzetu wengine hawajatoa maoni.

**Jackson Mwangemi:** Asante sana, kwa jina naitwa Jackson Mwangemi Waraka natoka Mtito wa Ndei nikiwakilisha wataita wale wanaoishi huko. Kulingana na muda, nilikuwa nimeandika mambo mengi lakini nitaongea machache kwa sababu mengi yameshazungumzwa. Kwanza nataka nizungumze juu ya kulinda mipaka. Mipaka ambaye inagawanya wilaya ningeomba iwe ikilindwa na kuheshimiwa kwa njia ya kuzuia visa vya makabila kwa sababu mara nyingi tunapata visa vya makabila kuzozana na hata na yakija kuangaliwa yanakutwa chanzo ni mizozo ya mipaka. Pale kama kwa mfano mpaka wa wilaya---

**Interjection:** ------------------- (inaudible)

**Mwangemi:** Pale Mtito wa Ndei tuna mgogoro wa mpaka, na umefikia sasa kama chuki baina ya Wataita na Wakamba, maana Wataita wakiweka kibao mahali mipaka ulipo.

**Interjection:** ------------------ inaudible

**Mwangemi:** Tunataka mipaka ambaye inagawanya wilaya iheshimiwe kwa sababu hakuna heshima pale kabisa. Jambo lingine pengine ningeliongezea kwa sababu baadhi ya yale ningekuwa naye yameshazungumzwa, ni kuhusu kiti cha urais. Kiti cha urais, naona kwamba makabila madogo hayana haki kwa upande huo. Ningeomba iaangaliwe kama merry-go-round, ili kwa mfano vile Central Province walipata na sasa Rift Valley Province wamepata, sasa province zilizo baki wapate nafasi kupiga kura na kupata Rais wao.

Number three ni Katiba ambayo inamlinda mwananchi. Katiba ikiwa ndio inayomlinda mwananchi na haki zake, ningependelea Katiba hiyo imwangalie mwananchi kwa mikono yote miwili, kwa sababu inaangalia mwananchi kwa upande wa mwizi peke yake. Kwa upande wa mchawi haimwangalii, na mchawi anaadhiri sana mwananchi wa kawaida katika shughuli zake za maendeleo. Kwa hivyo kwa upande wa mchawi naomba iangalie mwananchi kwa kupata usalama.

***Laughter:***

Jambo lingine ni kuhusu hao wazee wa vijiji, kwa mfano kama vile mwenzangu alivyozungumza aliyetangulia. Wazee wa kijiji wanafanya kazi nyingi na wanatumia muda mwingi na hawapati chochote, na kwa ujumla wao ndio wanaotegemewa kama kianzilishi cha maendeleo kuanzia vijijini. Kwa hivyo waangaliwe pia wawe wakipata kitu kidogo. Kwa hivyo singekuwa na mengi zaidi, kwa sababu yale mengine yameshazungumzwa, asante.

**Com. Ratanya:** Na sasa tutamwita Baria Mwanyota? Hayuko? Gideon Mwasingo.

**Gideon Mwasingo:** Basi kwa macommissioners, mimi ni Gideon Mwasingo, ninaenda haraka haraka kwa sababu ya wakati. Kwanza nina-recommend utangulizi wa Katiba, iweko kama vile wasemaji wa kwanza wamesema tuwe na utangulizi kama sisi wanakenya tumeunda Katiba ya kuangalia maslahi na maisha ya wananchi.

Two, system ya serikali, aina ya serikali tunayopenda. Mimi napendekeza Parliamentary system au majimbo na majimbo haya ni yale ya kufukuzara. Tunataka majimbo ambayo watu wata co-exist, watakaa kwa amani, kuendeleza maendeleo.

Three, President. Napendekeza President wa nchi awe na mamlaka kamili ya kutawala nchi hii. Lakini asiwe juu ya sheria na awe tena Commander in Chief of the Armed forces. Na President achaguliwe na wananchi.

Nne, ni Prime Minister. Katika hii system hii ya majimbo, napendekeza tuwe na Waziri Mkuu ambaye atakuwa na mamlaka juu ya serikali na aki-appoint mawaziri. Ministers. Mawaziri wapewe wadhifa wa uwaziri kulingana na ujuzi wao, kama minister wa agriculture kwa mfano lazima awe ana elimu kwa masomo hayo. Kenya Electoral system, yaani njia ya uchaguzi. Ili kupeana mwananchi wa Kenya au wananchi wa Kenya kila mtu nafasi, napendekeza kwamba ID cards zitumiwe badala ya voters cards, ili kupatia wananchi wengi nafasi wale ambao wamehitimu na wamekuwa na ID cards. ID cards zitumiwe badala ya voters cards. Rigging. Hii rigging ambayo imeharibu hasa kura ya uchaguzi, ninapendekeza kwamba kuwe na heavy penalty kwa wale ambao watapatikana wakifanya rigging na hii mambo ya kutegemea maboss wale kwenda bunge iwe ni kitu cha mwisho kulingana na uchaguzi ambao tutaenda yaani kila mtu apiganie haki yake ya kwenda bunge. Political parties. Hivi vyama vingi vimeundwa vingine viko ni vya kikabila na ninalipendekeza kwamba kuwe na checks and balances juu ya vyama hivi, ili vyama ambavyo vitakuwa vya kisiasa viwe, kwa sababu ambavyo vitapeana huduma kwa wananchi wote na sio ethnic basi kama vile vilivyokosaa, vya Wakikuyu na kadhalika. Kugawanya mamlaka. Ninapendelea kwamba mamlaka yagawanywe kwa province na madistrict ili madistrict yawe na power ya kutosha ya kuangalia rasilmali zao.

Judiciary; ninapendelea kwamba Judiciary iwe very much independent na iwe kwa protected kwa sababu ndio inaangalia sheria kwamba inahifadhiwa. Kwa hivyo iwe protected sawa sawa na iwe free from political interference. Judiciary. Na hapo hapo katika Judiciary kuna watu wengine wanahitaji msaada wa sheria. Ninapendekeza kwamba serikali itoe financial support kwa wale ambao wanataka ku-impose ya Constitutional rights. Re-cover gharama ambazo zinahusu mambo ya kisheria. Judges pia waandikwe na Commission, kuundwe Parliamentary Judicial Commission, ya kuteua majudge kulingana na uwezo wao. Court of Justice and ----------(inaudible) hii ni masilahi ya jamii na mahitaji yao. Serikali ihakikishe kwamba, ni wajibu wake kulinda mwananchi kwa kuwa na maisha yake, vile alivyoumbwa na Mungu, na ni haki ya mwananchi afanye kazi, apate chakula, awe na shelter, apate elimu na apate health care. Kwa hivyo katika sehemu kile nina-recommend, Serikali itoe free education ambayo ndio msingi wa maisha kwa elimu kutokea msingi wa primary school mpaka secondary school.

**Interjection:** Samahani Bwana Mwasingo ----------------- inaudible

**Mwasingo:** Basi wacha nimalizie na shamba. Kuhusu mashamba, ningetaka kusema ya kwamba tuwe na sheria katika hii Katiba mpya kwamba shamba za wataita zisitolewe kule na Commissioner of Land. Hivi nataka kusema ya kwamba local authority iwe na mamlaka kamili ya kusimamia mashamba yetu. Lastly but not the least, boundary zetu kama vile mwenzetu alivyosema, ziheshimiwe kwa sababu hivi sasa Taita imesukumwa mpka Mackinon Road na Taita imesukumwa mpaka hapa

……..(inaudible). Kwa hivyo kama serikali haitaangalia mambo haya basi kutaweza kutokea shida. Thank you very much.

**Com. Ratanya:** Sasa kwa kuwa muda wazidi kukua mfupi ningependa kujua nani ambaye akaliko hapa kisha tugawanye wakati uliobakia, kiti ya wale mlioko hapa. Hebu nione ni nani yuko hapa na nani hayuko. Sela Kakini yuko? Okay. Oliver Segena? James Mwashafu? Ameondoka? Ametoka? Okay. Silvesta Mwagine? Ameondoka. Jephita Lotodo? Nahashon Gadi? Yuko? Okay. Robert Masingo? Okay. Livingstone Mwadine? Pauline Mwabala? Hayuko. Raymond Mlaki, Patrick Mwachala? Dickson Kalange? Diana Mchale? Diana Mzera. Juma Asman? Mathew Mwabiri? Livingstone Mwanyota? Michael Mwaita? Joseph Mwachofi.

**Sarah Kachi:** Kwa majina naitwa Sarah Kachi. Kwa maoni ninatoa, natoa kwa niaba ya …….. **Interjection** ….(inaudible)

**Sarah Kachi**: Sarah Kachi Gatanga.. Kwa niaba yangu ninatoa hotuba kutoka kwa baba yangu, wazee na wananchi wote. Kwa sababu wananchi niko nao pamoja kila kabila na wale wanaoshindwa na neno la Bwana itawasaidia maana Yesu ni malaika wetu wa ulimwengu kila pahali. Kila mahali tuendapo ndani ya kanisa tunaona malaika lakini malaika hajui lolote. Lakini sisi watu wa Mungu tunajua yote, wema na ubaya. Sasa sisi tunapojua hayo, tunavuta yale mazuri. Hasa hapa tumeambiwa nyani amenusa uzuri wa kanisa na nyani ni kama mtoto wetu. Kristo llakini hatutaki aitwe nyani, tunataka aitwe mwana wetu Kristo, mzaliwa wa kwanza.

**Com. Ratanya:** Asante Bi Serah kwa maoni yako, tukiendelea mbele sasa tutamuita Rev. Ayo.

**Alfred Ayo:** Kwa majina Alfred Ayo, haya ndio mapendekezo niliyokuwa nayo kuhusu marekebisho ya Katiba.

1. Katiba ya Kenya isiwe inaruhusu tena Rais ama yeyote kuwa juu ya sheria.
2. Ninapendekeza serikali ya majimbo, ili kila jimbo lisimamie rasilimali zake; madini, wanyama, ardhi, mito, misitu ama mazingira kwa jumla.
3. Na miaka ya umilikaji wa ardhi kama ilivyokuwa, ipunguzwe na kuwa miaka hamsini. Umilikaji wa ardhi kama ranches.
4. Mtu yeyote atakayetambuliwa kwamba ameiba mali ya serikali, alazimishwe kurudisha, akishindwa kufanya hivyo mali yake yote itaitishwa.
5. Linalofuata ni kuhusu ma-chief na manaibu wao, wawe wakichaguliwa na wananchi wenyewe.
6. Linalofuata ni kwamba kuna kamati za vijiji na kamati za kusimamia vitambulisho ama vyeti hao wanafanya kazi ambayo haina malipo, wawe wakipewa marupurupu.
7. Wananchi wapatiwe mamlaka kamili kwa kuwaezesha kufuta kongozi waliomchagua ikiwa hatoi huduma ipasavyo.
8. Rais au yule atakayechaguliwa kuwa kiongozi wa taifa mara anapochaguliwa ajiuzulu na na kujiondoa kwa chama. Asiwe na chama.
9. Hali ya wabunge, ya kukae na kujiamulia mishahara yao wenyewe na kujiongezea vile wapendavyo, ile act na jukumu la

mishahara yao iachiwe serikali.

10. Mwisho ni kuhusu pension. Wale waliostaafu na wanaendelea kupata pension kama ni mume anapokufa bibi yake apewe pension mpaka na yeye afe. Kama ni mama amehitimu kupata pension na amefariki, atamwacha bwanake aendelee kutumia pension hiyo hadi afe. Hayo ndio mapendekezo niliokuwa nayo.

**Com. Ratanya:** Sasa Tutamuita Bwana Oliver Mwongelee. Dakika tano tu Bwana Oliver hasa kwa ufupi sana.

**Oliver Mwongele:** Jina langu ni Oliver Mwongelee. Yangu ni machache. Ninataka Katiba hii mpya iheshimu mwananchi. Iweze kuwa accepted Katiba imeheshimu mwananchi na Katiba ipatiwe wananchi kibao mbele kama hapa Taita, inaoneka wanyama ni muhimu kushinda wananchi, ndio maana wanyama wamepewa shamba kubwa kushinda wananchi. Ninataka Katiba mpya I-compell serikali iende kubuni kazi za kutosha, kila mwaka kwa vijana. Pia Katika i-compell serikali ku-create condusive atmosphere for foreign investors, and local investors to invest in Kenya and create jobs kila mwaka. Na tunataka Katiba mpya I-compell serikali ku-create agricultural based income generating produce in rural areas ili vijana wanaomaliza shule wapate kazi na vijana wa rural areas waache kuenda katika cities kutafuta kazi huko. Tunataka affirmative action kwa vijana. Nimesikia akina mama pia wanataka kuwa na affirmative action. Sisi vijana pia tunataka affirmative action, vijana waweze kuchaguliwa katika nyanja zote za uongozi nchini. Kuanzia juu mpaka chini. Kwa mfano kama hii Tume ya CKRC unakuta vijana hawako na hii Katiba mpya tunayoiunda ni Katiba ambayo inatakikana iangalie malengo ya vijana wa kisasa na vijana wajao na vijana ndio wenye kupata shida sana kwa ajili ya ukosefu wa kazi. Kwa hivyo vijana ndio wanajua uchungu wa vijana, naomba wawekwe mstari wa mbele waweza kuangalia haya mambo ya Katiba. Pia nataka ikiwezekana Local Government zetu ziwe empowered ili kuweza kufanya wale elected, elected individuals kama vile tuna Ma-diwani wawe wana uwezo wa kuwaajiri wafanyi kazi wa Local Government na kufuta. Mtu kama Town Clerk vile, awe anaweza kuaajiriwa na Council na kufutwa na Council na wafanyi kazi wengine. Mayors wawe wanachaguliwa na wananchi. Mayors wa Local Government na chairmen pia wachaguliwe na wananchi direct. Na P.C Provincial Commissioner awe anatoka kwa ile Province ambaye anasimamia. Na tunataka DDC isimamiwe na elected person, na sio watu kama D.C na watu wengine hivyo. Yangu ni hayo machache.

**Com. Ratanya:** Asante Bwana Oliver kwa maoni yako, na sasa ni Bwana

**Nahashon Ngari:** Kwanza kabisa napenda kupongeza ma-commissioner kwa kufika hapa, ili tutoe maoni yetu. Maoni yangu ni mafupi kwa sababu mengi yameshasemwa, jina langu ni Nahashon Ngari. Kwa hivyo watu wote na wanataita na wote ambao wamefika, mambo yangu ni haya tu, mambo yangu kwa ufupi.

Napenda Katiba itoe uwezo kwa wananchi wote. Mbunge akichaguliwa akiwa hafanyi wajibu wake kwa wananchi, arudishwe nyumbani. Rais asiwe na mamlaka zaidi, kwa sababu pengine wanazidi mpaka mpaka wananyanyasa wananchi. Hata kama wananchi hawamtaki lakini anazidi kuendelea.

P.C asiwe anatoka mkoa mwingine anafanya mkoa mwingine. P.C. atoke ule mkoa anafanyia kazi, atoke hapo hapo. Huyu P.C. pia awe amechaguliwa na wananchi. Chief achaguliwe na wananchi. Sub-chief achaguliwe na wananchi. Wazee wa kijiji wawe wakipata marupurupu kwa sababu wana kazi kubwa sana wanafanya hata kushinda machief na ma-D.C. D.C aadhirishe kufanya mkutano mara kwa mara kwa wananchi wale amewaakilisha. Kama hafanyi, wananchi wachukue hatua. Katiba itoe uwezo kulazimisha serikali kuwapatia wananchi matibabu wote kwa sababu tunaona kuna maskini wengi ambao hawawezi kuenda kwa matibabu. Wengi kama hapa Taita madaktari hatuna mahosipitali vile tunavyoongea hivi. Ukienda huko, dawa hakuna. Sasa je, maskini ataenda wapi? Kwa sababu kuna maskini wengi hapa Taita ambao hawawezi kuenda hospitali hana hata pesa ya kununu mafuta ya taa. Hata chakula anakosa, sasa huyo mwananchi ataenda wapi?

Haya Katiba, usalama wa mwananchi Katiba itoe usalama ya kuchunga wananchi. Unaona wananchi hawana usalama wa kutosha. Unaona kama mwananchi amefanya makosa unaona akienda katika kuona polisi anadhulumiwa. Kuna mtu ambaye ameshikwa na makosa akifika kule anapigwa mpaka anakufa. Haya magereza. Kuundwe Commission kama sasa Tume ya Katiba hii ya kuangalia magereza na kuangalia pay za police. Kwa sababu kuna wafungwa wengi wanakufa katika magereza, magonjwa yako mengi huko. Kwanza magereza hayangaliwi. Katiba itoe sheria, macommissioner waonywe na serikali, kila wakati wanaangalia hizo magereza, wafungwa wanateseka sana. Ni wengi wamekufa na hakuna kitu kinafanyika hasa Kenya hii.

Wabunge: Rais asiwe anatoa uwezo peke yake. Lazima apitishwe kwa wabunge wale tumechagua halafu wote wakubalie. Kuunda serikali. Tunataka serikali ya mseto kwa sababu mbunge ataenda pale amechaguliwa na mwananchi wa Kenya, kwa nini wanabaguliwa? Vyama, hatutaki vyama vingi. Tunataka vyama viwe kama ni vine au vitano isizidi hapo.

Upande wa dini. Tunajua kuna Biblia moja halafu kuna Koran moja. Madini haya yameundwa na yanaenda wapi? Tunataka madini yasiwe yanasumbua wananchi. Katiba iundwe madini yasiwe yakiundwa. Haya basi, serikali tunataka tuundiwe upande wa matibabu, wakati wanaajiri watu, waajiri watu ambao wamesoma, waajiri watu ambao wako na afya kwa hivyo tunasema wakati huu taifa limejaa na ukimwi, mtu asiajiriwe kazi kama ana ukimwi, kila mtu apimwe. Serikali haiwezi kukubali iajiri watu ambao ni wagonjwa. Madaktari watolewe waende katika kila wilaya watu wapimwe. Kama una ukimwi upewe kipande chako special. Kwa hivyo watu wengi wanakufa kwa sababu haujui kama wana ukimwi, hata mimi naeza kuwa na ukimwi lakini sijui kwa sababu hakuna madaktari ambao wanashughulikia wananchi kujua kwamba ana ukimwi ama hana. Haya serikali,

**Interjection**: (Inaudible)

**Speaker:** **N**aenda kumaliza sasa. Tunataka lazima katika kila wilaya kuwe na committee zimechaguliwa ambazo zinaangalia mambo ya ukimwi. Kama hapa Taita Hakuna, watu wengi wamekufa hapa watoto hawasomi wengine, hawana

chakula wameachiwa nyanya na mababu. Je huyu babu ataweza kusaidia hawa watoto? Serikali itafute Katiba na watu watiliwe hiyo mambo ili wale watu waliofiwa kwa ukimwi, watoto waweze kufuatiwa mpaka huko ndani ya vijiji. Na wakati wanafuatilia wahuzishe wazee wa mitaa pamoja na machief.

La mwisho, mimi napendekeza serikali ya mseto. Serikali iwe na waziri mkuu. Rais awe ni Rais wa Kenya yote, si Rais wa chama. Hatutaki Rais wa chama. Chama kiwe ni chama kinatafuta kura huko kwa wabunge lakini si wa urais. Urais uwe ni watu wote, kwa sababu Kenya ni moja. Halafu tena kama serikali itakuwa ya majimbo, Katiba itoe sheria ya kuchunga tusije tukawa na kabila inaweza kuinuka kimajimbo ianze kupigana na serikali kuu. Hayo yangu ndio ya mwisho. Nimeshukuru sana kwa kunipatia nafasi.

**Com. Ratanya:** Na sasa namwita Bwana Robert Masingo. Robert Masingo, dakika tatu tafadhali kwa ufupi kabisa.

**Robert Masingo:** Nasema asante sana, kwa majina yangu mimi ni Robert masingo na vile umesema kwa kifupi nitazungumza kwa kifupi na mengi ambaye ningezungumza yamezungumzwa. Mimi ---------------(inaudible) ni mtaita wa Wundanyi, nina haya ya kuyaeleza. Ninapendelea serikali ya majimbo. Mali za ardhi za Taita Taveta, mbuga za wanyama, madini, maji ya Mzima Springs yawe chini ya ulinzi wa Council ya Taita Taveta. Kulindwa kwa mpaka yetu, misitu na kazi. Wale wa lease sisirudishwe. Yale mashamba makubwa makubwa wakati muda wa lease ukiisha yaangaliwe Wataita wapewe sehemu ya kumiliki mashamba kama mashamba ya estates na kwingineko, yasitolewe na lease, kabla hazijachunguzwa kwa sababu ya wananchi wana haja na mashamba. Wapatiwe sehemu zingine kwa sababu zingine hawazitumii na zinakaa tu. Muda ukiisha wanapatiwa lease na sehemu ile inakaa. Kwa hivyo wataita ningelihitaji jambo hili liangaliwe na Wataita wapatiwe.

Uchimbaji wa madini, hasa ifanywe na Wataita wenyewe, kandarasi za Taita zifanywe na wataita wenyewe. Kura, wakati kura hizi ambazo zinafikia, kura ziwe za siri kuanzia mashinani kwa sababu kura zinafanywa za mlolongo na wakati huo, watu hawapati nafasi ya kupiga kura kwa njia ya heshima. Wanaangalia wale ambao wamekula chakula chao, lazima wawawekee kura, kukaa kwa kila mlolongo unasikia yake lakini kwa vile amekula basi anakaa pale. Kwa hivyo kura ziwe za siri. Watu walionyakua mashamba ……..(inaudible) badala ya kuuzia watu wanajinufaisha wao wenyewe. Kuna watu ambao walinyakua mashamba ambayo ni mali ilikuwa ya wananchi, na ardhi na wao walinyakua mashamba yale sasa wanaendelea kuuza kama mali yao.

**Interjection**: Pendekezo lako?

**Mr Masingo:** Pendekezo langu mashamba haya yarudishwe kwa wananchi.

**Interjection:** …. (Inaudible)

Na County Council iwe inasimamia watu wao. Namalizia hapo asante.

**Com. Ratanya:** Asante sana Bwana Masingo kwa maoni yako, tukiendelea mbele na kwa haraka kabisa maana wakati unazidi kupungua tutamwita Bwana Evanson Mwadime. Dakika tatu kwa ufupi kabisa.

**Evanson Mwadime:** Mimi kwa majina yangu naitwa Evanson Mwadime kutoka sehemu za Kigaro na siku ya leo nashukuru kwa nafasi hii hili niweze kutoa maoni machache kwa sababu mengi yamekwisha semwa. Mimi napendelea serikali ambayo ina nguvu na singependelea serikali ambayo haina nguvu. Serikali yenye nguvu ni serikali iliyo na Katiba yenye nguvu, iwe ya kwamba wakati wowote tunapozungumzia Katiba tunazungumzia serikali. Kwa hivyo mimi ningependelea ya kwamba uongozi wa nchi hii uwe wa chini ya watu ambao wanaweza kuongoza serikali sawasawa. Ningependelea Rais awe na uwezo ambo unaweza kumruhusu kuweza kutawala nchi hii bila maswali, kwa sababu wakati mwingi tunapokuwa na viongozi na hatuna uwezo hatutaweza kufanya serikali ama kufanya jambo lolote liweze kufanyika. Kwa hivyo tunazungumza ya kwamba Rais awe na uwezo.

**Com. Salim:** Tafadhali --------------- inaudible

Rais awe na uwezo wa kuweza kutawala nchi hii asiwe na uwezo wa kutumia kila kipengele na kuweza.
**Interjection**: ..(inaudible)

**Mr Mwadime:** Jambo lingine ambalo ningetaka kulisema hapa, ni kwamba tungependelea serikali ambayo inaheshimu maskini. Wakati mwingi tumekuwa na serikali ambayo haikuwa inadhamini maskini, na ndio tumekuwa na shida za kuweza kukutana hapa. Kwa hivyo kitu kilichoko ni kwamba serikali inayoheshimu maskini, ndio ambayo inayoweza kufanya nchi iweze kuenda mbele. Hiyo ndio hiyo kwa hivyo turegeshe vitu kama price control, virudi ili wale ambao hawajiwezi waweze kusaidika. Mambo ya cost-sharing vile tumezungumza ipate kuondoka maana haiwezia kutusaidia. Tunataka serikali ichukue nafasi ya kuelimisha watoto kwa free na health pia watu watibiwe for free. Kitu kingine ambacho ningetaka kukisema hapa ni kwamba, wakati watu wanapoenda retire wengine huwa ni professionals na wakati mwingi wanapotoka kazini huwa tunasahau kwamba wana uchuji wa kuweza kutumika katika nchi hii. Kwa hivyo tungependelea ya kwamba wakati watu wanapo-retire wapewe nafasi, wale professionals waweze kuzidi kusaidia wananchi pale mahali ambapo walifundishwe kufanya kazi.

Kitu kingine ambacho ningetaka kueleza maana mengi yameshazungumza sasa narudia ni kwamba kabla hatujafanya kitu kiwe law au kisheria ungepata wakati mwingine ama wakati mwingi wananchi tuweze kuhusishwa, maana wakati mwingine sheria zingine zinaundwa bila wananchi kuhusishwa na inakuwa ni matatizo kwa sababu hatuelewi ilikuwa namna gani. Kama vile mishahara ya wabunge kupandishwa na mambo mengine ambayo yanaamuliwa huko ambako sisi wenyewe wananchi hatupo. Na pia kitu kingine ambacho tungependelea kukieleza, ni kwamba tunataka kupatia responsibility mambo ya machokora kwa makanisa na watu ambao wanahusika na mambo ya religion. Tunajua ya kwamba wale ambao ni machokora wote ni watu wa Mungu. Na tunajua tunatoa fungu la kumi tunatoa mambo kama hayo. Nahitaji ya kwamba Katiba hii iweze kusukuma mambo

ya machokora kwa upande wa makanisa na madhehebu, ambayo yanasimamia mwananchi ili waweze kufanya kazi vile inavyotakikana. Kwa hivyo yangu ni hayo machache, singependa kuendelea sana, lakini ningependelea ya kwamba tuwe na serikali yenye nguvu na Katiba yenye nguvu. Asante sana.

**Com Ratanya:** Asante Bwana Mwadime na sasa tutamwita Bwana Herdson, hayuko? Johna Mzera.

**Mzera:** Jina langu ni Jonnah Mzera. Yangu ni machache tu, kwanza ni kuhusu wabunge. Naona wabunge wanaendeleza legalized corruption, kwa sababu wanaweza kuketi na kujiamulia juu ya mishahara yao. Ningelipendelea ya kwamba kuwe pengine na kamati ambayo itaweza kuketi na kujua mishahara ya wabunge na marupurupu yao. Kwa hivi sasa, nafikiri kuna tundu pahali ambapo inawaachia waketi, kama waajiriwa na wajipe mishahara wao wenyewe. Napendelea kama kungalikuwa na njia ya kuweza kuwapa wao mshahara badala wao kukaa na kujiamulia mishahara yao.

La pili, nitazungumza juu ya human rights of women and children. Hasa nitazuzungumzia juu ya watoto. Katika watoto naona kumepitishwa ya kwamba ikiwa mzazi ameshindwa kupeleka watotoi wake shule ataweza kufungwa kwa wakati ujao. Naona human rights imefanya vizuri ndio kwa jambo hilo kuwatetea wanafunzi, lakini dosari ni kwamba waliopitisha hawajajua ya kwamba watoto hawa wanapata shida kwa sababu ya economy. Hapo ndipo mambo kama haya yangetekelezwa.

Linalofuata ni kuhusu University loans kwa students wetu ambao wana-apply. Si wengi ambao wanapata hasa wale ambao wanatoka katika jamii maskini. Kuwe na njia ya kuweza kujua na wanafunzi wanaopita ili tusiwe na wowote ambao watakosa nafasi hii. Jengine ni kuhusu secondary education tulipopata uhuru najua kuna mahali ambapo mashule yalianzishwa mazuri mazuri kama Alliance na kadhalika mpaka sasa hakuna shulekama hizo katika district ingine. Sasa hapa kwetu kwa mfano hatuna, courts hatuna. Watu wanapopata kazi wengi wao ni wale wamepita vizuri. Nafikiri tumejiharibia ------------ (inaudible) job opportunity. Najua wakati huu wengi huwa wanapewa shahada. Lakini shahad zile kwa shule unakuta ya kwamba wanafunzi hawa wametoka mashule pengine ni ya harambee, mengine ambayo ni mabovu. Yule mtoto pengine ambaye amepita vizuri katika shule ile mbovu, that is the bright student, and should be given that job opportunity.

Lingine ambalo nitalizungumzia ni ……(inaudible) in our education system. Naona hasa hatujakuwa na ……..(inaudible), tumekuwa several changes kwa mfano hata mimi ninajua nimepitia teachings zimebadiliki mara nyingi sasa. Kuna wakati ……….(inaudible). Na katika mashule tukienda sasa nafasi utakuta vitabu vingi ambavyo viko vya------ (inaudible) na kila wakati mzazi analazimishwa kunua vitabu vipya ambayo inakuwa ni gharama kubwa kwake.

Lingine ambalo nitalizungumza ni about Administration and Provision. Tunajua katika nchi nyingi tuna upande mmoja, hatuii na wabunge pamoja na administration. Yaani nikisema juu ya administration nazungumza juu ya D.C, Chief na kadhalika. Pahali ambapo tuna true democracy vile watu wanazungumza ni kwamba tuna only one line. Tuna representative wa watu, hilo ningalipendekeza liwekwe kwetu sisi hapa Kenya.

Another one ambalo ningezungumza ni independent Judiciary, nalihimiza hili, nafikiri tuwe na total independent Judiciary tunaweza kuenda mbele. Lingine ni leadership ya DDC. Badala ya kuwa na D.C na chairmen napendekeza tungalikuwa na mtu ambaye anatoka katika area ile maana kutokana na DDC tunapata mikopo inatoka kwenye serikali, wakati mwingi mikopo haifikii lengo lake ambalo linatakikana. Na mwisho ninazungumzia juu ya taxation in Kenya, I think taxation is too high in Kenya, especially on some type of goods. Tukiangalia kwa mfano hasa beer yenyewe ambayo inauzwa, ina 125% or perhaps more tax wakati huu, 125%. I think this one is too high maana ingelikuwa imepunguzwa hata, yule maskini angaliweza pia kupata na kustarehe na mwenzake. Starehe sio kwa watu wakubwa tu peke yake, bali hawa, hata hawa wadogo pia wanataka. Ingalikuwa imepunguzwa na mambo hasa pengine yangekuwa mengine na kila mmoja angestarehe. Kwa hayo machache Mungu awabariki sana.

**Com. Ratanya:** Asante Bwana Mzera na naona tutaweze kumaliza in time na tutamwita Bwana Livingstone Munyota? Mwamota? Munyota. Karibu Bwana Mwanyota.

**Livingstone Mwanyota:** Mimi kwa majina naitwa Livingstone Mwanyota ningetaka kuchangia mambo kidogo juu ya Katiba tunayotaka. Katiba tunayotaka, ni Katiba ambaye inamheshimu kutoka cheo cha juu cha Rais mpaka chini mwananchi wa kawaida. Iwe ni kama amri kumi za Mungu ambazo hizo hazijali mtu mkubwa, mnyonge au akiwa na elimu.

Kitu cha pili ni juu ya advocates au mawakili. Mawakili tunataka waangaliwe wakati anamsaidia mteja katika kesi yake itakapokwisha, asipatiwe cheta ya mteja iende kwake bali chekiwe ipatiwe mteja, ndipo aende alipwe sawa sawa na mapatano waliokuwa nayo. Kitu kingine, kuna hii kutoa mimba. Wale wanaotoa mimba wanafanya makosa maana amri ya Mungu inasema usiue na hao wanaua. Wanatakiwa hawa waadhibiwe sawa sawa, ili wenzao wajifunze juu ya hao. Ikiwezekana hata wafungwe kifungo cha kumuadhibu kabisa.

Kitu kingine ni watu ambao wanaoajiriwa kazi. Kuna watu wanaoajiriwa kazi ambao hawana uchuji na tena hasa vile yeye anataka kufunzwa na wale wa chini yake, ambao anawasimamia kama wadogo wake na wao ndio wana uchuji. Sasa anapatiwa promotion tu kwa sababu yeye ni kabila fulani. Promotion isipatiwe kwa ukabila, ipatiwe kwa mtu aliye na uchuji wa kutosha

Jambo lingine Katiba ambayo tunayotengeneza sasa iangalie rasilimali za wananchi ambazo ziko katika sehemu ile kama Taita district ueona lake jipe, na lake chao. Hizi lazima zinaweza kula utajiri katika Coast nzima zikiwa zitaangaliwa. Zitolewe maji ili iende katika mashamba kwa njia ya chini ili watu wapate chakula cha kutosha katika sehemu hii. Ni hayo tu basi nimemaliza.

**Com. Ratanya:** Asante Bwana Livingstone Mwanyota kwa maoni yako mafupi na yenye maana. Na sasa Bwana Mathew Mwabiri, Mathew Mwabiri.

**Mathew Mwabiri:** Mimi kwa jina naitwa Mathew Mwabiri. Natoka Mbale. Mapendekezo yangu ni kama ifuatavyo. Huduma ambazo kwa sasa ziko chini ya mkuu wa sheria zitenganishwe, kwa mfano tuwe na mkuu wa sheria kwa serikali yaani Chief Legal Advisor. Pia tuwe na kiongozi wa mashamba ya umma sababu hii huduma yote inaita ---------(inaudible) ikiwa serikali imeshtakiwa, mkuu wa sheria ndio kiongozi wa mashaka na pia ndio mshauri mkuu wa sheria. Je haki itakuwa wapi? Jambo langu lingine ni baraza la mawaziri tukiwa serikali lisiwe na wabunge waliochaguliwa. Kiongozi wa taifa, yaani Head of state asiwe ndio tena kiongozi wa serikali yaani tuwe na Head of Government, na Head of state. Sababu ni kwamba kama kiongozia wa serikali amekosea ataenda kwa Head of state. Na ikiwa kama kiongozi wa serikali ndio head of state hatuwezi kumtoa makosa maana yeye ndio amekalia vyeo vyote viwili.

Pendekezo lingine, mkuu wa Police yaani Commissioner wa Police ateuliwe na bunge. Wengine hao vikosi kama vile vya GSU, Administration Police, vivunjwe, tuwe na kikosi kimoja cha Kenya Police, kwa sababu naona wananchi wengi wakiwa confused, huwa na wasi wasi na wanaogopa.

Pendekezo lingine, kusiwe na national cake hivi ninamaanisha -------------(inaudible) ambayo yanahusu mwananchi ufanyiwe mashinani. Kama hapa Taita tunafuga wanyama wa pori. Sisi ndio tupewe pesa halafu tuchangie kitaifa na kama pia kuna majani chai wachangie kitaifa. Sio pesa iatoke hapa iende huko Nairobi halafu isaidie kujenga taifa, haiwezekani. Sisi ndio tuchangie.

Pendekezo langu lingine Katiba ihakikishe maisha na uhai wa mwananchi, kwa kumfanya awe na moyo na pia fikira nzuri. Elimu ya kutosha na pia Katiba iwe inasaidia kuajiri kazi vijana kupata riziki. Pendekezo lingine, watakaoajiriwa kwa ofisi za umma na mawaziri na mabalozi wawe wakichaguliwa na bunge isiwe ni Rais. Pendekezo lingine makamu wa Rais achaguliwe moja kwa moja na wananchi. Asiwe anachaguliwa na Rais maana anaeza tumiwa. Maoni yangu, yangu ni hayo lakini natilia mkazo kitu kimoja, huduma za mkuu wa sheria zitenganishwe, tuwe na mkuu wa sheria, na pia kiongozi wa mashtaka yaani kuwe na Chief Legal Advisor na Public Prosecutor, maanake saa hii mkuu wa sheria ndio Public Prosecutor. Kwa hivyo ikiwa ninashtaki serikali nitakuwa nashitaki mkuu wa sheria na yeye tena ndio kiongozi wa mashtaki. Hakutakuwa na haki. Yangu ni hayo.

**Com. Ratanya:** sasa ni Bwana Joseph Mwachori. Dakika tatu tafadhali.

**Joseph Mwachori:** Mengi yamezungumziwa na wenzangu, kwa jina kwanza najitambulisha, jina langu ni Joseph Mwachori kutoka Mbale location. Mapendekezo katka Katiba hii ambayo tunaitaka kwa vizozi vilivyoko sasa na baadhi ya miaka hamsini ambayo vitakuja. Hali ya hapa Taita Taveta, wataita na wataveta, ardhi yao kubwa iko katika mbuga ya wanyama, tuko na kilometer elfu mbili na kumi na nane. Kutokea mwaka wa 1875 ndio wakoloni walitugawiya hiyo ardhi na kufikia sasa, Wataita wameongezeka mara ngapi, na hizo ndizo ziko za mababu zetu sasa. Sisi wengine ambao tuko hapa, hatuna kipande

ingawa hata nusu acre. Tunataka hizo acre elfu mbili na kumi na nane ziongezwe mara mbili kwa Katiba ya sasa. Vile vile kuhusu mapato yaliyoko katika shamba hii ya wanyama hawa wa pori, wataita na wataveta wanataka walipwe shilling million kumi kila mwezi kulingana na mapato hayo, kutoka kwa KWS maana hiyo ndipo kahawa yao na majani katika wilaya hii. Watumishi wanaofanya kazi katika idara hiyo, waweke wenyeji wa hapa wawe themanini kwa mia, katika ulinzi wa kuangalia hawa wanyama maana ni kahawa yetu. Pili walio sehemu za mkoa mwingine, walio themanini kwa mia wanachuna kahawa na majani pande zile. Watoto wa hapa wapate kuajiriwa.

Kuhusu serikali, mamlaka ya Rais yapunguzwe na vile vile kuwe na serikali ya mseto. Katika kila mkoa upewe mamlaka yake ya uongozi katika kuhudumia mali za asili zilizoko katika mkoa ule. 80% ya mapato yanayotokana na mkoa ule, yawekwe katika mkoa ule katika mfuko uliokomkoa wa Pwani, yaweze kustawisha sehemu zile kimaendeleo kwa maana rasilimali hizo ziliumbwa na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya watu hawa. Kwa mfano maji ambayo mwenzangu amesema kutokea chala Taveta na maji hayo, rasilimali hizo za pesa zikitoka maji kama hayo yanasambazwa ili mashamba, ---------(inaudible) katika viwanda vijana hawa wetu waweze kupewa mashamba, walime wapande pamba, mchele, ------------- mahindi kuliko kuletewa mahindi kutokea nje, na sisi tunataka wilaya hii itoe mahindi hapa ili wapewe wenzetu nje. Tunao uwezo, sio wavivu watu wa Pwani, lakini tungetaka hivyo.

Kuweko mfano katika Katiba hii. Wale ambao hawana kazi kuanzia watoto, akina mama na wazee wakongwe tufanye kama uingereza, kila mwezi wapatiwe sehemu fulani ya mapato za kumuezesha kula bila kukosa chakula maana wanastahili kuishi sisi hawa watu. La muhimu sana ni kuhusu viwanda. Katika mkoa wa Pwani, viwanda vilivoko katika humo 80% ya nafasi za kazi ipewe wakaazi wa huko, na 20% wapewe wakaazi kutoka mikoa mingine. Na vile vile mikoa mingine nao wafanye hivyo hivyo na itakuwa na usawa wa maendeleo. Walio bora wakiwa na aina zozote za mali ambazo wamerundika na mamillioni ya pesa pia, katika nchi za nje, zirudishwe hapa nchini Kenya, iweze kustawisha nchi hii. Asante kwa hayo naomba Mungu abariki Tume yetu hii na vile ikimaliza kuna hata mpango ambayo tuna sisi kidogo pia kila wilaya ipeleke watu watatu katika huko makao makuu ya kung'ang'ania mambo haya. Je sisi wazazi ambao pengine katika mapendekezo yetu ambayo tumepeana hapa, yanaweza kwenda kupuuzwa, kwani hata kama ni sungura ana haki naye kulindwa kama mnyama mkubwa vile vile. Kwa hayo machache Mungu abariki Tume hii na Kenya ibarikiwe na tupate nchi iliyo na ustawi.

**Com. Ratanya:** Sasa pengine naona tunaenda wa mwisho huyu Gibson lakini nasikia kuna mzee mwingine anataka kusema jambo. Okay, kwa hivyo Rev. uendelee uuna memorandum? Okay ni kuhighlight usisome yote lakini tupe tu maoni kidogo.

**Rev. Gibson Mwadime:** Asante sana macommissioner wetu, ningetaka kusema majina yangu ni Rev. Gibson Mwangai Mwadime kutoka ACK. Maoni yangu ni kwamba uchaguzi usifanyike kabla sheria hii kuu haija kamilika. Kwa hivyo tuhakikishe kwamba imekamilishwa ndipo uchaguzi uweze kufanyika ili kulinda viraka ambavyo vilizoko. Halafu Katiba iwe na mahali ya wananchi wenyewe na iwe ya kuinua wananchi.

Utangulizi: Ningependekeza kwamba preamble ambayo itatumika, ufanane na ya America. Inapendeza sana, na inajumuisha watu katika Constitution yake, kwa hivyo napendekeza ya Amerika iweze kuwa moja wapo. Halafu mamlaka kama wengine walivyosema yapunguzwe. Yaweze kuwa shared down katika viwango vyote. Halafu sheria zitakazo tungwa ziwe za usawa kwa watu wote. Tumepata wakati mwingine minister ameiba pesa nyingi, na mwizi wa mahindi anaadhibiwa vikali kuliko waziri. Kwa hivyo tuhakikishe ya kwamba sheria hiyo inafuata wote. Nilikuwa nikiangalia katika Section 14 hii one, two, three inam-favour President na mwananchi wa kawaida ananyimwa haki. Lengine ni katika Legal, katika vituo vyetu vya sheria. Ni kwamba kuwe na ruhusa, wakati mwingine tunapata shida, tunapata shida ya kuweza kuapa mbele ya Mungu. Kwa hivyo kuwe na affirmation, Watu waweze ku-affirm kwamba what they are going to say is nothing but the whole truth other than swearing. Kwa hivyo hilo liweze kuangaliwa.

Lingine ni kuhusu hii sheria inayosema ya kwamba leasehold iwe 999. I-skip from 99 halafu iende 999. That is unrealistic. Kwa hivyo hiyo iweze kuangaliwa iweze kuondolewa. Na lingine ni kwamba iwe minimal, iwe fixed pengine 60 pengine instead of 999 kama inavyosemwa sasa. Pia ardhi yangu niruhusiwe kuchukua hata chini, maana tunasikia ya kwamba below 6 feet, katika ardhisi yangu. Kwani naomba ya kwamba hizi sheria za mashamba ziweze kurekebishwa zote. Halafu ningeomba ya kwamba hizi basic human rights, hii chapter five ingeweza kuletwa mapema hata kabla mambo ya uongozi hayajaelezwa, kwa sababu ni za muhimi. Kwa hivyo zisitupwe mbali sana. Na ingine ni hili la watoto. Hii issue ya kwamba defilement inakuwa ni ndogo kidogo, ku-defile mtoto inakuwa chini kuliko rape si vizuri. Lazima hiyo ichukuliwe juu kuliko hayo mengine. Na mengine yameendelea kusemwa, pengine ningesema ya kwamba elimu hii ya citizenship ianzishwe kutoka standard one kuendelea mbele, ili watu waweze kujua haki zao kimapema.

Ningetaka kusema ya kwamba katika tolerance, kuwe na tolerance ya religion. Na nilikuwa nikisema kuhusu utumizi wa hii mitambo. Pengine kuwe na masaa ambayo ya kutumia hiyo mitambo haitaruhusiwa kama wakati wa usiku, lakini kutumia mitambo ni jambo ambalo ni nzuri. Nafikiri kwa sababu nime-promise kwamba kesho nitaweza kutumana hii kwa hivyo niruhusu niweze kukoma hapo. Mungu awabariki.

**Clapping.**

**Com. Ratanya:** Asante sana Rev. kwa maoni yako hayo na sasa nafikiri tumefikia mwisho wa maoni kwa leo, na tumesikia kwamba yuko mmoja wetu ambaye angependa kutoa maoni yake kisiri. Yuko hapo? Kwa hivyo ningependa kwanza kabla ya kukusikiza kuwashukuru wote wale ambao wamefika hapa leo kutoa maoni na pia ningependa labda tumalize kwa maombi. Rev. turahitajia msaada wako na baadaye tutakaa na huyu mwenzetu mmoja ambaye angependa kutoa maoni mengine kisiri. Kwa hivyo shukrani sana Mungu awafikishe nyumbani mwenu kwa usalama hivi leo, na kesho pia tutakuwapo hapa Wundanyi kwa kusikiza maoni ya watu. Tutakuwa Weruga nasikia, St. Paul Church kwa hivyo wale ambao hawajatoa maoni waweza kufika hapo kutupa maoni yao. Lakini kwa sasa tumalize kwa maombi na Rev. utatuongoza.

**Rev. Gibson:** Tuinamishe vichwa vyetu tuweze kuomba. Mwenyezi Mungu tunakushukuru kwa sababu umeweka nchi yetu katika kazi hii ya kihistoria ya kuweza kuandika Katiba. Tunawaombea Commissioner wote pamoja na chairman wao, Yash Pal Ghai, Bwana tunaomba enda ukawasaidia katika kazi hii ambayo ni ngumu na Baba wa mbinguni ili kwamba kabla ya uchaguzi tuweze kuwa na Katiba isiyo na dosari yoyote. Bwana uwalinde katika harakati za kusafiri uwapatie watu vizuri ili kwamba waweze kutoa mawazo yao. Tunaomba sasa eh Bwana tunapoenda Bwana amani yako ipitayo fahamu zote, izidi kutulinda na kutuhifadhi na kutubariki. Kwani tunaomba ni katika jina kuu la Yesu Kristo, tunaomba na kuamini, Amen. Tusema neema sote pamoja "neema ya Bwana ya Bwana Yesu Kristo na mapenzi ya Mungu Baba na ushirika wa roho mtakatifu uwe pamoja nasi sote sasa hata milele. Amen.

**Com. Ratanya:** Sasa tuko katika Taita Taveta District Wundanyi Constituency. Kuna mzee mmoja hapa ambaye angetaka maoni yake yasizikizwe na watu wengine na sisi kama Commission tunaweza kuchukua maneno yako bila kusikizwa na wengine, na halafu yawekwe kwa hiyo siri. Mzee umeniambia jina lako ni Romano Mwambingu, si ndivyo?

**Romano:** Mh
**Com. Ratanya**: wa Mwamburi?
**Romano:** Mh

**Com. Ratanya:** Na umesema ya kwamba ungetaka kusema maoni yako kwa Commission hii tume yetu ya kurekebisha Katiba bila kusikilizwa na mtu mwingine, ili tuweke haya maoni yako kama siri na wakati wa kutengeneza Constitution yaweze kuingia kama maoni yako. Umekubali hivyo?

**Romano:** Ndio

**Com. Ratanya:** Kwa hivyo utapewa nafasi ya kusema mambo yako kwa hiyo siri na nakuhakikishia kwamba Commission yetu itaweka mambo hayo kisiri kama vile unavyotaka na hayatachukuliwa watu wengine nje ya Commission. Ni Commission yenyewe itatumia. Lakini kwa ile njia ningetaka utumie mzee, kwanza utasoma maoni yako kama vile umeyaandika na tutayachukuwa hapa kwa tape recorder. Tutaenda na maneno ambayo yatakuwa recorded hapa pamoja na yale utaandika ndio tutapeleka kwa Commission ili yafanyiwe kazi. Tumekubaliana hivyo?

**Romano:** Ndio

**Com. Ratanya:** Kwa hivyo hapa anza na kusema jina lako na usome hayo yote umeandika. Kwanza pengine nimekwaambia jina langu, nimekwambia hapo mbele au unataka nirudie?

**Romano:** Uliniambia.

**Com. Ratanya:** Mimi jina langu naitwa Com. Domiziano Ratanya kwa Tume ya kurekebisha Katiba. Hiyo ni sawa sawa?

**Romano:** Ndio

**Com. Ratanya:** Kwa hivyo mpee sasa aendelee na wewe uanze na jina lako.

**Romano wa Mwamburi:** Mimi ni Romano Mwambingu wa Mwamburi kutoka ------------- village Ngerenyi sub-location Idaa ya Ngerenyi location. Maoni yangu. Ya kwanza mke hanipi ndoa na hataki mapatano kwa kanisa. Na kanisa halitoi talaka. Ya pili mke anaharibu jina langu, defamation of my character. Anahatarisha maisha yangu na hataki kuondoka au kuniacha. Wanangu waliomaliza form four wanahatarisha maisha ya nduguye. Niki-refer kuna watu waliopoteza maisha yao kupitia wanao na mke kama huyu wangu. Naomba Katiba ilinde hali hii, refer memorandum yangu nambari ishirini na mbili.

**Com. Ratanya:** Kwa hivyo mzee umemaliza, na haya maneno yako tutayachukua na tunasema asante sana. This is Com. Ratanya in Wundanyi constituency on Monday 29th April 2002. Thank you.

Meeting ended at 4.00 p.m.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**